Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

# BUNGE LA TANZANIA

## MAJADILIANO YA BUNGE

## MKUTANO WA KUMI NA TISA

**Kikao cha Saba - Tarehe 21 Aprili, 2005**

*(Mkutano Ulianza Saa Tatu Asubuhi)*

D U A

*Spika (Mhe. Pius Msekwa) Alisoma Dua*

## MASWALI NA MAJIBU

**Na. 88**

**Makao Makuu Dodoma**

**MHE. JANET B. KAHAMA** aliuliza:-

Kwa kuwa, Serikali kupitia Ofisi ya Waziri Mkuu imegusia kukamilishwa kwa mpango wa kuhamia Dodoma ukiwemo mpango thabiti wa kuendeleza Mamlaka ya Ustawishaji Makao Makuu Dodoma *(Capital Development Authority - CDA)* kwa kutenga Bajeti ili kuboresha miundo mbinu ya Makao Makuu na kutokana na kazi nzuri ya awali ya usambazaji wa mifereji ya maji taka *Storm Warm Water Drainage Sewage Dodoma*:-

Je, fedha zilizotengwa zitawezesha *Oxidation Pond* ifanye kazi yake sawa na kuwezesha mabwawa makuu yaliyojengwa kujaza maji ili kuwezesha *boating* na umwagiliaji maji katika bustani ufanyike?

**NAIBU WAZIRI WA KAZI, MAENDELEO YA VIJANA NA MICHEZO (K.n.y. WAZIRI MKUU)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kabla sijajibu swali la Mheshimiwa Janet Kahama, naomba kutoa maelezo yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli Serikali imejizatiti kutekeleza mpango wa kuhamia Dodoma ikiwemo kuendeleza mipango thabiti ya kuupitia upya na kuuboresha mfumo wa utekelezaji wa azma hii. Suala zima la uimarishaji wa miundo mbinu unasimamiwa na *CDA* na katika kuupitia mfumo wa utekelezaji, majukumu mengine ya uendelezaji wa miundo mbinu yamekabidhiwa kwenye mamlaka zinazohusika na utekelezaji wa masuala husika moja kwa moja. Kwa mfano, mifereji ya maji taka pamoja na mabwawa ya maji taka imekabidhiwa Mamlaka ya Maji Safi na Maji Taka mjini Dodoma *(DUWASA),* kwa uendeshaji na ukarabati.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo, sasa naomba kujibu swali la Mheshimiwa Janet Kahama, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kufuatana na hali halisi ya bajeti, katika miaka ya hivi karibuni, Mamlaka ya Ustawishaji Makao Makuu *(CDA)* haikuweza kupata fedha za miradi ya Maendeleo kutoka Bajeti ya Serikali. Hata hivyo, fedha zilizotengwa kwa mwaka 2004/2005 zimelengwa kwenye maeneo machache na zitaongezwa kadri ya fedha zitakavyokuwa zinapatikana.

**MHE. JANET B. KAHAMA:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, nina swali moja la nyongeza.

Kwa kuwa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania linapanuliwa na hivi karibuni litakuwa tayari. Vile vile kwa kuzingatia kuwa barabara ya Mwanza - Dodoma itakuwa imekamilika kwa kiwango cha lami na kutumaini pia barabara ya Arusha - Dodoma na yenyewe itakuwa ya kiwango cha lami hapo baadaye. Je, Serikali haioni sasa ni wakati muafaka kuhakikisha kuwa barabara zote za mji huu wa Dodoma zinawekwa na kukarabatiwa kwa kiwango cha lami?

**NAIBU WAZIRI WA KAZI, MAENDELEO YA VIJANA NA MICHEZO (K.n.y. WAZIRI MKUU):** Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba Serikali sasa inaona umuhimu wa kuongeza huduma muhimu za jamii katika mji wa Dodoma, si katika barabara tu lakini katika maeneo mengi. Kwa mfano, hivi sasa Wizara ya Ujenzi inahangaika kweli kweli kukamilisha nyumba za kuishi hapa hapa Dodoma. Wizara ya Maji na Maendeleo ya Mifugo tayari imeshawasiliana na watu wa *World Bank* kwa ajili ya kuisaidia *DUWASA* kwa kiwango cha jumla ya dola za Kimarekani 12,459,690. Kwa hiyo, kadri Bajeti itakavyokuwa inaruhusu kila Wizara kwa wajibu wake itakuwa inatekeleza lile linalokusudiwa ili kuufanya mji wa Dodoma uwe Makao Makuu kweli kweli na kuweza kuhimili vishindo vya watu watakaoongezeka.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Spika, napenda kuongeza majibu mazuri kabisa yaliyotolewa na Mheshimiwa Naibu Waziri, Mudhihir M. Mudhihir, kama ifuatavyo:-

Ni kweli kabisa Dodoma inastahili kuwa na barabara za lami hasa zinazounganisha Mikoa yote ili mji huu uweze kupanuka.. Wizara ya Ujenzi sasa hivi inafanya jitihada kubwa ya kuunganisha Arusha - Dodoma na Dodoma - Iringa na katika

utaratibu huo pamoja na kwamba sisi tunatafuta pesa za wafadhili na zetu lakini tuko tayari vile vile kupokea mtu yeyote ambaye yuko tayari kuwekeza katika *BOT* kwa barabara hizi.

**MHE. ISMAIL J. R. IWVATTA:** Mheshimiwa Spika, kwanza nakushukuru sana kwa kunipatia nafasi ili niulize swali la nyongeza lakini pia naishukuru Serikali kwa majibu mazuri.

Katika jibu la msingi ambalo Mheshimiwa Naibu Waziri amelitoa ameonyesha kwamba Serikali kidogo imekuwa na ugumu wa kuweka Bajeti ya kutosha kwa ajili ya Mamlaka ya Ustawishaji Makao Makuu. Kwa kuwa Serikali haijahamia Dodoma kutokana na kutokamilika kwa huduma nyingi katika mji huu. Je, hali ya kutotenga pesa za kutosha haionyeshi kwamba Serikali haina dhamira ya kutosha ya kufanikisha suala zima la uhamishaji Makao Makuu Dodoma? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA KAZI, MAENDELEO YA VIJANA NA MICHEZO (K.n.y. WAZIRI MKUU):** Mheshimiwa Spika, ukiangalia *CDA* peke yake unaweza kusema Serikali haithamini ukuzaji wa mji huu wa Dodoma lakini kwa kuwa Serikali imeamua kukabidhi baadhi ya majukumu kwa sekta husika moja kwa moja kama vile masuala ya maji na maji taka kwenda *DUWASA,* masuala ya makazi ya watu kukabidhiwa Wizara ya Ujenzi na upimaji wa viwanja kukabidhiwa Wizara husika ya Ardhi. Kwa hiyo, kwa kweli Serikali inafanya jitihada kubwa na kila anayeiona Dodoma sasa anaweza kuona kwamba Serikali inafanya kila jitihada za kuhakikisha kwamba mji huu unakamilika mapema iwezekanavyo ili kila inapowezekana Wizara moja baada ya nyingine ziweze kuhamia Dodoma kama zilivyoanza hivi sasa.

**WAZIRI WA MAJI NA MAENDELEO YA MIFUGO:** Mheshimiwa Spika, naomba niongezee majibu mazuri sana aliyojibu Mheshimiwa Naibu Waziri wa Kazi na Maendeleo ya Vijana, kama ifuatavyo:-

Tatizo la maji katika mji wa Dodoma tumelifuta. Mahitaji ya maji katika mji wa Dodoma ni galoni milioni 25 kwa siku tunazalisha galoni milioni 40. Kwa hiyo, tatizo la maji kwa Dodoma tumelifuta. *(Makofi)*

Na. 89

**Majengo na Matatizo Mbalimbali - Shule ya Msingi Kigoma Ujiji**

**MHE. DR. AMANI W. A. KABOUROU** aliuliza:-

(a) Je, Serikali inatoa kauli gani kuhusu kutumika kwa majengo ya Muumini yaliyokodishwa na Halmashauri ya Mji wa Kigoma Ujiji tangu mwaka 2003 ili yatumike sambamba na Shule ya Sekondari ya Kichangachui?

(b) Je, Serikali inasema nini kuhusu utaratibu uliotumika katika ujenzi wa Shule ya Msingi ya Rutale, Kata ya Kitongani Ujiji ambayo mpaka sasa haijaanza kutumika?

(c) Je, Serikali itakuwa tayari kufuatilia kwa karibu matatizo ya elimu katika Halmashauri ya Mji wa Kigoma Ujiji ambako kuna kila dalili ya mambo niliyoelezea katika swali hili yanayofanywa kwa makusudi ili watu wa Kigoma Mjini wasipate fursa ya kusoma na hivyo kutoshiriki kikamilifu katika masuala ya Serikali yao?

**NAIBU WAZIRI WA KAZI, MAENDELEO YA VIJANA NA MICHEZO (K.n.y. WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKAO NA SERIKALI ZA MITAA)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Aman Kabourou, Mbunge wa Kigoma Mjini, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, majengo ya Muumini ni majengo yaliyojengwa na yanayomilikiwa na *Muumini Islamic Centre* kwa lengo la kuendesha mafunzo yanayolenga kukidhi haja na malengo ya waumini wa madhehebu ya Kiislam. Majengo haya yapo karibu na Shule ya Sekondari ya Kichangachui iliyojengwa na Halmashauri ya Mji wa Kigoma Ujiji. Mwaka 2004, Halmashauri ya Mji wa Kigoma iliweka malengo ya kuandikisha wanafunzi 80 waliofaulu kuingia Kidato cha Kwanza kujiunga katika shule hiyo lakini kukawa na upungufu wa vyumba viwili vya madarasa. Kutokana na kufaulu watoto wengi na kutokuwepo shule ya karibu ya sekondari ambayo ingeweza kuwachukua watoto hao, Halmashauri ya Mji Kigoma Ujiji ililazimika kuingia mkataba na wamiliki wa majengo ya *Muumini Islamic Center* ili watoto hao waweze kuanza masomo.

(b) Mheshimiwa Spika, Shule ya Msingi Rutale ujenzi wake ulianza mwezi Machi 2004 kwa lengo la kupunguza msongamano wa wanafunzi katika Shule ya Msingi Ujiji. Ujenzi wake umetokana na fedha za Mpango wa Elimu ya Msigi (MMEM) Sh.12,400,000/= zilizotolewa na Serikali kukamilisha vyumba vinne. Shule ya Msingi Rutale haijaanza kupokea wanafunzi kama ilivyokusudiwa kwa sababu Kamati ya Shule hiyo iliongeza malengo ya ujenzi kwa kujenga ofisi mbili za Walimu hivyo majengo bado kukamilika. Kazi zilizobaki katika ujenzi huo ni pamoja na kuweka sakafu vyumba vyote na ofisi za Walimu, kufunga milango, kupiga ripu nje na ndani, kupaka rangi, kuweka mbao za kuandikia na kuweka kofia majengo yote. Jumla ya Sh.3,650,000/= zinahitajika kukamilisha majengo yote.

(c) Mheshimiwa Spika, napenda kumfahamisha Mheshimiwa Mbunge pamoja na Bunge lako Tukufu kuwa ujenzi wa shule za sekondari za kutwa pamoja na shule za msingi ni jukumu la wananchi wa eneo husika na Serikali hutoa mchango wake pale inapokuwa na uwezo. Napenda kumhakikishia Mheshimiwa Mbunge na Bunge lako Tukufu kwamba Serikali itaendelea kuchangia nguvu za wananchi popote ambapo wataonyesha kuchangia nguvu zao.

**MHE. DR. AMANI W.A. KABOUROU:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, napenda kuuliza maswali mawili madogo tu.

(a) Je, anafahamu kuwa hata baada ya kuingia mkataba kati ya Halmashauri na wamiliki wa shule hiyo ya Muumini mwaka 2004 na kulipiwa zaidi ya Sh. 4 milioni kukarabati majengo hayo mpaka sasa shule ile haijaanza?

(b) Je, Mheshimiwa Naibu Waziri anafahamu kuwa matatizo ya ujenzi wa Shule ya Msingi ya Rutale yaliyosababisha mpaka sasa isianze kufanya kazi na kama ni kweli ilitokana na kuongeza ofisi mbili za Walimu anajua kwamba shule hiyo inajengwa chini ya *DC* wa Kigoma na siyo Kamati ya Shule iliyochaguliwa na Halmashauri?

**NAIBU WAZIRI WA KAZI, MAENDELEO YA VIJANA NA MICHEZO (K.n.y. WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKAO NA SERIKALI ZA MITAA):** Mheshimiwa Spika, juu ya mkataba ambao unasemekana kwamba uliwekwa baina ya Halmashauri ya Mji wa Kigoma Ujiji pamoja *Muumini Islamic Center,* ni kweli yalikuwa ni makubaliano ya pande hizo mbili na yalikuwa ni makubaliano yenye nia njema ili kuweza kuongeza nafasi kwa vijana ambao wamefaulu. Lakini tatizo la kutokuanza kwa shule hiyo limo ndani ya Halmashauri kutokana na vitu vichache ambavyo vinatakiwa vimalizike.

Mheshimiwa Spika, upande wake Serikali unajitahidi kuiona Halamshauri ya Kigoma sawa na Halmashauri nyingine zote na ndio maana katika Mpango huu wa Kuendeleza Elimu ya Sekondari, Halmashauri ya Mji wa Kigoma Ujiji peke yake imetengewa milioni 49 lakini haziwezi kutoka bila kwanza wananchi kuchangia nguvu zao.Katika Mkoa huo huo wa Kigoma Wilaya nyingine kama vile Wilaya ya Kigoma mwaka huu wa 2005 inatarajia kujenga madarasa mawili, Kasulu matatu, Kibondo matatu wakati wenzetu wa Kigoma Mjini bado wana shule hiyo moja ambayo nayo haijakamilika vizuri. Kwa hiyo, namwomba Mheshimiwa Mbunge tushirikiane kuhamasisha wananchi wetu ili waweze kuchangia ujenzi wa shule hizi kama tunavyofanya katika Halmashauri nyingine zote.

Mheshimiwa Spika, shule ya Msingi Rutale imelazimika *DC* kuingilia kati baada ya kuona kwamba Kamati yenyewe imeshindwa kabisa kuhamasisha wananchi katika kukamilisha ujenzi huo. Kwa mfano, hizi milioni 12,400,000 zilizotumwa kama wananchi wangehamasishwa basi pamoja na nia nzuri ya Kamati ya Shule kuongeza malengo kwa kujenga ofisi mbili bado ingeweza kukamilika lakini nguvu za wananchi haziendi pesa hizi hizi ambazo Wilaya nyingine zinatosha kukidhi mahitaji zitakuwa hazitoshi katika Wilaya ya Kigoma Mjini.

Na. 90

**Uharibifu wa Mazingira**

**MHE. JOHN E. SINGO** aliuliza:-

Kwa kuwa, mazingira ya Tanzania sasa yanaharibika kwa kasi kubwa sana kutokana na umaskini wa chakula na kipato na kwa kuwa, umaskini huo umesababisha watu kuchoma mkaa na kuvuna mbao ovyo, kuchoma misitu, kilimo na ufugaji usiozingatia hifadhi ya ardhi na vyanzo vya maji na kwa kuwa, uharibifu huo wa mazingira umekuwa chanzo kikubwa cha mafuriko ya mvua na vimbunga vya upepo vinavyoharibu makazi ya watu, miundombinu ya barabara, reli, bomba na umeme; na kwa kuwa, mafuriko na vimbunga vinaliletea Taifa hasara kubwa ya fedha kila mwaka; na kwa kuwa, Wilaya ya Same ni moja kati ya Wilaya zilizoathirika sana na janga hilo katika sehemu ya Magharibi mwa Wilaya hiyo katika barabara kuu ya Dar es Salaam - Arusha:-

(a) Je, Serikali ina mpango gani wa kuinusuru Wilaya ya Same ambayo kwa miaka mingi sana imekuwa ikipata majanga ya mafuriko na vimbunga vya upepo na kusababisha hasara kubwa ya mali na uhai wa watu?

(b) Je, Serikali ina mpango gani wa kukabili umaskini wa chakula na kipato ambao umeonekana kuwa chanzo kikuu cha uharibifu wa mazingira unaofanywa na watu wetu?

(c) Je, Serikali ina mpango gani wa kulinusuru Taifa kwa ujumla na janga hilo la uharibifu wa mazingira hasa ikizingatiwa kuwa Tanzania sasa imeshika nafasi ya Rais wa Baraza la Mazingira Dunia?

**NAIBU WAZIRI WA MAJI NA MAENDELEO YA MIFUGO (K.n.y. WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kabla ya kujibu swali la Mheshimiwa Singo, napenda kutoa maelezo ya utangulizi kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli kuwa katika miaka ya hivi karibuni pamekuwa na ongezeko la majanga ya vimbunga na mafuriko yanayoathiri makazi ya watu pamoja na miundombinu mbalimbali nchini kote. Majanga haya pamoja na athari zake, kwa kiasi kikubwa yanasababishwa na ongezeko la joto duniani *(global warming).* Hali hii duniani inachangiwa na nchi zenye viwanda vingi kuendelea na shughuli za kiuchumi na kijamii zinazotoa gesi zinazoongeza joto duniani. Pamoja na sababu hizi, umbile tambarare asili *(natural flat terrain)* la Wilaya ya Same hasa Same Magharibi na sehemu nyingine zenye milima na miteremko mikali, hali ya ukame, pamoja na idadi kubwa ya mifugo, kwa pamoja huchangia uharibifu wa ardhi na hivyo kuzidisha kasi ya uharibifu kutokana na matukio ya vimbunga na mafuriko. Aidha kilimo kisichozingatia utaalamu maeneo ya milimani, hususani kwenye miteremko mikali huchangia kuharibika kwa mazingira. Kulingana na sensa ya 2002, Wilaya ya Same ina wakulima 211,738 na hufungua mashamba mapya kila mwaka. Tatizo hilo nalo huzidi kuchangia uharibifu wa mazingira. Aidha, Wilaya ya Same iko kwenye ukanda wa ukame, hivyo inapata mvua kidogo tu kama milimita 600 kwa mwaka. Hivyo, wakati baadhi ya sababu za uharibifu wa mazigira ziko nje ya uwezo wetu, nyingine zinatokana na namna tunavyoendesha shughuli zetu wenyewe.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo, napenda sasa kujibu swali la Mheshimiwa Singo, Mbunge wa Same Magharibi, lenye sehemu (a), (b) na (c) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Serikali imeendelea kuchukua hatua mbalimbali za kukabiliana na matatizo ya uharibifu wa mazingira katika Wilaya ya Same na kwingineko nchini kwa mfano:-

Kwa kupitia Wizara ya Kilimo na Chakula, Serikali inatoa huduma ya ugani kuelimisha wananchi kuzingatia kanuni za kilimo bora na kuongeza tija katika kilimo cha mazao ya chakula na biashara bila kuharibu mazingira. Aidha, Serikali inatekeleza Mpango wa Kuendeleza Sekta ya Kilimo Nchini *(Agricultural Sector Development Programme - ASDP)* ambao unalenga kuondoa umaskini kwa kukuza kilimo, kutoka kilimo cha kujikimu, kitoe ziada kwa ajili ya biashara. Katika msimu wa 2002/2003, Serikali iliipatia Wilaya ya Same Shs.11,434,743/= kununulia mbegu za mahindi kwa ajili ya maeneo ya umwagiliaji Ndungu. Msimu wa 2003/2004 Wilaya ilipata tani 20 za mbegu za maharagwe na tani 10 za mtama na Sh.1.0 milioni kununulia mbegu za mhogo. Kwa mujibu wa Mpango wa Maendeleo ya Kilimo wa Wilaya *(District Agriculturl Development Plans - DADP's)* ambao unalenga kuinua kipato cha wananchi, Serikali, kwa mwaka 2003/2004 pekee, ilitoa Sh.60,600,000/= za kukarabati miundo mbinu ya umwagiliaji na kuwawezesha wananchi kushiriki katika kusimamia utekelezaji wake.

Mheshimiwa Spika, mnamo mwezi Novemba, 2003, nilibahatika kushiriki katika warsha ya mazingira Wilayani Same, warsha iliyoitishwa na kugharamiwa na Kiongozi wa Kanisa Katoliki, Mhashamu Askofu Jacob Venance Koda. Warsha iliwashirikisha viongozi wa Vyama vyote vya Siasa Wilaya ya Same na Mwanga; watendaji ngazi ya kijiji hadi Wilayani, viogozi na waumini wa madhehebu ya dini mbalimbali ikiwa ni pamoja na dini za asili. Mikakati kadhaa ilibuniwa kuendeleza na kuhifadhi mazingira. Natoa wito kwa wakazi wa Same kushirikiana na Serikali pamoja na viongozi wa madhehebu mbalimbali Wilayani kutekeleza maazimio yaliyofikiwa na mikakati iliyowekwa. Vile vile Serikali imeiteua Wilaya ya Same kuwa moja kati ya Wilaya 27 nchini zitakazonufaika na Mradi wa Usimamizi Shirikishi wa Misitu *(Participatory Forest Management)* ulioanza Julai 2004. Katika kipindi cha mwaka 2004/2005, mradi utatoa zaidi ya Sh.60,000,0000/=. Elimu ya kuhamasisha matumizi ya majiko sanifu na namna ya kupata nishati mbadala itapewa kipaumbele ili kupunguza kasi ya kukata miti na kuchoma mkaa. Aidha Serikali, kupitia Wizara ya Maliasili na Utalii itaendelea kutekeleza mradi wa huduma ya ugani, sekta ya misitu kwa kuwashirikisha wananchi na kuhimiza upandaji wa miti maeneo yenye ukame kipindi cha mvua katika Wilaya ya Same.

**MHE. JOHN E. SINGO:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza maswali mawili ya nyongeza pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri.Kwanza naipongeza Wizara kwa hatua ambayo imeanza kuchukua kwa lengo la kunusuru uharibifu wa mazingira kule Same lakini pamoja na pongezi hizo nina maswali mawili:-

(a) Kwa sababu uko Mfuko wa Kuhifadhi Mazingira Duniani *(Global Envinromental Facility) je,* Mfuko huo utachangia vipi katika kuhifadhi mazingira yanayoharibika kule Same?

(b) Kwa kuwa Mheshimiwa Waziri amekubali kwamba wananchi wenyewe wamekuwa wakishiriki katika kuharibu mazingira kule je, Serikali inachukua hatua gani kwa ajili ya kuelimisha na kuwafundisha matumizi bora ya ardhi *(land use planning)?*

**NAIBU WAZIRI WA MAJI NA MAENDELEO YA MIFUGO (K.n.y. WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS):** Mheshimiwa Spika, katika jibu la msingi nimeeleza kwamba Serikali itatoa Sh.60 milioni katika kuchangia kuelimisha wananchi na mpango huu utahusisha matumizi ya majiko sanifu na kazi nyingine ambazo zinalenga kutunza mazingira. Kama ilivyoelezwa na kutokana na maazimio yaliyotolewa kwenye semina ambayo nimeieleza ni vizuri Mheshimiwa Mbunge wakishirikiana na wananchi waanze kuona kwamba tatizo hilo linalenga kuwaumiza wenyewe kama hawatakuwa makini na hawatafuata maelekezo ambayo yanatolewa na wataalam. Ni vizuri wananchi wote Wilaya ya Same wahusike na waone tatizo hilo sio tu linaathiri maisha yao bali linaweza kuwa na athari mbaya zaidi.

Na. 91

**Posho Kwa Askari Polisi**

**MHE. ALI MACHANO MUSSA** aliuliza:-

Je, Serikali inaweza kutueleza sababu za msingi za kutokamilika kwa posho ya Askari Polisi kama ilivyotakiwa mwaka 2003/2004?

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Ali Machano Mussa, Mbunge wa Tumbatu kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali huwalipa Askari Polisi posho za aina mbili. Aina ya kwanza ni posho zinazolipwa kupitia kwenye mishahara yao ikiwa ni pamoja na posho za upelelezi, msaada wa kodi za nyumba kwa wale ambao wanaishi nje ya kambi na posho ya ukufunzi. Aina ya pili ni ya posho ambazo hulipwa kwa kutumia fungu la matumizi mengineyo, *(OC)* ambazo ni pamoja na posho za kujikimu, nauli wakati wa safari za kikazi, posho za usumbufu na posho ya resheni. Kutokana na viwango hivi kupitwa na wakati ikilinganishwa na kupanda kwa gharama za maisha, Serikali imeandaa utaratibu za kuboresha viwango hivyo vya posho. Hata hivyo, mpango wa uboreshaji wa posho hizi za Askari haukutekelezwa mwaka uliotajwa na Mheshimiwa Mbunge mwaka 2003/2004 kutokana na ufinyu wa Bajeti. Aidha, Serikali itatekeleza mpango huo katika Bajeti zijazo kutegemea hali ya kuboreka kwa uchumi na ongezeko la makusanyo ya fedha za Serikali.

**MHE. ALI MACHANO MUSSA:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza maswali ya nyongeza pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri. Kwanza, kwa kuwa Maaskari Polisi mara nyingi wamekuwa wakilalamikia posho hizi na majibu yao huwa hawaridhiki na kwa kuwa Askari Polisi tunawategemea kutekeleza kazi zao vizuri zaidi ili kuhakikisha usalama wa raia na mali zao, tunawahitaji waendelee kufanya hivyo. Je, Mheshimiwa Waziri ili kupata majibu yenye uhakika na yanayoeleweka una mpango gani wa kufanya kikao cha pamoja kwa Maaskari ambao wako Mikoa mitatu ya Zanzibar kama ilivyo kawaida kwa Mawaziri kuwapitia watendaji wao ili wapate majibu ya kuridhisha na waendelee kufanya kazi yao vizuri? Pili, kwa kuwa Askari Polisi huwa wanashiriki katika kazi za kawaida unapotokea uchaguzi au mambo mengine kama wanavyopewa posho baadhi ya watendaji wanaposhughulikia masuala hayo na Askari Polisi hutakiwa walipwe. Je, unayo taarifa kwamba baadhi ya Maaskari hawajalipwa posho kama hizo na mpaka sasa wanaendelea kusubiri na hatima yake mara nyingine wanazikosa kabisa?

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Ni kweli Askari wanalalamikia posho zimepitwa na wakati, hilo nimeshajibu kwamba sasa tunafanya utaratibu wa kuziboresha. Lakini vile vile yako malalamiko ya kutolipwa posho zao za siku za nyuma. Kutokana na ufinyu wa bajeti tulikuwa tunadaiwa kwa miaka mingi sana, kuanzia mwaka 1994/1995 lakini tumekuwa tunalipa na tumeshalipa madeni hayo mpaka mwaka 2000. Sasa hivi Askari wanadai posho za kati ya mwaka 2000-2004 kiasi cha Sh.9bil ambazo zinatafutwa na watalipwa kwa sababu ni haki yao.

Swali la pili kuhusu posho za uchaguzi, kwanza kimsingi bajeti ya uchaguzi hasa wale maafisa mbalimbali wanaosimamia uchaguzi inasimamiwa na Tume ya Uchaguzi, wale wote ambao wanapigisha kura kwenye vile vituo, wanaolinda vituo. Ni kweli ilitokea hitilafu kwenye uchaguzi uliopita baadhi ya Askri hawakulipwa lakini Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ameshaelekeza kwamba sisi wenyewe ndani ya Wizara tutawalipa Askari hawa.

Na. 92

**Usikivu wa Simu za Mikononi - Kondoa**

**MHE. KHALID S. SURU** aliuliza:-

Kwa kuwa, nilimwandikia barua Mheshimiwa Waziri wa Mawasiliano na Uchukuzi kwamba, maeneo ya Kata za Kikore, Kisese, Masange, Bumbuta, Mnenia, Pahi, Busi, Kwa delo, Soera na Haubi bado hayajafikiwa na usikivu wa mtandao wa simu za mkononi kupitia mnara mkubwa ulioko mjini Kondoa kwa sababu ya vikwazo vya milima mirefu ambayo inafanya maeneo hayo kwa bondeni; na kwa kuwa, maudhui ya barua hiyo ya tarehe 6/9/2004 ni pamoja na kujengwa kwa mnara wa wastani kwenye mlima uliopo katika bonde au tambarare ya Kata hizo ili usikivu wa simu uwanufaishe wananchi kwa maslahi ya uchumi na maendeleo:-

(a) Je, ushauri huo ulizingatiwaje na ni hatua gani zimechukuliwa ili kuondoa utata huo?

(b) Je, hizo hatua zitakazokuwa zimechukuliwa ni pamoja na kufika kwenye mlima huo Mahongo kuthibitisha usahihi wa ushauri huo?

(c) Je, ni lini sasa usikivu wa simu hizo za mkononi zitakamata maeneo hayo niliyoyataja?

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI (k.n.y.WAZIRI WA MAWASILIANO NA UCHUKUZI)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kabla ya kujibu swali la Mheshimiwa Suru, napenda nitoe maelezo mafupi. Ili kutumia simu ya mkononi, ni budi mtumiaji wa simu awe katika eneo linalofikiwa na mtandao wa kampuni ya simu husika, yaani network coverage. Ili kuwafikia wateja wake, makampuni hujenga minara mbalimbali ambapo gharama ya mnara mmoja ni kati ya Sh.100 mil hadi Sh.350mil.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo, sasa napenda kujibu swali la Mheshimiwa Khalid S. Suru, Mbunge wa Kondoa Kaskazini, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Ushauri wa Mheshimiwa Mbunge ni mzuri, hata hivyo uamuzi wa kujenga minara hii katika eneo fulani hutegemea pamoja na mambo mengine ubora wa eneo husika kibiashara na urahisi wa upatikanaji wa njia za mawasiliano yaani *Transmission Links.*

(b) Mheshimiwa Spika, ili kuwezesha maeneo aliyoyataja Mheshimiwa Mbunge kupata mtandao makampuni husika pamoja na kutumia ramani mbalimbali hufika maeneo husika ili kuchukua vipimo mbalimbali. Kwa mfano *Vodacom* iko mbioni kuidhinisha ujenzi wa mitambo ya simu katika Mji wa Kondoa na eneo la Mingali lililopoKaskazini mwa Mji wa Kondoa. Inatarajiwa kuwa maeneo yaliyotajwa na Mheshimiwa Mbunge yana uwezo wa kupata mawasiliano mitambo hiyo itakapojengwa.

(c) Mheshimiwa Spika, kimsingi maeneo aliyoyataja Mheshimiwa yanaweza kufikiwa kwa simu vizuri hapo mitambo ya simu za mkononi itakapojengwa katika naeneo hayo. Mwisho ningependa kuwashukuru Wabunge wa Kondoa Mheshimiwa Suru na Mheshimiwa Degera kwa jinsi wanavyofuatilia kwa makini huduma za mawasiliano katika Wilaya ya Kondoa.

**MHE. KHALID S. SURU:** Mheshimiwa Spika, kwanza nakushukuru kwa kunipa nafasi niweze kuuliza maswali mawili mepesi mepesi ya nyongeza.

(a) Kwa kuwa Mheshimiwa Waziri au Serikali imezingatia barua yangu niliyoiandika kwa ajili ya kufikisha simu katika kata nilizozitaja. Kata ya Kikore, Kisese, Masange,

Bumbuta, Mnenia, Pahi, Busi, Kwa Delo, Swera na Haubi. Je, Waziri sasa kwa sababu kuna Makampuni yanapeleka mtandao pale atasimamia ili simu zifike kwenye Kata hizo?

(b) Hapa kwetu Tanzania upigaji wa simu ni ghali sana kuliko hata nchi nyingine kama Kongo, Kenya na kadhalika. Je, ni kizuizi gani hasa au kigugumizi gani kinaipa Serikali kushindwa kupunguza gharama za upigaji simu hapa Tanzania?*(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WIZARA YA MAMBO YA NDANI YA NCHI (k.n.y WAZIRI WA MAWASILIANO NA UCHUKUZI):** Mheshimiwa Spika, napenda kujibu maswali mawili ya Mheshimwa Suru kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kama nilivyoeleza katika majibu yangu ya msingi kwamba baada ya Mheshimiwa Mbunge kuleta barua yake kwamba maeneo hayo yanatakiwa yapate simu Serikali imewasiliana na makampuni mbalimbali na makampuni ya *Mobitel, Vodacom* na *Celtel* yako tayari na kwa kweli mwezi Mei wanaanza kwenda kufanya tathmini ya hali ya soko katika maeneo hayo aliyoyataja lakini pamoja na maeneo ya Farkwa na maeneo ya Kwamtoro, yote haya yatafanyiwa tathmini ya soko na hali ikiwa nzuri watafika kule na sisi Serikali tutaendelea kusimamia.

Kuhusu gharama za kupiga simu, Mheshimiwa Mbunge amesema ni aghali na ni kweli kwamba kuna malalamiko mengi ya wateja lakini suala hili linashughulikiwa na Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania na sasa hivi tunapozungumza mazungumzo yanaendelea na wamewekeana ratiba katika makampuni yote haya ya simu taratibu na ratiba ya kupunguza hizi gharama. Kwa hiyo, nataka kulihakikishia Bunge lako Tukufu kwamba Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania inashughulikia suala hili kwa ukamilifu.*(Makofi)*

Na. 93

**Gharama za Matumizi ya Simu za Mkononi.**

**MHE. HERBERT J. MNTANGI** aliuliza:-

Kwa kuwa Kampuni nyingi za Simu za mkononi duniani zinapanga gharama za matumizi ya simu hizo kwa kipimo cha Sekunde badala ya dakika kama ilivyo kwa baadhi ya Kampuni hapa Tanzania, kwa mfano, katika mfumo wa dakika, mteja akituma muda wa dakika moja na sekunde analazimika kulipia muda wa dakika mbili yaani ziada ya sekunde 40 ambazo hazikutumika.

(a) Kama hivyo ndivyo, Je, kwa kufanya hivyo si kwamba Kampuni hizo zinajipatia fedha za ziada bila gharama na hivyo kuwaumiza wateja wao?

(b) Je, ni lini Kampuni hizo zitabadilisha mfumo huo ili wateja walipie gharama halisi kwa muda halisi uliotumika?

**NAIBU WAZIRI WIZARA YA MAMBO YA NDANI YA NCHI (k.n.y WAZIRI WA MAWASILIANO NA UCHUKUZI):** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Herbet James Mntangi, Mbunge wa Muheza, lenye sehemu (a) na (b) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Nakubaliana na Mheshimiwa Mbunge kwamba kampuni nyingi za simu za mikononi duniani zinapanga gharama za matumizi ya simu hizi kwa sekunde badala ya dakika. Kulipia kwa dakika kunaweza kuwaumiza wateja kwa kutozwa gharama ambazo si za muda halisi waliotumia.

Mheshimiwa Spika, Makampuni yetu ya simu za mkononi yalishindwa kupanga gharama za matumizi ya simu kwa kipimo cha sekunde kutokana na teknolojia waliyokuwa nayo wakati ule ya kuendesha mitambo ya simu.

Hata hivyo, napenda nichukue fursa hii kulitaarifu Bunge lako Tukufu na wananchi wote kwa ujumla kwamba serikali kupitia Mamlaka ya Mawasiliano imekwisha chukua hatua madhubuti ya kulitatua tatizo hili. Hivyo, hivi sasa makampuni yote ya simu za mkononi yanatoza gharama zao za simu kwa sekunde badala ya dakika.

**MHE. HERBERT J. MNTANGI:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, lakini ningeomba kuuliza maswali mawili madogo ya nyongeza.

Kwa kuwa, teknolojia iliyokuwa iliyokuwa ikitumika hapo awali ilisababisha watu wengi kulipa fedha nyingi kwa muda ambao hawakuutumia na kwa kuwa sasa teknolojia imebadilika. Je, Mheshimiwa Waziri haoni kwamba Kampuni hizo zina haja sasa ya kufikiria namna ya kuwafidia wananchi ambao walipoteza hela nyingi kwa wakati ule?

Mheshimiwa Spika, Swali la pili. Kwa sababu sasa mtandao wa simu umefika katika naeneo mengi sana vijijini lakini wananchi wa vijijini wanashindwa kutumia simu hizo kutokana na gharama kuwa kubwa na kwa sababu ya kiutaalam jinsi unavyokuwa na soko kubwa ndivyo gharama zako zinavyoweza kuteremka, Je, kampuni hizi hazioni sasa kwamba ni vima zikateremsha gharama zao ili watumiaji wakaongezeka na wakaendelea kupata faida? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WIZARA YA MAMBO YA NDANI YA NCHI (k.n.y WAZIRI WA MAWASILIANO NA UCHUKUZI):** Mheshimiwa Spika, napenda kujibu maswali mawili ya Mheshimiwa Mntangi, Mbunge wa Muheza, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kama nilivyoeleza katika jibu langu la msingi kwamba hapo awali haya makampuni yalikuwa na teknolojia ya kizamani kwa hiyo bei zao walikuwa wanatoza kwa dakika hata kama wewe utazungumza kwa sekunde sasa hali hiyo ilijitokeza kwa sababu teknolojia ya wakati huo ilikuwa vile, sasa hivi tumepata

teknolojia mpya sasa kuanza kusema walipe fidia ama kuwatoza faini kwa hali ambayo ilisababishwa tu na teknolojia ya wakati ule, kwa sababu teknolojia inakwenda inaendelea kwa hiyo, tushukuru tu kwamba sasa na sisi tumeingia katika teknolojia mpya kupitia katika haya makampuni.

La pili kuhusu mitandao vijijini kwanza kwamba gharama ni kubwa kama nilivyosema katika jibu langu la awali kwamba suala la gharama sasa hivi liko mikononi mwa Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania linajadiliwa na linafuatiliwa kwa lengo la kupunguza hizi gharama. Lakini tatizo la vijijini pengine siyo gharama ila kutokupata mitandao yenyewe, vijiji vingi sasa katika Majimbo yetu vinatamani sana na vyenyewe vipate mitandao ya simu hizi lakini havijafikiwa nadhani hilo ndilo tatizo kubwa la Serikali na inashughulikia tatizo hili kwa maana ya kuanzisha, kama juzi tulipopitisha mfuko wa Umeme Vijijini vilevile Serikali inaandaa Sheria ya kuweka mfuko mwingine kwa ajili ya kusambaza simu vijijini.

Na. 94

**Ujenzi wa Barabara ya Dar es Salaam - Kibiti - Lindi**

**MHE OMAR S. CHUBI:** Kwa kuwa hivi sasa kuna mradi kabambe wa ujenzi wa barabara ya Dar es Salaam - Kibiti - Lindi na kwa kuwa, mradi huo unarahisisha kampuni tofauti kama vile kampuni ya Kichina inayojenga barabara toka Somanga - Matandu, na kampuni nyingine ya Kichina inayojenga toka Nangurukuru hadi Mbwemkuru na kampuni ya Kiarabu inayojenga toka Mbwemkuru hadi Mingoyo:-

(a) Kwa kuwa, wajenzi hao ni binadamu wenye utashi na inaonekana kuwa wameshazaa watoto chotara na binti zetu katika maeneo hayo. Je, mradi ukiisha watoto hao walalelewa na nani?

(b) Je, isingekuwa jambo la busara kama wenye mikataba wangekuwa na kifungu cha *contingency* sawa na asilimia 20 ya fedha za mradi wote kwa ajili ya matunzo ya watoto hao na gharama nyingine?

(c) Kama haiwawezekani, Je, Waziri mwenye dhamana ya ujenzi atakuwa tayari kulipa fidia kwa walioathirika na tatizo hilo?

**NAIBU WAZIRI WIZARA YA UJENZI (K.n.y WAZIRI WA UJENZI):** Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Omar Said Chubi, Mbunge wa Kilwa Kaskazini, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, suala la mabinti waliopo maneo ya miradi kuamua kuzaa na wageni ambao wanajua kuwa wapo hapo kwa muda ni la utashi pia kwa mabinti wenyewe. Hivyo ni jukumu la hao mabinti kuwajibika kuwalea watoto iwapo waliozaa nao hawataendelea kuwatunza baada ya mradi kukamilika. Aidha ni wajibu wa jamii husika kuwaelimisha Mabinti madhara ya vitendo hivyo ambavyo baadaye vinasababisha maisha magumu kwao siyo tu kwa kutokana na uhusiano na wageni bali pia na

Watanzania wenzao. Jambo kubwa la kuepuka hilo ni kutumia kinga ambayo itazuia mimba na UKIMWI. Inafaa dada zetu tuwape elimu hiyo. *(Makofi)*

(b) Mheshimiwa Spika, mikataba ya ujenzi wa barabara haitengi vifungu kwa ajili ya matunzo ya watoto. Naomba nirudie sehemu hii mikataba ya ujenzi wa barabara haitengi vifungu kwa ajili ya matunzo ya watoto, kwani jambo hili ni la kibinafsi na wala halihusu mkataba husika. Ni jukumu la mfanyakazi husika wa mkandarasi kutenga kiasi fulani cha mshahara wake kwa ajili ya matunzo hayo ya watoto.

(c) Mheshimiwa Spika, Wizara ya Ujenzi haipo tayari kulipa fidia kwa walioathirika na tatizo hilo na nawashauri watakaoathirika na tatizo hilo, wawasiliane na Wizara inayohusika na Ustawi wa Jamii. Wizara ya Ujenzi inaamini kuwa na watoto si kuathirika bali ni mpango halisi. *(Makofi/Kicheko)*

**MHE. OMAR S. CHUBI:** Kwanza pamoja na kuishukuru Wizara kwa kumaliza barabara katika eneo ambalo nawakilisha na Mheshimiwa Rais aliifungua tarehe 23 Machi, 2005 lakini niseme tu kwamba mbona Wizara inapojenga barabara huwa wanalipa fidia kwa mazao kama mikorosho, minazi na mazao mengine. Sasa inakuwaje katika hili watutupie sisi viongozi ambao tunawajibika kwa sababu tunaombwa hela ya maziwa na watoto wenyewe hawaeleweki? *(Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, swali la pili, inatokea kwamba hawa makandarasi wakimaliza kazi wanavunja yale maeneo na vitu vyote wanachimba mashimo wanafukia. Sasa je katika makubaliano kwa mfano walipojenga majumba isingekuwa vema hata yale mabati wanayovunja kuwaachia wananchi kwa bei nafuu hata kuwauzia bati moja kwa shilingi 5,000/= badala ku-*destroy* kazi nzima. Wizara haiwezi ikafanya msimamo hasa ikizingatia hasara nyingi tunapata? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WIZARA YA UJENZI:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Chubi, kama ifuatavyo:-

(1) Mheshimiwa Spika, ni sheria ya ujenzi inayosema wazi kwamba kama zipo mali katika barabara iliyopima upya , na watu hao wanaokaa kwenye mali hiyo iliyoko kwenye barabara ni ya mtu binafsi na barabara ndio inamvamia badala wao kuvamia *road reserve* basi lazima mali hiyo izidiwe. Lakini binadamu aliyokuwepo katika mazingira hayo ya barabara hahusiki kufidiwa yeye binafsi. Kwa hiyo, suala la kuombwa maziwa kwa viongozi mimi ninafikiri ni utaratibu wa kawaida tu Waheshimiwa Wabunge tunautumia kwamba wananchi wetu wakija wakiwa na matatizo wanatuomba tuwasaidie. Kwa hiyo, Mheshimiwa Mbunge endelea kusaidia kutoa maziwa. *(Kicheko)*

(2) Kuhusu kuvunjwa kwa kambi kwa kawaida kambi zinazotengeneza barabara, majengo hayo ni mali ya Serikali kama wajenzi wanavunja majengo hayo wanakosea wanatakiwa wayarudishe kwa regional manager ili regional manager watumie inavyotakiwa. *(Makofi)*

Na. 95.

**Malalamiko ya Wafanyakazi wa Tanzania Elimu**

**MHE. DR. WILLIAM F. SHIJA** aliuliza: Kwa kuwa, Serikali inao utaratibu wa kuchunguza kwa makini na kufuatilia ili kujua ukweli wa malalamiko ya wananchi na kuwapa haki yao kama ilivyofanya kwa wafanyakzai wa Jumuiya ya Afrika Mashariki na wengine wengi:-

(a) Je, kwa nini malalamiko ya wafanyakazi waliokuwa Shirika la Elimu Tanzania *(Tanzania Elimu Supplies)* yamepunguzwa?

(b) Je, ni nini hatma ya mali nyingi isiyoondosheka ya Shirika hilo?

(c) Je, kwa nini mapato ya mali hizo za *TES* yasitumike kuwalipa haki za mafao ya wafanyakazi hao waliotumikia Shirika kwa miaka mingi ikiwwa ni pamoja na kutunza mali hizo.

**WAZIRI WA ELIMU NA UTAMADUNI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Dr. William Shija, Mbunge wa Sengerema, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, ni kweli kuwa Serikali inaoutaratibu wa kuchunguza kwa makini na pia kufuatilia kujua ukweli wa malalamiko ya Wananchi ili kuwatendea haki raia wake wote; na hivyo ndiyo ilivyofanyika kwa malalamiko ya Watumishi wa *Tanzania Elimu Supplies (TES).*

Shirika hilo lilikabiliwa na matatizo makubwa ya ukata, kiasi cha kushindwa kuendesha shughuli zake za uzalishaji mali na kuwa na madeni makubwa yasiyolipika. Kutokana na matatizo hayo *TES* kuanzia Mei 2003 iliwekwa chini ya Mufilis; na Serikali ilichukua hatua ya kulipa madeni ya mafao yakiwemo ya *PPF* na kuwalipa Watumishi haki zao stahili kama ifuatavyo:-

* Mshahara wa mwezi mmoja badala ya notisi;
* Mshahara badala ya likizo ya siku 28;
* Nauli ya Mtumishi na familia yake;
* Nauli ya mizigo kulingana na ngazi ya Mtumishi;

* Mafao ya *PPF* badala ya Serikali kulipa deni la mchango wa *PPF* zaidi ya shillingi milioni 900 uliokuwa umekusanywa kutoka kwa wafanyakazi ukatumiwa na shirika. Jumla ya mafao waliolipwa wafanyakazi wa *TES* ni shilingi 324,523,989/=.

(b) Mheshimiwa Spika, hatma ya mali isiyoondosheka ya *TES* iko chini Mufilisi aitwaye *LART* kirefu chake *(Loans and Advances Realization Trust).* Kisheria Shirika likiwa chini ya Mufilisi mali zake lazima kwanza zitumike kuwalipa kwanza wadai. Hivi

sasa mali kama vile nyumba za Shirika hilo zimekwisha kutangazwa kuuzwa kuptia *LART*.

(c) Mheshimiwa Spika, kama nilivyosema katika sehemu (b) ya jibu kuwa Shirika likiwa chini ya Mufilisi mali zake haziwezi kutumiwa kwa shughuli nyingine zaidi ya kuuzwa na kulipa wadai. Kwa hiyo, mapato ya mali hizo hayawezi kutumika kulipa mafao ya wafanyakazi ndiyo maana Serikali kwa kuzingatia ukweli huo iliamua kubeba Serikali yenyewe jukumu la kuwalipa wafanyakazi haki zao za msingi badala ya kutegemea mali za Shirika ambazo zimekwisha kufilisiwa.

**MHE. NJELU E. M. KASAKA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kuniona. Mimi nilitaka tu niulize kwamba hivi karibuni madai ya wafanyakazi waliopo katika mashirika mbalimbali yamekuwa ni mengi, hilo shirika la elimu ni mmojawapo tu lakini kuna hawa wafanyakazi wa Jumuiya ya Afrika Mashariki iliyovunjika, kuna *Ubungo Farm Implements (UFI)* na mashirika mengine.

Je, Serikali inatamka nini katika kuwalipa hawa watu na kufuta kabisa malalamiko haya na kuondolea matatizo ambayo yanawapata wafanyakazi wa mashirika yaliyokuwa ya Serikali zamani.

**WAZIRI WA ELIMU NA UTAMADUNI:** Mheshimiwa Spika, naomba kumjibu Mheshimiwa Njelu Kasaka, swali lake la nyongeza, kama ifuatavyo:-

Kwa kuwa mashirika haya ni tofauti kama alivyosema Mheshimiwa Njelu Kasaka mwenyewe kwamba wafanyakazi wengine ni wale wa mashirika yaliyokuwa ya Jumuiya ya Afrika Mashariki na kama hivi sasa nilikuwa najibu swali kuhusu *Tanzania Elimu Supplies* si rahisi kupata jibu la kiujumla kwamba tutapata jawabu la kiujumla inabidi itazamwe hali halisi, mikataba iliyopo, hali ya shirika lenyewe na hili la kuwa na madai mengi kutoka kwa wafanyakazi ni kwa sababu tumekuwa katika zoezi kubwa.

Uchumi wetu ulikuwa unaulikuwa una Sekta kubwa sana ya mashirika ya Umma kwa hiyo katika mchakato wa kuyaondoa mashirika ya Umma na kuingiza uchumi wa soko huria ama sekta binafsi ndiyo inayoongoza katika kukuza uchumi ndiyo maana tumekuwa na mambo mengi.

Lakini ukiangalia tuko mwishoni mwa kazi hiyo na nina uhakika tukimaliza haya madai machache yaliyobakia hali itatengemaa zaidi. *(Makofi)*

Na. 96.

**Elimu ya Sekondari iwe Kwa Wote.**

**MHE. ABDILLAHI O. NAMKULALA** aliuliza:-

Kwa kuwa hizi ni zama za Sayansi na Teknolojia. Je, kwa nini elimu ya Sekondari sasa isifanywe kuwa ya lazima kwa wote kama ilivyo kwa elimu ya msingi?

**WAZIRI WA ELIMU NA UTAMADUNI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibuswali la Mheshimiwa Abdilahi Namkulala, Mbunge wa Mtwara Vijijini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, namhakikishia Mheshimiwa Mbunge kuwa huko ndiko tunakoelekea. Kupita MMEM 2002-2006 mwaka huu tunatoa Elimu ya Msingi kwa asilimia 95 ya watoto wote wa rika lengwa yaani wa miaka saba hadi kumi na tatu; na kupitia MMES 2004-2009 tumelenga kufika Elimu ya Sekondari kwa asilimia 50 ya wote wa rika husika yaani miaka kumi na nne hadi kumi na saba kwa elimu ya Sekondari ya kawaida. Katika awamu itakayofuata ya Mpango wa Elimu ya Sekondari lazima tulenge kufikia elimu ya sekondari kwa wote kama anavyosema Mheshimiwa Mbunge.

Lakini lazima tusonge mbele hatua kwa hatua huku tukifanya maandalizi yote yanayohitajika ikiwa ni pamoja na kuongeza idadi ya shule na walimu walioandaliwa vizuri.

Mheshimiwa Spika, lengo la mwaka huu ni kuongeza utoaji wa elimu ya sekondari hadi asilimia 35 ya rika lengwa kutoka asilimia 13 ilivyokuwa mwaka jana.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha Serikali ya Awamu ya Tatu wanafuzi katika shule zetu za sekondari wameongezeka zaidi ya maraduru kutoka 196,000 mwaka 1995 hadi zaidi ya 5,000,000 mwaka huu wa 2005 na watafikia milioni mbili mwaka 2010 watakapokuwa shuleni asilimia 50 ya rika lengwa kutokana na utekelezaji wa MMES 2004/2009 ulioanza mwaka huu.

**MHE. ABDILLAHI O. NAMKULALA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi na ninashukuru kwa majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri ila nina maswali mawili ya nyongeza.

Kwa kuwa wakazi wa Mtwara vijijini wamejiandaa na huko tunakoelekea kwa elimu ya sekondari kwa wote na kwa kuwa vijana wa Mtwara Vijijini pia wamejianda kwa kufaulu mwaka huu *to the maximum* kiasi kwamba pamoja na hela za MMES tulizogawiwa bado tuna vijana 900 hatujawapeleka shuleni kwa sababu wamefaulu wengi.

Kwa kuwa kwa Mtwara vijijini wana shule mpya ambazo hazijafunguliwa Kisiwa, Kitaya, Dihimba, Nima, Mahurunga na Libobe zimebakia nyingine kupaua, nyingine kumalizia vyoo.

Je, Mheshimiwa Waziri kwa umahiri wake, kwa ushujaa wake anaweza akapeleka angalau milioni 10 Kisiwa, milioni 10 Kitaya, milioni 10 Dihimba, milioni 10 Nima, milioni 10 Mahurunga na milioni 10 Libobe ili kumaliziamalizia kupaua na kuezeka ili vijana hawa 900 wakaenda darasani? *(Makofi)*

Swali la Pili, kwa kuwa kuwapa elimu ya sekondari kwa wote kunahitaji maandalizi hasa kutakuwa na wimbi la ongezeko la madarasa na ongezeko la waalimu.

Je, Serikali imejiandaaje katika huduma kuwahudumia hawa walimu watakao kuwa wengi maana yake mpaka naondoka kuja huku tuna shule nne tu za sekondari zinazosoma sasa hivi kule Mtwara Vijijini lakini kuna mwalimu ametoka Kilwa kuhamia shule ya Ziwani anahangaika mpaka sasa hivi uhamisho wake haujakamilika, hizo shule nne, je zikiwa shule ishirini Wizara imejiandaaje na kuweka mazingira ya walimu kutokuhangaikahangaika? *(Makofi)*

**WAZIRI WA ELIMU NA UTAMADUNI:** Mheshimiwa Spika, napenda kumjibu Mheshimiwa Abdilahi Namkulala maswali yake mawili ya nyongeza kama ifuatavyo:-

Nianze na la kwanza, kwanza kabla sijajibu napenda niwapongeze sana viongozi, walimu na watendaji wote wa Mkoa wa Mtwara kwa kuongeza ubora wa matokeo ya mtihani wa Darasa la Saba hata baada ya ongezeko kubwa la wanaokwenda sekondari wamebakia wengine 900. Kwa hiyo, natoa hongera sana kwa kazi nzuri ya walimu. *(Makofi)*

Lakini kwamba nitumie umahiri sasa hivi nito shilingi milioni 10 kwa shule zote zile alizozitaja kila moja hilo siyo rahisi kwa sababu mbili. Moja tunaendesha mambo kwa kufuata mpango na mpango ule tuliupitisha hapa Bungeni na tukapanga tunatoa shilingi kiwango tunachotoa kwa kila shule na mikoa yenyewe ikapendekeza shule zipi zipate fedha kwa mwaka huu wa kwanza. Kwa hiyo, hii ni sababu ya kwanza.

Sababu ya pili, ni kwamba tunao utaratibu kwamba kufungua kidato cha kwamba huwezi ukafungua wakati wowote kuna tarehe ya mwisho na Afisa Elimu Kiongozi alikwisha tangaza kwamba tarehe ya mwisho kwa mwaka huu kufungua kidato cha kwanza ni tarehe 1 Aprili, 2005 ambayo imekwisha pita. Kwa hiyo, hata tungekurupua hela mahali wanafunzi hawa 900 waliobakia wamekwisha chelewa kwa hiyo tukazane kuwafanyia maandalizi shule zao hizo ziwe tayari mwaka kesho.

Swali la pili, kuhusu maandalizi ya walimu, kama nilivyowahi kueleza hapa maandalizi yamekamilishwa kabisa, Chuo cha Ualimu cha Dar es Salaam kinajulikama zaidi kwa jina la Chang'ombe kinabadilishwa kuanzia mwaka huu kuwa Chuo Kikuu Kishiriki cha Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, *Mkwawa High School* inabadilishwa kuanzia mwaka na vyuo vyote hivi vitachukua walimu wa namna mbili, wapo wakaosomea *Diploma* ya Mwaka mmoja ya ualimu na wapo watakaosomea *degree* za ualimu wa miaka mitatu. Tumepanga kuchukua kwa namba kubwa ili tuandae walimu wa kutosha.

Kuhusu mazingira kule tunakowapeleka walimu katika Bajeti ya mwaka huu 2005 kwa mara ya kwanza tumetenga fedha kwa ajili ya ujenzi wa nyumba 1000 za walimu wa shule za sekondari na katika mpango wa MMES tutaendelea kujenga nyumba za

sekondari 1000 kila mwaka kwa miaka mitatu mfululizo na tunategemea tutapunguza tatizo hili la walimu wa shule za sekondari kutokuwa na nyumba. *(Makofi)*

Na. 97

**Kuanzisha Maeneo ya Uhifadhi wa Wanyamapori**

**MHE. BAKARI M. MBONDE** aliuliza:-

Kwa kuwa Sera ya Serikali ni kuwashirikisha wananchi katika uhifadhi wa wanyamapori kwa kuanzisha maeneo ya uhifadhi *(Wildlife Management Areas - WMAs):-*

(a) Je, mradi uliokubaliwa wa kuanzisha WMAs katika Kata ya Mwaseni vikiwemo Vijiji vya Mtanza, Msona, Mibuyu Saba, Mwasemi na Mloka katika Wilaya ya Rufiji utaanza kutekelezwa lini?

(b) Je, wananchi wa Vijiji hivyo vya Kata ya Mwaseni vitanufaika vipi kwa kuwepo kwa mradi huo wa kuwashirikisha wananchi hao katika uhifadhi wa wanyamapori?

**WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Bakari Mbonde, Mbunge wa Rufiji, lenye sehemu ya (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mnamo mwezi Februari 2001, Wizara yangu iliomba Serikali ya Ubelgiji kusaidia katika masuala ya uhifadhi na usimamizi wa maliasili katika Wilaya za Kilwa na Rufiji kwenye Kata zinazopatikana na Pori la Akiba la *Selous.*

Maombi hayo yalilenga katika kutekeleza dhana ya ushirikishaji wa wananchi katika usimamizi na utumiaji wa maliasili katika ukanda wa Kaskazini Mashariki mwa Pori la Akiba la *Selous,* unaojumuisha Vijiji vya Mtanza, Msona, Mibuyu Saba, Mwaseni na Mloka. Mwezi Agosti, 2001, Serikali ya Ubelgiji ilikubali ombi hilo. Mwezi Oktoba 2002, Tume ya pamoja kati ya Serikali ya Tanzania na Serikali ya Ubelgiji ilikaa na kuandaa taratibu za utekelezaji wa mradi. Utaratibu huo unajumuisha hatua zifuatazo:-

1. Utambuzi wa mradi *(Project Identification);*
2. Maandalizi ya mradi *(Project Formulation)* na
3. Utekelezaji wa Mradi *(Project Implementation).*

Kazi za utambuzi na maandalizi ya mradi zimekamilika na makubaliano ya utekelezaji yalitiwa sahihi tarehe 25 Juni, 2004. Kazi iliyobakia ni utekelezaji ambao unategemewa kuanza mwezi Julai 2005.

(b) Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Kanuni za Uhifadhi wa wanyamapori (Jumuiya ya Hifadhi ya Wanyamapori) 2002, wananchi wa Vijiji vya Kata ya Mwaseni watanufaika kwa kuwepo kwa mradi huo wa kuwashirikisha wananchi katika uhifadhi wa wanyamapori kwa:-

* Kushiriki moja kwa moja katika kusimamia uhifadhi na matumizi endelevu ya wanyamapori kwenye ardhi ya Vijiji vyao; na

* Kupata mapato ya moja kwa moja kutokana na shughuli za uhifadhi wa wanyamapori na maliasili nyingine kwenye ardhi ya Kijiji.

**MHE. BAKARI M. MBONDE:** Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu mazuri sana ya Mheshimiwa Waziri ya matumaini kwamba wananchi wa Vijiji vya Kata ya Mwaseni nao watanufaika na rasilimali wanyamapori walio katika eneo lao nina swali moja dogo la nyongeza.

Mheshimiwa Waziri atakubaliana nami kwamba tatizo la mpaka ambalo limekuwepo kati ya pori la *Selous* pamoja na Vijiji vya Kata ya Mwaseni kutokana na kuwepo kwa mradi huu utakapotekelezwa kwamba ndio utakuwa ufumbuzi wa tatizo hili la mpaka kati ya Hifadhi ya Selous na Vijiji vya Kata ya Mwaseni kwa sababu sasa hii itaondoa kule kutoaminiana na kuleta uhusiano mzuri kati ya wahifadhi wa *Selous* pamoja na wanavijiji wa Vijiji vya Kata ya Mwaseni? *(Makofi)*

**WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Spika, labda niseme kwamba tatizo hili la mpaka limekuwa linashughulikiwa na ndio maana nafikiri Mheshimiwa Mbunge anajua kwamba kidogo tumechelewa kuanza mradi huu kutoka wakati ule 2001 ilivyokubaliwa na sasa. Kwa hiyo, tatizo hili la mpaka linafuatiliwa na limetambuliwa.

**MHE. DR. RAPHAEL M. CHEGENI:** Mheshimiwa Spika, nashukuru sana. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri, kwa vile matatizo yaliyoko kule Rufiji yanafanana sana na matatizo yaliyo katika Jimbo la Busega na hasa katika Vijiji vya Mwakiloba, Kijereshi ambavyo wanapakana kati ya Pori la Serengeti na ile *Game Reserve.*

Je, Serikali haioni kwamba sasa ni muda muafaka kwa Mheshimiwa Waziri kujaribu kuliangalia tatizo hili kwa sababu kuna matatizo kati ya wafugaji na wale walinzi wa *Game Reserves,* hivyo wafugaji mara nyingi wa maeneo haya wanakamatiwa mifugo yao na kuwa *harrased* kwa mambo mbalimbali? *(Kicheko)*

**WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Spika, ningependekeza kwa Mheshimiwa Dr. Chegeni kwamba, masuala kama haya pengine mngeyazungumza pia katika ngazi za Wilaya huko halafu likaletwa kwetu ili kwa kushirikiana kwa pamoja tuweze kulitatua. *(Makofi)*

Na. 98

**Umilikaji wa Vitalu vya Uwindaji**

**MHE. MICHAEL L. LAIZER** aliuliza:-

Kwa kuwa utaratibu wa *WMA* unawawezesha wananchi walioko kwenye maeneo ya uwindaji kulinda wanyamapori watakaowaletea faida:-

Je, kwa nini Serikali isibadilishe utaratibu wa vitalu vya uwindaji *(hunting blocks)* kuwa maeneo ya *WMA?*

**WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kabla ya kujibu swali la Mheshimiwa Michael Lekule Laizer, Mbunge wa Longido, naomba kutoa maelezo yafuatayo:-

Kitalu cha uwindaji wa Kitalii ni eneo ambalo lina wanyamapori na limetengwa kwa ajili ya uwindaji wa kitalii, kulingana na Sheria ya Wanyamapori (uwindaji wa kitalii) na Kanuni za mwaka 2000 na marekebisho yake 2002/2003.

Kitalu cha uwindaji kinaweza kutengwa katika Pori la Akiba *(game reserve),* pori tengefu *(Game Controlled Area)* au katika maeneo ya wazi *(open areas).*

Mheshimiwa Spika, maeneo ya Jumuiya ya Hifadhi ya Wanyamapori *(Wildlife Management Areas - WMAs)* yanaanzishwa kulingana na Sheria ya Wanyamapori maeneo ya Jumuiya ya Hifadhi ya Wanyamapori, Kanuni za mwaka 2002. Haya ni maeneo ambayo wananchi wataruhusiwa kushiriki katika shughuli za uhifadhi wa rasilimali ya wanyamapori katika ardhi ya Kijiji na kuweza kupata faida kutokana na uhifadhi huo. Hivyo dhana ya *WMA* inaweka mipango halali ya matumizi endelevu ya wanyamapori katika ardhi ya Kijiji.

Kwa sasa, utaratibu huu unaendelea katika maeneo 16 ya majaribio, ambayo yapo katika hatua mbalimbali za utekelezaji ili yaweze kutengwa kuwa *WMA.* Baadhi ya maeneo yaliyoorodheshwa kuwa maeneo ya majaribio ya *WMA* pia ni vitalu vya uwindaji wa kitalii.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo naomba sasa kujibu swali la Mheshimiwa Michael Lekule Laizer, Mbunge wa Longido kama ifuatavyo:

Mheshimiwa Spika, Serikali haina nia ya kubadili vitalu vya uwindaji wa kitalii kuwa *WMA.* Kulingana na Kanuni za *WMAs 2002,* wananchi wanapoanzisha *WMA* huainisha matumizi ya rasilimali katika mpango wa usimamizi *(General Management Plan)* wa eneo hilo. Hivyo *WMA* au sehemu yake inaweza kuwa kitalu cha kuwindia kama wananchi watapanga aina hiyo ya matumizi ya wanyamapori kwenye eneo hilo.

**MHE. LEKULE M. LAIZER:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ili niulize swali la nyongeza. Kwa kuwa katika maeneo hayo 16 aliyosema Waziri kwamba wameruhusiwa kuendesha biashara *WMA* bado kuna wawindaji waliopo pale. Je, ni lini Serikali itaweka utaratibu ili hao wawindaji wenye *blocks* hizo waweze kuondoka ili wananchi waweze kufanya biashara?

Mheshimiwa Spika, pili, kwa kuwa bado sheria ina utata. Je, ni lini Serikali italeta sheria hapa Bungeni ili uwekwe utaratibu wananchi hawa waweze kufanya shughuli katika maeneo hayo?

**WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Spika, kuanzishwa kwa *WMA* kuna taratibu ambazo lazima zifuatwe na ndio maana nikasema hapa kwamba *WMA* zinaanzishwa katika ardhi ya Kijiji. Kwa hiyo, kwa maeneo yale ambayo sio ardhi ya Kijiji kwa mfano, *Game Controlled Area* na *Game Reserve* ambapo uwindaji unafanyika, utaratibu lazima ufanywe kubadilisha matumizi ya ardhi ile kutoka ardhi ya Serikali Kuu kwenda kwenye ardhi ya Kijiji. Kwa hiyo, hiyo *process* lazima ifanyike.

Lakini pamoja na hayo maeneo hayo 16 tuliyoyatambua, *process* ya kuelimisha wananchi inafanyika na imefanyika na baada ya hapo lazima Kijiji kizima kikae na kufanya maamuzi na *minutes* za kikao hicho lazima ziende kwa Mkurugenzi wa Idara ya Wanyamapori. Baada ya hapo ndipo matumizi ya eneo hilo yanatambulika. Kwa hiyo, katika maeneo haya, *process* hizi zisipokamilika haitawezekana kwa kweli kubadilisha matumizi ya ardhi husika.

Mheshimiwa Spika, kuhusu suala la Sheria, nafikiri ni Sheria ya Mwaka 1974 ndiyo ambayo Mheshimiwa Laizer anaielezea. Naomba niseme kwamba, tupo katika hatua ya mwisho ya kumalizia sheria hii na baada ya hapo italetwa hapa Bungeni. *(Makofi)*

**MHE. SEMINDU K. PAWA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi hii ili niulize swali moja dogo la nyongeza. Kwa kuwa taratibu zote hizi alizokuwa anaeleza ni sahihi na zinalinda wanyama wetu na kwa kuwa taratibu zimeshafuatwa kwenye Jimbo la Morogoro Kusini na Kusini Mashariki kwa kuandika muhtasari wa Vijiji kumi na tatu kwa ajili ya Pori la Matambwe na tulipeleka Ofisini kwa Afisa Wanyamapori Taifa, lakini mpaka leo bado hatujapata majibu na tumeunda Tume ya watu watano kwenda kumwona Mheshimiwa Waziri. Je, yupo tayari? *(Kicheko)*

**WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Spika, tunajua kwamba tumepata maombi ya *WMA* kama manne, nafikiri mojawapo litakuwa la Mheshimiwa, lakini kulikuwa na matatizo na ndio maana yalichelewa.

Tatizo mojawapo ni kwamba kuna *WMA* zililetwa bila ya kuleta *minutes* na zingine zililetwa bila kuleta *General Management Plan* (mipango ya matumizi ya maeneo hayo). Kwa hiyo, kama katika eneo la Mheshimiwa Mbunge haya yote yamefanyika, basi utaratibu huu haupaswi kuchelewa.

Na. 99

**Fadhila kwa Wastaafu**

**MHE. IBRAHIMU W. MARWA** aliuliza:-

Kwa kuwa hivi karibuni Serikali iliamua kutoa upendeleo wa kuboresha maisha ya wafanyakazi wake kwa kuwauzia nyumba za Serikali wanazoishi kwa bei nafuu *(book value)* na kwa kuwa, wapo watumishi wengi waliotumikia nchi hii kwa uadilifu mkubwa na kujenga nchi kwa nguvu na maarifa makubwa wakati wa ujana wao hadi walipostaafu kwa mujibu wa sheria na kwa kuwa ni kweli kwamba wastaafu hao wanaishi maisha ya dhiki na duni kutokana na kiwango kidogo cha pensheni wanacholipwa na baadhi kutolipwa kutokana na sheria ya mkupuo ambayo imewaathiri sana:-

(a) Je, Serikali ya Awamu ya Tatu ambayo imeonyesha kuwajali watumishi wake waliopo kwenye ajira ina mpango gani wa kulipa fadhila kwa wazee wastaafu angalau kwa kuongeza kiwango cha pensheni kutokana na pato la Taifa kuongezeka?

(b) Je, hadi kufikia Juni, 2002 ni watumishi wangapi waliostaafu na ni wangapi waliopoteza maisha yao katika kipindi cha miaka 10 iliyopita?

(c) Je, Serikali imefanya utafiti wowote kujua maisha ya watumishi waliostaafu ili kuiwezesha kuwa na mpango wa Kitaifa wa kutoa unafuu kwenye gharama za huduma mbalimbali kama vile Maji (Mfano, Namibia wanafanya hivyo), umeme, matibabu na baadhi ya kodi wanazostahili kulipa?

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. DR. FESTUS B. LIMBU)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kabla ya kujibu swali la Mheshimiwa Ibrahim Wankanga Marwa, Mbunge wa Musoma Mjini, naomba kutoa maelezo ya utangulizi kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni sera ya Serikali ya Awamu ya Tatu kuhakikisha inawajali wananchi wake wote, ikiwa ni pamoja na wastaafu na wasio na ajira, katika jitihada za kuboresha maisha ya wananchi wake.

Jitihada ambazo zimekuwa zikichukuliwa na Serikali katika kuboresha maisha ya wananchi wake zimekuwa zikielekezwa aidha kwa makundi ya wananchi, kama vile watumishi waliopo katika ajira Serikalini kupewa upendeleo wa kuuziwa nyumba wanazoishi kwa bei nafuu, kupandisha mishahara ya watumishi Serikalini, ikiwa ni pamoja na viwango vya pensheni kwa wastaafu au kwa namna nyingine yoyote ile ambayo azma yake ni kufanikisha lengo la Serikali la kuboresha maisha ya wananchi.

Mheshimiwa Spika, kutokana na malalamiko ya wastaafu kuwa kiwango cha pensheni zao kwa mwezi ni kidogo, Serikali ilipendekeza na Bunge lako Tukufu likapitisha Sheria ya kuwaruhusu wastaafu wanaopenda kuchukua pensheni zao zote kwa mara moja yaani mkupuo, badala ya kuchukua kidogo kidogo kila mwezi, lakini katika kufanya hivyo, ingawa nia ya Serikali ilikuwa nzuri, imeonekana utaratibu huu unawaathiri wastaafu baadaye. Hapo Bunge lako Tukufu likapitisha tena sheria ya kuwarejesha katika daftari la pensheni wastaafu wote waliokuwa wamechukua mkupuo.

Mheshimiwa Spika, baada ya kutoa maelezo hayo ya jumla, sasa napenda kujibu swali la Mheshimiwa Ibrahim Wankanga Marwa, Mbunge wa Musoma Mjini, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, Serikali ya Awamu ya Tatu imekuwa ikiongeza kiwango cha pensheni kwa wastaafu kila wakati hali ya fedha inaporuhusu. Ndiyo maana kiwango cha pensheni kimeongezeka kutoka Tshs.400/= kwa mwezi miaka ya 1980 na kufikia Tshs. 20,077/= kwa mwezi hivi sasa.

Mheshimiwa Spika, kiwango hiki cha pensheni cha Tshs. 20,077/= kwa mwezi bado ni kidogo kulingana na hali halisi ya maisha. Serikali inaelewa tatizo hili na jitihada zitaendelea kufanywa ili kuhakikisha kiwango cha pensheni kwa wastaafu kinaongezwa kadri hali ya uchumi itakavyoruhusu.

(b) Mheshimiwa Spika, hadi Machi, 2005 watumishi waliostaafu walikuwa 42,575. Watumishi waliopoteza maisha yao katika kipindi cha miaka 12 iliyopita ni 23,642 ikiwa ni wastani wa karibu wastaafu 1,970 kwa mwaka.

(c) Mheshimiwa Spika, Serikali haijafanya utafiti kuhusu maisha ya watumishi waliostaafu ili kuiwezesha kuwa na mpango wa Kitaifa wa kutoa unafuu kwenye gharama za huduma mbalimbali kwa watumishi hao. Mipango inayofanywa sasa na Serikali ni kukamilisha maandalizi ya Sera ya Kufuta Umaskini kwa watu wote.

Sera hii inazingatia makundi ya aina zote katika jamii, ikiwa ni pamoja na wastaafu. Aidha, Serikali kwa kupitia Taasisi/Asasi mbalimbali huandaa mipango mbalimbali kama vile sensa ya kuhesabu watu ambayo imekwishafanyika ili hatimaye iweze kujua na kubaini mahitaji ya makundi mbalimbali katika jamii yetu.

**MHE. IBRAHIMU W. MARWA:** Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri naomba niulize maswali mawili ya nyongeza. Kwa kuwa katika siku za karibuni waliokuwa wastaafu wa Jumuiya ya Afrika Mashariki walifanya maandamano kwenda Wizara ya Fedha kudai haki zao na kwa kuwa siku hiyo walivyokwenda pale zilitumika nguvu sana za kuwadhibiti ikiwa ni nguvu ambazo zilikuwa zinaashiria ubabe wa namna fulani. Je, hii ndio shukrani tunayowalipa wastaafu hawa? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, swali la pili, je Serikali ina mpango gani wa kuweka vivutio kwa hawa wastaafu ili wasiweze kung'anga'nia kwenye kazi waweze kustaafu na kuacha nafasi hizi ili wanaomaliza vyuoni na kwenye mashule waweze kupata ajira? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. DR. FESTUS B. LIMBU):** Mheshimiwa Spika, kwanza napenda nimpongeze sana Mheshimiwa Marwa kwa juhudi kubwa anayofanya katika kufuatilia masuala mbalimbali katika Jimbo lake na kuwaendeleza wananchi pamoja na wastaafu.

Mheshimiwa Spika, suala la wafanyakazi wa iliyokuwa Jumuiya ya Afrika Mashariki linashughulikiwa kwa kina na Serikali inachukua hatua na ufumbuzi wa tatizo hili upo njiani.

Hivyo, nawaomba wahusika wawe na subira kwani Serikali inalifanyia kazi tatizo hili. Nguvu iliyotumika walipoandamana haikuwa ya kuwadhalilisha wala kutaka kuwaonyesha ubabe wa aina yoyote. Serikali kwa vyovyote ipo pale kusaidia na kuwatumikia wananchi sio kuwaonyesha ubabe.

Mheshimiwa Spika, pili, vivutio ambavyo vinaweza vikawekwa ili watu wastaafu mapema, sheria imeweka wazi umri wa kustaafu, kwa hiyo muda ukifika wa kustaafu inabidi mtu ama mfanyakazi astaafu.

Lakini pengine ningependa kutumia Bunge hili Tukufu kuwaomba watu wanaostaafu wafanye maandalizi ya kustaafu ili muda wa kustaafu ukifika wasiwe na hali mbaya ya maisha.

**MHE. DR. WILBROD P. SLAA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali dogo la nyongeza. Kwa kuwa njia ya kuboresha maisha ya wastaafu sio mishahara tu na kwa kuwa nchi nyingi duniani zinatumia njia mbalimbali ikiwemo matibabu pamoja na usafiri.

Je, Serikali ina mpango gani mahsusi wa kuwaandalia utaratibu mahsusi kabisa kwamba wapate manufaa katika huduma mbalimbali zinazotolewa katika nchi yetu ili hiyo iwe ni nyongeza kwa mishahara midogo waliyonayo? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. DR. FESTUS B. LIMBU):** Mheshimiwa Spika, Serikali imetoa matibabu bure kwa wazee ambao umri wao ni zaidi ya umri fulani. Kwa hiyo, hiyo ni huduma mojawapo pia ambayo Serikali imetoa kama kivutio au kama msaada kwa watu wenye umri mkubwa ikiwa ni pamoja na wastaafu.

Lakini katika jibu langu la msingi nimesema kwamba Serikali inajua matatizo ya wastaafu kwamba posho ama pensheni ambayo inatolewa ya shs. 20,077/= kwa mwezi haitoshi kulingana na hali halisi ya maisha na nimwombe tu Mheshimiwa Mbunge na Bunge lako Tukufu na wastaafu kwa ujumla kwamba Serikali itazidi kuboresha maslahi haya kadri hali ya uchumi wetu itakavyokuwa inaimarika.

Na. 100

**Mzunguko wa Fedha**

**MHE. THOMAS NGAWAIYA (k.n.y. MHE. MUTTAMWEGA B. MGAYWA)** aliuliza:-

Kwa kuwa hivi sasa kumekuwepo na mzunguko mdogo sana wa fedha nchini:-

Je, Serikali inakubali kwamba kuondolewa kwa fedha katika mzunguko kunatokana na wafanyabiashara wengi kuhamisha fedha za kigeni na pia fedha za ndani kwa kununua madini na kuyapeleka nje ya nchi kuyauza?

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. DR. FESTUS B. LIMBU)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Muttamwega Mgaywa, Mbunge wa Mwibara, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa, napenda kumfahamisha Mheshimiwa Mbunge, kuwa si kweli kwamba kuondolewa kwa fedha katika mzunguko kunatokana na wafanyabiashara wengi kuhamisha fedha za kigeni na pia fedha za ndani kwa kununua madini na kuyapeleka nje ya nchi kuyauza.

Mheshimiwa Spika, wafanyabiashara na wananchi wengine kwa ujumla hununua fedha za kigeni kutoka kwenye mabenki na maduka ya fedha za kigeni kwa ajili ya kuagiza bidhaa au kulipia huduma nyingine kama elimu, matibabu, usafiri na kadhalika kulingana na sheria zilizopo.

Kwa kuwa fedha ya ndani inayotumika kununulia fedha hizo za kigeni inabakia humu nchini, hakuna uwezekano wa fedha ya ndani kupungua katika mzunguko. Pale ambapo Benki Kuu inanunua fedha za kigeni kwa ajili ya kulipa madeni ya nje ya Serikali, kitendo hicho huongeza fedha ya ndani kwenye mzunguko badala ya kupunguza.

Mheshimiwa Spika, vile vile kununua madini na kuyapeleka nje ya nchi kuyauza hakuwezi kupunguza fedha katika mzunguko kwa sababu aliyelipwa fedha hizo yuko ndani ya nchi hivyo fedha hiyo inabakia kwenye mzunguko.

Mheshimiwa Spika, njia ambazo zingeweza kupunguza fedha kwenye mzunguko au kufanya fedha iliyoko kwenye mzunguko ionekane kidogo ni kama zifuatazo:-

(i) Kama wafanyabiashara anaowazungumzia Mheshimiwa Mbunge wangesafirisha fedha ya Tanzania nje ya nchi, fedha hizo zingekuwa zimeondolewa kwenye mzunguko.

(ii) Vile vile kama wafanyabiashara hao ama wananchi kwa ujumla, wakihifadhi ama kuhodhi fedha taslim majumbani mwao, hupunguza fedha kwenye mzunguko kwa kipindi ambacho fedha hiyo inabaki imehifadhiwa. *(Makofi)*

(iii) Endapo pato la Taifa na hivyo pato la wananchi wake likiongezeka fedha iliyoko kwenye mzunguko huonekana kidogo kuliko kiwango kinachohitajiwa kwa vile wananchi hufanya shughuli zao na hivyo kuonekana kuwa fedha iliyoko kwenye mzunguko imepungua.

Mheshimiwa Spika, kutokana na kuendelea kukua kwa uchumi wa Tanzania katika miaka ya karibuni, kiasi cha fedha katika mzunguko kiliongezeka kutoka Sh. 219.2bn/= mwezi Juni, 1996 na kuendelea kuongezeka hadi Sh. 632.1bn/= kufikia mwezi wa Februari, 2005 sawa na ongezeko la zaidi ya mara tatu. Hii imekwenda sambamba na nia ya Serikali katika jitihada ya kushusha mfumuko wa bei kwa madhumuni ya kuboresha maisha ya Watanzania. Mfumuko wa bei uliendelea kushuka kutoka asilimia 21.0 mwaka 1996 hadi kufikia asilimia 4.1 mwezi Februari, 2005.

Takwimu hizi, zinaonyesha kwamba kiasi cha fedha kwenye mazunguko kimeongezeka kwa karibu mara tatu katika kipindi cha miaka tisa bila kuchochea kuongezeka kwa mfumuko wa bei. Tafsiri yake kiuchumi ni kwamba ongezeko hili la ujazo wa fedha kwenye mzunguko limetokana na ongezeko la uzalishaji katika uchumi. Kwa hiyo, hakuna upungufu wa fedha kwenye mzunguko kama anavyoeleza Mheshimiwa Mbunge, bali katika kipindi hicho, Watanzania wameendelea kunufaika kutokana na kukua kwa pato la Taifa na kushuka kwa mfumuko wa bei.

Mheshimiwa Spika, katika kusimamia mfumo wa malipo na utekelezaji wa sera ya fedha hapa nchini, Benki Kuu imekuwa inahakikisha kwamba kuna kiasi cha fedha cha kutosha katika mzunguko kulingana na mahitaji ya wananchi katika kufanya malipo. Mikakati ambayo Wizara yangu imejiwekea katika kuhakikisha kwamba fedha ya kuwahamasisha wananchi kuanzisha benki ndogo ndogo za Vijijini na kuzitumia kwa ajili ya kujiwekea akiba zao badala ya kuweka fedha majumbani.

Wananchi wengi wamepoteza fedha zao kwa kuunguliwa na nyumba ama kuliwa na wadudu waharibifu kama mchwa na hata panya, jambo ambalo lingeliweza kuepukwa kama wangeweka akiba zao kwenye mabenki. Hii itasaidia sio tu kuondoa tatizo la upungufu wa fedha kwenye mzunguko, linalotokana na wananchi kuhifadhi fedha nyingi majumbani. Pali pia kuondoa au kupunguza uchapishaji wa fedha mpya ili kurudishia zile ambazo zimepotea ama kuharibika.

**MHE. THOMAS NGAWAIYA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Kwa kuwa Mheshimiwa Waziri amekiri mwenyewe kwamba fedha zipo kwa wingi katika mzunguko. Je, ni kwa nini wananchi wa Tanzania wa kawaida hawana hizo fedha mifukoni kwao kwa sasa kulingana na miaka iliyopita? *(Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, swali la pili, kuna watu wengi sana wanaidai Serikali na ilisemekana kwamba ilikuwa inasita kuwalipa kwa kuogopa huo mzunguko wa fedha. Je, Serikali ipo tayari sasa kuagiza watu hawa wanaoidai Serikali walipwe madeni yao?

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. DR. FESTUS B. LIMBU):** Mheshimiwa Spika, wananchi hawana fedha mifukoni mwao kwa sababu mbalimbali aidha, hawajishughulishi ipasavyo ama zingine. Itakumbukwa kulikuwa na wakati watu walikuwa wanapata fedha bila kufanya kazi, yaani kwa kufanya ujanja ujanja.

Sasa hali hii ilipozuiliwa na kumtaka kila mwananchi afanye kazi au apate fedha kwa kufanya kazi ndio maana wananchi wengi hawana fedha mifukoni. Kuna wengine walikuwa wanatembea na fedha kwenye soksi na wale waliokuwa na ajira walikuwa wanaonekana kama hawana akili sawasawa kwa sababu watu ambao walikuwa wanapata fedha kwa ujanja ujanja ndio walikuwa wanaonekana wa maana zaidi kwa sababu walikuwa na fedha. Hali hiyo sasa haipo, Watanzania watapata fedha kwa kufanya kazi.

Mheshimiwa Spika, Serikali ina aina mbili ya madeni; madeni ya ndani na ya nje. Madeni ya nje yanalipwa kulingana na taratibu na Bajeti na pia madeni ya ndani. Kwenye matangazo ya kila mwezi ambayo yanatolewa na Wizara ya Fedha kwa ajili ya malipo mbalimbali kwenye Wizara na Idara za Serikali ni pamoja na madeni ya ndani yanayolipwa.

Kwa hiyo, Mheshimiwa Ngawaiya kama ana deni ambalo anafikiri limechelewa kulipwa au halijalipwa basi tuwasiliane ili tuweze kulipa, lakini Serikali inalipa madeni yote kulingana na taratibu na ratiba. *(Makofi)*

Na. 101

**Pembejeo za Kilimo kwa Wakulima wa Tumbaku Msimu wa 2004/2005**

**MHE. DR. JAMES A. MSEKELA** aliuliza:-

Kwa kuwa wakulima wa tumbaku walipokea na kugawana pembejeo katika msimu huu wa 2004/2005 bila kufahamishwa bei ya pembejeo hizo wala bei mpya ya tumbaku:-

(a) Je, Serikali inasema nini kuhusu uzembe wa taasisi zote zilizohusika na zoezi hilo?

(b) Je, taasisi hizo ni zipi na Serikali inachukua hatua gani dhidi ya hali hiyo?

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO NA CHAKULA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kabla ya kujibu swali la Mheshimiwa Dr. James Alex Msekela, Mbunge wa Tabora Kaskazini, lenye sehemu (a) na (b) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kilimo cha tumbaku nchini kinafanywa kwa mfumo wa Mkataba kati ya mzalishaji (au mkulima) na mnunuzi wa tumbaku *(contract farming).* Chini ya utaratibu huo, mnunuzi huagiza pembejeo za kilimo na kuziuza au kuzikopesha kwa mkulima kwa makubaliano kwamba mkulima atamuuzia mnunuzi tumbaku atakayozalisha na iwapo mkulima atakuwa amechukua pembejeo kwa mkopo, deni lake litakatwa kutokana na mauzo yake ya tumbaku.

Mheshimiwa Spika, utaratibu huu umekuwa na manufaa makubwa kwa wakulima wa tumbaku kwa kuwa unawahakikishia upatikanaji wa pembejeo za kilimo na kwa mkopo. Kilimo cha tumbaku kinahitaji mbolea nyingi, madawa mengi na vifaa vya kilimo na ujenzi wa mabanda ya kukaushia tumbaku.

Mheshimiwa Spika, katika msimu wa 2004/2005, Halmashauri ya Tumbaku ambayo inajumuisha wawakilishi wa wakulima kupitia kwenye Vyama vyao vya Ushirika, wanunuzi na wasindikaji wa tumbaku na Bodi ya Tumbaku ilikutana mara tatu kujadili bei za pembejeo bila kufikia makubaliano. Halmashauri hiyo iliamua na kuagiza kwamba pembejeo za kilimo zisambazwe wakati majadiliano yakiendelea ili zisicheleweshwe kumfikia mkulima. Baada ya makubaliano kufikiwa, wakulima walijulishwa bei za pembejeo na za madaraja mbalimbali ya tumbaku.

Mheshimiwa Spika, uamuzi wa kusambaza pembejeo mapema bila kusubiri makubaliano ya bei ulikuwa wa busara, vinginevyo wakulima wangechelewa kupata pembejeo zao, jambo ambalo lingeweza kuathiri kilimo cha tumbaku kwa msimu wa 2004/205. Kwa hali hiyo, Serikali haioni kwamba kulikuwa na uzembe na badala yake inaipongeza Halmashauri ya Tumbaku kwa uamuzi wake wa busara na uliofanyika kwa wakati.

Mheshimiwa Spika, chombo kilichoamua kwamba pembejeo zisambazwe wakati majadiliano ya bei yakiendelea ni Halmashauri ya Tumbaku. Serikali haikuichukulia na wala haikusudii kuichukulia hatua zozote.

**MHE. DR. JAMES A. MSEKELA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru na naomba nimwulize Mheshimiwa Waziri maswali ya nyongeza. Kwa kuwa ametamka bayana katika majibu yake kwamba kilimo cha tumbaku kimsingi ni kilimo cha mikataba kwa maana ya *contract farming* ambapo mkulima mdogo anakuwa hana sauti na kwa kuwa vile vile amethibitisha kwamba kulikuwa na mikutano mitatu ambayo haikuzaa matunda kiasi kwamba ikaamuliwa basi pembejeo zigawanywe. *(Makofi)*

Je, kama itatokea wakulima baada ya kuwa wametumia pembejeo hawataridhika na bei ambazo zitatolewa baada ya kuwa wameshapokea pembejeo na kuzitumia, nani atakayehusikana hasara hiyo? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, swali la pili, kwa kuwa sasa misimu hii ya kilimo cha tumbaku inafahamika kwa uzoefu uliokuwepo, kwa nini Serikali kwa kuwa inafahamu sasa taratibu fika zinazohusika katika kilimo kizima cha tumbaku, kwa nini Serikali

isipange ratiba ya kuona kwamba hili kufikia tarehe fulani litakuwa limetimizwa na kuifanya Bodi ya Tumbaku ikasimamia ratiba hiyo kikamilifu?

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO NA CHAKULA:** Mheshimiwa Spika, mikataba inayomhusu mkulima mdogo hufanyika na Halmashauri ya Tumbaku. Halmashauri ya Tumbaku inamwakilisha mkulima mdogo na mkubwa kwa ifuatavyo:- Wawakilishi wa wakulima hawa wadogo wadogo kupitia Vyama vya Ushirika. Halafu wanunuzi wa tumbaku wenyewe, wasindikaji wa tumbaku na bodi ya tumbaku yenyewe kwa ujumla na humo ndani ya Bodi tuna Mheshimiwa Mbunge mwenzetu yuko pale anatuwakilisha kuhakikisha kuwa maslahi ya wadogo yapo.

Kwa hiyo, ninaamini kuwa pamoja na mikutano mitatu iliyokuwepo ile inaonyesha umakini kwa shughuli hizo ilibidi wajadiliane mpaka kupata muafaka na muafaka ulipopatikana mambo yalitekelezeka. Sasa kama mtu haridhiki na bei baada ya hapo haitatokea kwa sababu majadiliano hayo yanafanyika kusudi watu wote waridhie kupata *consequence.* Kwa hiyo, kwa mwaka huu *consequence* ilikuwepo na hiyo hali anayoeleza Mheshimiwa Mbunge haitatokea kwa sababu ya demokrasia iliyojengeka ndani ya muundo wa Halmashauri ya Tumbaku.

Halafu kuhusu misingi Serikali ipange ratiba. Ratiba zipo kama kawaida inaeleweka kwa mfano, sasa hivi utaratibu wa kupeleka mbolea unaanza kufanyika sasa na tunategemea mbolea itakuwepo na vilevile mbolea ya ruzuku ya Serikali iko pale pale isipokuwa yenyewe kwa bei taslimu.

**SPIKA:** Uliza swali lako Mheshimiwa Mossy Mussa, swali la mwisho kwa leo. Amekwenda Mtera, basi muda wa maswali umekwisha. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge tunaendelea na matangazo ya vikao vya leo vya Kamati. Kamati mbili zifuatazo zimepangiwa vikao na Wenyeviti wao. Kamati ya kwanza, ni ya Miundombinu, Mheshimiwa Prof. Henry Mgombelo, anawaomba Wajumbe wa Kamati hiyo wakutane leo tarehe 21 Aprili, 2005 saa 7.00 mchana katika ukumbi wa 231 kwa ajili ya kukutana na Ujumbe wa Shirika la Usafiri Dar es Salaam (UDA).

Kamati ya pili, ni ya Fedha na Uchumi Mwenyekiti wake anawatangazia Wajumbe wa Kamati hiyo kuwa leo tarehe 21 Aprili, 2005 kutafanyika kikao saa 4.30 asubuhi yaani mara baada ya kipindi hiki cha maswali katika chumba namba 227. Mwisho wa matangazo ya vikao vya Kamati.

Tangazo la mwisho ni kwamba Waheshimiwa Wabunge mmegawiwa ratiba ya vikao vinavyoendelea vya Mkutano huu, lakini ukurasa wa pili una makosa. Kwa hiyo, ukurasa ambao ni sahihi umegawiwa baadaye kuonyesha kwamba tarehe 30 Aprili, 2005 ni siku ya Jumamosi na siyo Ijumaa. Naomba mzingatie masahihisho hayo. Tunaendelea na *Order Paper* Katibu endelea.

## HOJA ZA SERIKALI

### Taarifa ya Mwaka ya Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora Kuanzia Julai, 2001 Mpaka Juni, 2002

**WAZIRI WA SHERIA NA MAMBO YA KATIBA:** Mheshimiwa Spika, awali ya yote naomba nitoe pole na rambirambi zangu kwa ndugu, jamaa na familia ya Mheshimiwa Marehemu Ahmed Hassan Diria na pia kwa wapiga kura wote wa Jimbo la Rahaleo Zanzibar kutokana na kifo cha Ndugu na Mbunge wao mpendwa kilichotokea huko Ujerumani na Marehemu kuzikwa Dar es Salaam.

Wakati anafariki Mheshimiwa Marehemu Ahmed Hassan Diria alikuwa ni Waziri wa Nchi katika Ofisi ya Rais, huko Zanzibar akishughulikia masuala ya Katiba na Utawala Bora. Nikiwa ni Waziri wa Sheria na Mambo ya Katiba katika Serikali ya Jamhuri ya Muungano ndugu Marehemu Ahmed Diria aliendeleza ushirikiano wa karibu kati ya Wizara hizi mbili tuliokuwa nao tangu Mheshimiwa Dr. Ali Mohammed Shein na baadaye Adam Mwakajuki walipokuwa wakishikilia wadhifa huo. Hivyo, kifo cha Marehemu Ahmed Diria siyo tu ni pigo kwangu mimi binafsi bali pia kwa Wizara ninayoiongoza ya Sheria na Mambo ya Katiba.

Aidha, natoa pole kwa Ndugu na jamaa wa Marehemu Paul Bomani aliyefariki baada ya kulitumikia Taifa hili katika nyadhifa mbalimbali tangu enzi za kupigania uhuru na hata baada ya uhuru. Naomba Mwenyezi Mungu aziweke roho za Marehemu hao wote mahali pema peponi. *Amin.*

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa kifungu 33(1)(a) -(c) cha Sheria ya Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora na Namba 7 ya mwaka 2001, ninaomba kuwasilisha mbele ya Bunge lako Tukufu taarifa ya mwaka ya Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora kwa kipindi cha kuanzia tarehe 1 Julai, 2001 hadi 30 Juni, 2002.

Mheshimiwa Spika, Waheshimiwa Wabunge watakumbuka kwamba mnamo mwaka 2000 walipitisha Sheria ya Mabadiliko ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Namba 3 ya mwaka 2000. Katika mabadiliko hayo Sura ya Sita, Sehemu ya Kwanza Ibara 129(1) ilifanyiwa marekebisho kwa kuifuta iliyokuwa Tume ya Kudumu ya Uchunguzi na badala yake kuanzisha Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora.

Mnamo mwaka 2001, Bunge lilipitisha Sheria ya Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora Namba 7 ya mwaka 2001 ambayo ilifafanua kwa undani zaidi mamlaka ya Tume kama yalivyoelezwa katika Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania 1977 na pia kuelezea namna ambavyo Tume itafanya shughuli zake. Sheria hiyo ilianza kutumika mwezi Mei, 2001 na Tume ilianza kama Idara inayojitegemea tarehe 1 Julai, 2001 baada ya Tangazo la Serikali Namba 311/2001. Kazi na majukumu ya Tume kama yalivyoainishwa kwenye Ibara ya 130 ya Katiba na kufafanuliwa na fungu la 6 la Sheria namba 7, 2001 ni kama ifuatavyo:-

(a) Kupokea malalamiko na kufanya uchunguzi juu ya mambo yanayohusu uvunjaji wa Haki za Binadamu na ukiukwaji wa misingi ya Utawala wa Bora.

(b) Kufanya utafiti na kueneza nchini elimu kwa umma kuhusu Haki za Binadamu na Utawala Bora.

(c) Kufungua mashauri Mahakamani ili kuzuia vitendo vya uvunjaji wa Haki za Binadamu au kurekebisha haki inayotokana na uvunjaji huo wa Haki za Binadamu au ukiukwaji wa misingi ya Utawala Bora.

(d) Kutoa ushauri kwa Serikali na vyombo vingine vya umma na vya sekta binafsi kuhusu Haki za Binadamu na Utawala Bora.

(e) Kuchukua hatua zipasazo kwa ajili ya kukuza na kuendeleza usuluhishi na suluhu miongoni mwa watu na Taasisi mbalimbali wanaofika au kuwafikisha mbele ya Tume.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa mamlaka aliyopewa chini ya Ibara 129(3) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kifungu namba 7(2) cha sheria Namba 7 ya mwaka 2001 aliwateua Makamishna wa Tume tarehe 14 Machi, 2002 na kuwaapisha siku iliyofuata tarehe 15 Machi, 2002. Kwa maana hiyo Makamishna wa Tume walifanya kazi katika mwaka wa fedha 2001/2002 kwa kipindi cha miezi mitatu tu.

Mheshimiwa Spika, kwa ujumla Tume imetekeleza majukumu yake vizuri. Kwanza, kwa kuyashughulikia malalamiko yaliyorithiwa kutoka Tume ya Kudumu ya Uchunguzi baada ya kuanzishwa Tume hii. Ingawa Makamishna wa Tume walianza kazi rasmi baada ya kuapishwa tarehe 15 Machi, 2002 kulikuwa na Sekretariet ambayo ilipewa jukumu na Serikali la kuendeleza kazi ya Tume hiyo kwa kufanya mawasiliano ya kupokea na kukiri upokeaji wa malalamiko ya wananchi.

Kwa hiyo, Makamishna walipoteuliwa walikuta jumla ya malalamiko 2,237 ambayo yalikuwa hayajakamilishwa na iliyokuwa Tume ya Kudumu ya Uchunguzi na malalamiko 1,074 ambayo yalipokelewa na Sekretariet kuanzia kipindi cha Julai, 2001 hadi tarehe 30 Juni, 2002.

Mheshimiwa Spika, malalamiko ambayo yaliachwa na Tume ya Kudumu ya Uchunguzi na yaliyopokelewa na Sekretariet naweza kuyagawanya katika makundi makubwa matano ambayo ni:-

(a) Malalamiko juu ya ajira na nidhamu katika Serikali Kuu ambayo yalikuwa ni asilimia 27.2 ya malalamiko yote.

(b) Malalamiko juu ya ajira na nidhamu katika Serikali za Mitaa, Halmashauri za Wilaya, Jiji, Manispaa na Mashirika ya Umma ambayo yalikuwa ni asilimia 10.3 ya malalamiko yote.

(c) Madai ya mafao ya pensheni kutoka *GEPF, LAPF, NSSF,* Bima, *PPF, WADU* ambayo ni asilimia 20.1 ya malalamiko yote.

(d) Malalamiko kuhusu Sheria, Mahakama, Mahakama ya Kazi juu ya mirathi, leseni mbalimbali, jinsia, mazingira, ukwepaji wa kodi mbalimbali. Malalamiko ya aina hii yalikuwa ni asilimia 16.3 ya malalamiko yote.

(e) Malalamiko yanayohusu Vyombo vya Dola kwa maana ya Polisi, Magereza, ukiukwaji wa Haki za Binadamu, fidia, ardhi, rushwa na mengine ya jumla. Haya yalikuwa ni asilimia 22.9 ya malalamiko yote yaliyokuwa mbele ya Tume.

(f) Malalamiko yote ambayo Tume inayo mamlaka ya kuchunguza yaliyoko Zanzibar, malalamiko ya aina hii yalikuwa ni asilimia 3.2 ya malalamiko yote.

Mchanganuo wa malalamiko wa kijinsia, Mikoa na kadhalika umefanywa katika majedwali 5.2 ukurasa wa 13 - 5.3 ukurasa wa 14 - 5.4 unaohusu Mikoa iliyoko Zanzibar ukurasa wa 15.

Aidha, mchanganuo wa aina ya malalamiko yaliyopokelewa kutoka Tume ya Kudumu ya Uchunguzi na walalamikiwa yameonyeshwa katika jedwali 6.1 ukurasa 16 hadi ukurasa 114.

Orodha ya malalamiko mapya yaliyopelekwa kuanzia mwezi Julai, 2001 hadi tarehe 30 Juni, 2002 ikionyesha aina ya malalamiko na mlalamikiwa imeonyeshwa katika jedwali 6.2 ukurasa wa 115 hadi ukurasa 186.

Mheshimiwa Spika, taarifa ya Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora, kwa kipindi cha kuanzia tarehe 1 Julai, 2001 hadi 30 Juni, 2002 ndiyo ya kwanza tangu shughuli za Tume kuanza na inaelezea shughuli muhimu ambazo zilifanywa na Tume katika kipindi hicho.

Pamoja na kushughulikia malalamiko yaliyorithiwa kutoka Tume ya Kudumu ya Uchunguzi kama nilivyokwisha kueleza, shughuli nyingine zilizofanywa na Tume katika kipindi hicho ni:-

1. Kufanya ziara za kujitambulisha kwa baadhi ya Viongozi Wakuu wa Serikali Tanzania Bara na Tanzania Zanzibar.

2. Kuandaa Muundo *(Organization Structure)* ya Tume.

3. Kuandaa mpango wa kazi wa muda mrefu na mpango wa kazi wa mwaka *(Strategic and Annual Action Plans).*

4. Kuhudhuria mafunzo juu ya Haki za Binadamu na Utawala Bora.

5. Kushiriki katika mikutano ya Kimataifa kwa ajili ya kujenga mahusiano na kujifunza uzoefu wa Tume nyingine zinazoshughulikia masuala ya Haki za Binadamu na Utawala Bora.

6. Kukutana na Sekretariet ya baadhi ya Mikoa kwa lengo la kujitambulisha na kuelezea kazi za Tume. Katika taarifa hii, Tume inaonyesha pia matatizo na changamoto katika kipindi kinachohusika. Maelezo na matatizo na changamoto hizo zipo katika ukurasa wa 198 hadi 199 wa Taarifa.

Taarifa hii Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora ya mwaka 2001/2002 iligawiwa kwa Waheshimiwa Wabunge sambamba na taarifa ya mahesabu iliyokaguliwa na Mkaguzi na Mdhibiti Mkuu wa Serikali ambayo kama mtakavyoona yamepata Hati Safi (*Clean Certificate of Accounts*). *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba nichukue nafasi hii kutoa pongezi na kuwashukuru Waheshimiwa Makamishna na watumishi wa Tume ambao wametekeleza majukumu yao vizuri na hatimaye kuniwezesha kuwasilisha Taarifa hii mbele ya Bunge lako Tukufu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kueleza hayo machache, nakushukuru wewe binafsi na Waheshimiwa Wabunge kwa kunisikiliza. Sasa naomba kutoa hoja kwamba Taarifa ipokelewe na ijadiliwe na Waheshimiwa Wabunge. Ahsante. *(Makofi)*

**WAZIRI WA MAWASILIANO NA UCHUKUZI:** Mheshimiwa Spika, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*

**SPIKA:** Hoja hii haikupelekwa kwenye Kamati yoyote kwa sababu kanuni zinasema Spika ataamua kama hoja fulani ipelekwe kwenye Kamati kwanza au iende moja kwa moja Bungeni.

Waheshimiwa Wabunge hii haikupelekwa kwenye Kamati, kwa hiyo hakuna taarifa ya Kamati. Ila Kambi ya Upinzani ina nafasi ya kutoa maoni yake na nadhani wamejiandaa. Kwa hiyo, namwita Msemaji wa Kambi ya Upinzani Mheshimiwa Dr. Willbrod Peter Slaa atoe maoni ya Kambi hiyo.

**MHE. DR. WILLBROD P. SLAA- MSEMAJI MKUU WA UPINZANI KWA WIZARA YA SHERIA NA MAMBO YA KATIBA:** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Kambi ya Upinzani ninaomba nitoe maoni ya Kambi ya Upinzani kuhusu hoja iliyoko mbele yetu. Kwa kuwa ni mara yangu ya kwanza kusimama hapa ningependa kutoa rambirambi zangu binafsi za wananchi pamoja na watu wote wa mapenzi mema kwa kifo cha Ndugu yetu mpendwa wetu, Mheshimiwa Marehemu Balozi Ahmed Hassan Diria ambaye kwa bahati nzuri nilipata nafasi ya kufanya kazi naye kama mwakilishi wa Bunge letu katika Bunge la *SADC* kwa muda mrefu.

Kwa kweli nilijifunza mengi kutoka kwa Mheshimiwa Marehemu Balozi Ahmed Hassan Diria. Nilifarijika sana kufanya kazi naye na ninapenda Mwenyezi Mungu katika nafasi hii aiweke roho ya Marehemu mahali pema peponi. *Amin.*

Napenda pia kutoa rambirambi kwa familia ya baba yetu Marehemu Paul Bomani Mwenyezi Mungu naye aiweke roho yake mahali pema peponi na kutoa faraja kwa ndugu wote.

Mheshimiwa Spika, pamoja na kwamba taarifa hii tuliipata siyo muda mrefu, lakini maoni ya Kambi ya Upinzani ni kwamba kwanza tunaipongeza Tume ya Jaji Kisanga kwa kazi nzuri walioifanya katika kipindi chote cha 2001 na 2003. Tumefarijika kwamba mambo mengi yameonekana na yameshughulikiwa kwa kiwango fulani na ninamshukuru Mheshimiwa Waziri kwa kuiwasilisha kwa ufasaha vilevile.

Mheshimiwa Spika, ninapenda kuongelea maeneo machache kama manne hivi. Eneo la kwanza, ambalo Kambi ya Upinzani tungependa kutoa maoni yetu ni kuwa masuala mengi yaliyowasilishwa kwa Tume yanahusu unyanyaswaji wa wananchi au kwa makundi au watu mbalimbali binafsi na vyombo mbalimbali vya dola. Hasa kubambikiziwa kesi na polisi; kufunguliwa kesi za kusingiziwa zikiwemo kesi mbaya na ngumu kama kesi za kukutwa au kutumia silaha ambazo mara nyingi hata rufaa yake inakuwa ni ngumu au mdhamana wake unakuwa ni mgumu.

Kuna malalamiko dhidi ya kunyanyaswa na Mahakama ambayo yenyewe ni chombo cha kutoa haki inakuwa vigumu kwa mwananchi wa kawaida akimbilie wapi iwapo Mahakama ambayo ndiyo chombo cha haki na chenyewe ndiyo kinaninyanyasa. Matukio ya aina hiyo yako mengi katika jedwali lililotolewa. Tuna malalamiko pia mengi yametolewa dhidi ya Wakuu wa Wilaya na dhidi ya Wakurugenzi wa Halmashauri haya ni matukio ya wazi ya unyanyasaji yanayotajwa humu.

Kambi ya Upinzani inafikiri kwamba haitoshi tu kuyaorodhesha hapa. Tulifikiri Serikali inatakiwa sasa kuandaa taarifa rasmi ya kuona ni hatua gani zimechukuliwa dhidi ya vyombo hivi. Tunafikiri pia ni wakati muhimu wa kuandaa kwamba hawa wote waliotajwa na kwa bahati nzuri kesi hizi nyingi au kitabu hiki ni vyema kikasomwa na taarifa ya Tume ya Ukaguzi wa Magereza ambayo ilitolewa pia mwaka jana.

Waheshimiwa Wabunge wote waliipata na kwenye taarifa ile Magereza yote yaliyotembelewa nilipata nafasi ya kuhesabu matukio moja moja kati ya Magereza nadhani 42 kama sikosei, matukio 35 ya wafungwa waliohojiwa na Tume yanataja kwamba wako gerezani kwa kesi za kubambikizwa. Haya ni magereza yaliyotembelewa moja moja, watu walihojiwa mmoja mmoja ni vigumu kusema kwamba matukio haya ni ya kutungwa kwa sababu Gereza linapotembelewa halijui kule kwingine nini kilisemwa.

Kwa hiyo, tunaamini kabisa taarifa ile katika kile kitabu cha kwanza na taarifa hii ikiunganishwa kwa pamoja zinatoa picha wazi kabisa kwamba kuna hatua makusudi inatakiwa ichukuliwe na Serikali. Ni imani ya Kambi ya Upinzani kwamba haitoshi sasa

kuleta taarifa, lakini inatakiwa taarifa rasmi inayoandaliwa na Serikali kueleza nini kimechukuliwa au hatua gani imechukuliwa kuhusiana na taarifa ile ya awali ambayo ni *detailed* au ni ya undani zaidi kuliko taarifa sasa ambayo ni majedwali tu hayaelezi kwa kina ni kitu gani kimefanyika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, adha ya wafungwa na hapa kuna kesi mbalimbali zimetajwa na mfano mmoja tu ninachukua ni kesi ya wafungwa walioko Gereza la Ukonga. Wafungwa wamelalamika kwamba rufaa zao hazisikilizwi kwa wakati.

Kwa hiyo, Mheshimiwa Spika, wanakaa Gerezani kwa muda mrefu, hawapati nafasi ya kupewa nakala za hukumu na hivyo wanashindwa kukataa rufaa kwa hiyo, haki haitendeki. Tunadhani kwamba kazi hii inahitaji irekebishwe mara moja kwa sababu haki isipotendeka *Justice delayed is Justice denied* na kama haki haitendeki na mtu yuko Gerezani anakaa pale kwa sababu nakala ya hukumu inashindwa kupatikana. Kwa kuwa tu Serikali haikutoa fedha za kutosha kuchapisha karatasi au makarani hawatoshi kuchapisha nakala mwananchi anapoteza haki yake bila sababu. Tunafikiri kwamba hapa vilevile Serikali ni vyema ikatoa kauli nini sasa kinafanywa baada ya kuwa na Tume hii ambayo inaainisha lakini kwa yenyewe baada ya kuainisha inawasilishwa Serikalini na Serikali inawasilisha Bungeni. Ni juu ya Bunge hili pia nalo kutoa Azimio au kutoa tamko nini kifanyike kwa watu hawa ambao wamekaa hivyo kwa muda mrefu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kesi nyingine ambazo zinawahusu wafungwa ni kesi za wafungwa ambao wamehukumiwa kifo. Kwa bahati nzuri Kamati ya Katiba na Sheria ambayo mimi ni Mjumbe nimetembelea Magereza mbalimbali na katika lalamiko la kwanza tulilopata ni kwamba kuna watu wamehukumiwa kifo wamekaa zaidi ya miaka 6, 7, 8 na hao watu wanapokaa gerezani hawajui nini kinatokea kila asubuhi mlango unapofunguliwa kwa sababu yoyote ile wanafikiria kwamba leo siku imefika ndiyo wanakwenda kunyongwa. Hakuna adhabu kubwa kama hiyo. Hiyo kwa peke yake ni sawa na adhabu ya kunyongwa. Tunafikiria wakati umefika sheria yetu iangaliwe upya. Suala hili la adhabu ya kifo basi ni lazima liangaliwe upya.

Mheshimiwa Spika, kwa bahati mbaya ni kweli Mheshimiwa Rais anapewa nafasi ya kuangalia na kutumia huruma yake au awasamehe au atoe yeye kibali chake wanyongwe. Sheria yetu haimpi Mheshimiwa Rais muda wa kufanya hivyo. Tunafikiri kwamba sasa wakati umefika pia Mheshimiwa Rais angalau awe na muda. Huruma ikizidi inageuka kuwa adhabu.

Tungependa Mheshimiwa Rais awe na muda ambapo ndani ya muda huo kwa kusaidiwa na vyombo vyake aweze kuamua. Ni vyema kama wamehukumiwa basi wafe na kama hawatakufa, basi angalau ipunguzwe ile adhabu wapate adhabu ya kifungo cha maisha. Lakini kuwaacha kwa muda wote ni kweli ni huruma. Lakini huruma inapogeuka kuwa ni adhabu inakuwa ni adhabu mara mbili. Tungependekeza kwamba hilo suala liangaliwe upya.

Mheshimiwa Spika, suala lingine ambalo tumeliona sisi ni suala la Tume kutokuwa na meno. Ni kweli Tume imefanya kazi nzuri sana.

Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba Tume imejitahidi kusikiliza kesi nyingi, Tume imetumia nafasi kuzunguka maeneo mbalimbali, Tume imetoa hata semina mbalimbali kuwaelimisha wananchi, Tume imefanya kazi katika mazingira magumu, wametuambia hawana jengo moja ambapo wanaweza kufanyia kazi yao, hawana watumishi wa kutosha. Lakini pamoja na hayo yote wamefanya kazi kubwa sana. Lakini kuonyesha kwamba Tume haina meno ni mfano mzuri wa kesi iliyofanyika Serengeti ambayo Tume imetumia fedha nyingi za Taifa hili, fedha za walalahoi dhidi ya kesi inayomhusu Mkuu wa Wilaya wa Serengeti pamoja na *OCD* wake. Huyu ni mtu ambaye amepatikana na hatia, Tume imetoa hukumu yake kwamba ni kweli nyumba za wananchi 135 zimechomwa moto kwa agizo la Mkuu wa Wilaya likisimamiwa na *OCD* wa Wilaya hiyo. Tume imetoa siku 90 kwa Serikali kufidia wale watu mpaka leo Serikali imepata kigugumizi.

Mheshimiwa Spika, Kambi ya Upinzani inapenda Serikali itoe tamko ndani ya Bunge hili. Kwanza ni vipi wale wananchi wanafidiwa na lini watafidiwa na pili nini kinafanyika kwa yule Mkuu wa Wilaya ambaye ametumia madaraka yake vibaya pamoja na *OCD* wake.

Mheshimiwa Spika, inasikitisha kila siku tunazungumzia Utawala Bora inapothibitika pale kwamba Utawala Bora umekiukwa na Kiongozi wa Serikali na anaachiwa kazini na wananchi wanyonge wanapelekwa rumande kwa ajili ya kesi ndogo ndogo za shilingi 5,000/=, 10,000/= lakini Kiongozi mzima anachoma mali ya wananchi na tuliambiwa ni ng'ombe wangapi waliungua, tuliambiwa ni mahindi na mazao kiasi gani yalipotea, nyumba 135, maghala zaidi ya 2,000 mtu huyu au watu hawa wawili Mheshimiwa Sabaya pamoja na *OCD* wake Lyimo bado wanadunda tena katika Wilaya hiyo hiyo, katika nafasi hiyo hiyo na wanaendelea eti kana kwamba hakuna kilichotokea na Serikali ipo. Dunia haitatuelewa na inaelekea kwamba Utawala Bora ni kwa maneno si kwa matendo. Vitabu peke yake havitusaidii, taarifa peke yake haitusaidii kama hakuna hatua yoyote inayochukuliwa kwa wale ambao wamethibitika kwa mambo mazito wameyafanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa kumalizia ningependa kusema tu kwamba matukio mengine kwa mfano ya kupandishwa vyeo, utaratibu mbovu wa ajira, yote haya ni mfumo wa Serikali. Kwa kuwa tuko katika wakati wa Utawala Bora, wakati wa uwazi na wa ukweli ni vyema taratibu zetu zote zikaangaliwa ni kwa nini haya mambo yanaendelea kufanyika. Ni lazima kuna kasoro mahali kama utaratibu unakuwa ni mbovu ni wazi kwamba vyeo havipandishwi. Kuna Wizara hazijapandisha watu wake vyeo kwa muda mrefu maelfu, Wizara ya Kilimo na Chakula ni mojawapo ambayo inalalamikiwa sana katika kitabu hiki. Ningependa kujua na Kambi ya Upinzani inataka kujua ni kwa nini hasa Wizara hii ya Kilimo na Chakula imeshindwa kuangalia maslahi ya watu wake. Je, ni mfumo mbaya, je, hakuna uwajibikaji, je hakuna Ofisa anayehusika, je, maafisa *manpower* wanafanya kazi gani. Lakini vile vile tatizo ambalo nimeliona ni kwamba Wizara hii ina utata kwa sababu kuna kipengele kingine kinasema Wizara ya

Kilimo na Chakula halafu inaungana bado na Wizara ya Maji na Mifugo. Kuna watu wa Mifugo bado wako Kilimo hawajui wakimbilie kwa nani hasa kule Wilayani, hawajui uwajibikaji wao unakwenda kwa nani. Tungependa haya mambo ambayo yanagusa haki za mtu mmoja mmoja na makundi ziweze kuangaliwa kwa misingi inayostahili.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo siungi mkono mpaka nipate taarifa ya Serikali na maelezo ya kina hasa kuhusu *DC* wa Serengeti pamoja na *OCD* wake. Lakini nimhakikishie Mheshimiwa Waziri kwamba ninaiunga kazi inayofanywa na Tume yenyewe.

Mheshimiwa Spika, ninamwunga Mheshimiwa Waziri kwa sababu anafuatilia haya mambo lakini napenda Serikali katika umoja wake ituambie ni nini tamko la Serikali kwa Bunge hili na kwa Taifa hili hasa kwa Mkuu wa Wilaya anayeagiza kuchoma na inasimamiwa na *OCD* ambaye kazi yao ni kulinda ulinzi na usalama wa wananchi sasa wameachwa wanaendelea kuwa viongozi wa Taifa hili, tunapenda kupata kauli ya Serikali. *(Makofi)*

**SPIKA:** Waliojiandikisha kuchangia hoja hii ni hawa wafuatao Mheshimiwa Dr Diodorus Kamala, Mheshimiwa Dr William Shija, Mheshimiwa Thomas Ngawaiya na Mheshimiwa John Singo. Wakimalizika hawa nitamwita mtoa hoja ahitimishe hoja yake.

**MHE. DR DIODORUS B. KAMALA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi ya kuchangia hoja hii muhimu. Naomba nianze kwa kusema kwamba naipongeza Tume kwa kazi ngumu inayofanya na ningependa niseme labda hii Tume ikishafanya kazi yake basi vizuri mhusika anapoelekezwa na Tume kwamba kuna haki fulani haikutendeka kama wewe unawajibika kutoa haki hiyo basi ni vizuri ukatekeleza wajibu wako mapema kabla ya kusubiri ripoti nyingine ya Tume kueleza kwamba jambo fulani lilishatajwa kwenye taarifa ya Tume kwamba kabla haijafanyika na bado inaendelea kutofanyika. Kwa sababu kama hatutatekeleza maagizo au mambo mbalimbali ambayo Tume inatuelekeza itakuwa ni kulidharau Bunge lililotunga sheria iliyoiweka Tume hiyo. Lakini itakuwa vile vile ni kudharau Tume yenyewe na vile vile itaonyesha kwamba tunaongea tu Utawala Bora na hatujui maana yake. Huo ni ushauri wangu ambao nautoa kwa moyo wa dhati kabisa.

Mheshimiwa Spika, lakini naomba niseme yako mambo ambayo si vizuri kuyaongea lakini kama yanakuwepo unalazimika kuyaongea. Moja sote tunafahamu kwamba *MV Bukoba* ilipozama Serikali kwa nia nzuri ilitoa kifuta machozi. Lakini hadi leo ninapoongea wapo wananchi 25 ambao hadi leo wanaendelea kudai kifuta machozi. Jambo hili nililiwasilisha kwa Ofisi ya Waziri Mkuu, Mheshimiwa Waziri anayeshughulikia Sera analifahamu na la kusikitisha na baya zaidi kuna mama mmoja ambaye watoto wake wawili walikufa katika hiyo meli na akaandikiwa *cheque* moja lakini baadaye akaambiwa kwa kuwa waliokufa ni watu wawili ni vizuri *cheque* hii tuichukue tuirudishe kwa wahusika ili uandikiwe *cheque* mbili.

Mheshimiwa Spika, sasa hadi leo hii kila nikifungua Ofisi huyu mama anakuwepo kwa Mbunge wake akielezea tatizo hili na mimi namweleza tatizo hili nilishawasilisha

mpaka Ofisi ya Waziri Mkuu linafanyiwa kazi lakini nikamshauri baadaye basi peleka hata kwenye hii Tume ya Haki za Binadamu, lakini mambo ya namna hii yanakuwa ni mambo madogo madogo lakini ambayo baadaye yanageuka yanakuwa kero kubwa.

Kwa hiyo, ningependa nitoe ushauri ni vizuri tukatambua kwamba Haki za Binadamu na Utawala Bora tusiangalie mambo makubwa makubwa peke yake hata haya mambo yanayoonekana kuwa madogo madogo yakiachiwa baadaye yanakuwa makubwa na yanakuwa matatizo makubwa zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mbali na hilo liko lingine ni dogo lakini ni kubwa ukianzia kule Kashenye Mpakani ukaenda kule Minziro, ukaenda Kakunyu sote tunafahamu Serikali ya Tanzania na Serikali ya Uganda tumeamua kuweka sawa sawa mipaka yetu ili ionekane. Kwa sababu hiyo tukaamua kufyeka. Tumefyeka migomba, mibuni tumeporomosha majumba na tumekaa Watanzania na Wakenya, vikao vingi vinakaa wanasema vya ujirani mwema wamekubaliana kwamba fidia ilipwe. Lakini tatizo la vikao hivyo vya ujirani mwema ni moja, hata siku moja Mbunge haitwi kwenye hivi vikao vya ujirani mwema. Lakini wakishakaa kwenye vikao vya ujirani mwema wakakubaliana hawaendi kwa wananchi kueleza walichokubaliana. Matokeo yake Mbunge ambaye wewe kwa sababu wananchi wanakumiliki ukifanya ziara tu unabebeshwa mzigo na kuhojiwa hii fidia iko wapi. Kumbe wapo watu wengine wamekaa kwenye vikao, wamelipwa posho, wamekubaliana watalipa lakini taarifa hazifikishwi kwa wananchi. Kwa hiyo, tatizo lingine linalopelekea kero nyingi nyingi zinazoonekana kwenye kitabu hiki si kwamba ni kero, ni kwa sababu ya watu wanaokaa kwenye vikao kutofikisha taarifa kwa wananchi na kwa hiyo, wananchi wanajenga mawazo kwamba labda haki zao hazipatikani na kwa hivyo wanaendelea kudai na kudai kwa sababu taarifa hazifikishwi. Kwa hiyo, tukijifunza kufikisha taarifa kwa muda muafaka kwa wananchi tutaweza kupunguza kazi ambazo Tume inazifanyia kazi ambazo ingeweza kufanyia kazi mambo mengine.

Mheshimiwa Spika, lakini lipo tatizo lingine maana tunaposema haki za binadamu ni pamoja na mishahara. Ukimwajiri mtu na ukasema utamlipa mshahara ni vizuri ulipe mshahara wake kwa wakati unaofaa. Tulipitisha hapa kwenye Bajeti kwamba kuanzia sasa Watendaji wa Vijiji na Kata sasa watalipwa mishahara na Serikali. Kinachojitokeza ni nini, ukienda kwa wananchi utakuta baadhi ya Watendaji wa Vijiji na Kata hadi leo hii wanadai mishahara ya zaidi ya miezi sita hadi saba. Sasa hii inageuka inakuwa kero kwamba ilikuwaje Mheshimiwa Mbunge sisi tuliambiwa mishahara yetu Serikali Kuu inatulipa na ametuambia mapato ya Serikali yameongezeka lakini mimi sijalipwa mshahara wa miezi sita.

Kwa hiyo, unakuta na wananchi kwa kumwonea huruma huyu Mtendaji wa Kijiji kero inakuwa kubwa inatoka kwa Mtendaji wa Kijiji inakuwa kero ya wanakijiji wote. Kwa hiyo, ningependa mambo ya namna hiyo si lazima mpaka Watendaji wa Vijiji waiandikie Tume kwamba kuna kero kubwa hapa hatujalipwa mishahara yetu miezi sita, Tume ianze kufanya kazi, watu wakae ni mambo ya kiutendaji. Nadhani ndio maana ya Utawala Bora kwamba kila mtu awajibike na tukishasema sasa tunawalipa Watendaji wa Vijiji mishahara basi tuwalipe kweli mishahara. Tukisema Watendaji wakati tunawalipa

mishahara basi tuwalipe. Haina maana kwamba tunaamua halafu hatutekelezi. Kama hilo limeshindikana basi Serikali iseme ili turejee kwenye utaratibu wetu wa kawaida kuliko kusema kwamba tutalipa mishahara lakini hatulipi mishahara na tatizo lake inakuwa kero kwa sababu huyu Mtendaji wa Kijiji na Kata ni watu muhimu kwenye Serikali. Kwa hiyo, si vizuri wakaendelea kujiona wanyonge na wakaendelea kujiona kwamba wanadharauliwa.

Mheshimiwa Spika, lingine ambalo ningependa kulisema ni kuhusu walimu. Imeundwa Tume hapa imefanya kazi nzuri lakini liko tatizo lingine linahusu Bima. Ukiangalia ile Bima ya Maisha *(Life Insurance)* asilimia 90 ya wateja wa *Life Insurance* ni walimu. Lakini ni kwa bahati mbaya sana walimu hawa Bima zao zinapoiva hawalipwi. Ukisoma kwenye hiki kitabu utakuta yako mambo mengi sana hawa wanalalamikia Bima. Sasa Shirika letu hili la Bima hata kama Serikali hatutaki kusema linaelekea kufilisika tukubali kwamba limeshindwa na tukubali kwamba sasa ni kero basi Serikali ichukue wajibu wa kuangalia inamaliza kero hiyo namna gani.

Mheshimiwa Spika, la mwisho ambalo ningependa niliseme si zuri lakini ni vizuri tukalisema tunaposema Utawala Bora ni pamoja na mwananchi kumhakikishia kwamba kama akiibiwa aweze kufika Mahakamani na aweze kufungua kesi. Lakini tatizo linalojitokeza hivi sasa maeneo mengi Vijijini kama mwananchi akiibiwa kwa mfano kuku wake akaamua kwenda Polisi itabidi aingie gharama kwanza za kumlisha huyu aliyemwibia ndicho kinachotokea maeneo ya Vijijini. Wewe kama umeibiwa kuku sasa huyu tutamshughulikia lakini kwanza tulipe fedha za kwenda kumkamata la kwanza itabidi utoe shilingi 5,000/= au 10,000/= ili hao wanaokwenda kumkamata waende kumkamata. Lakini wakishamkamata wanasema ili tuweze kumweka mahabusu hapa inabidi kila siku ulete chai asubuhi, chakula cha mchana na chakula cha jioni vinginevyo tutamwachia, sisi hatuna uwezo wa kumtunza. Lakini haishii hapo inabidi umlipie huyu uliyemshtaki fedha za kumpeleka kwenye Mahakama ya Mwanzo ambayo iko zaidi ya kilomita 100.

Mheshimiwa Spika, sasa mambo ya namna hii unajiuliza Utawala Bora uko wapi na tunafanya nini. Watu wanaokosa haki za msingi ni watu maskini, watu wa chini, watu wadogo wadogo kabisa na sisi tunaokwenda kwenye milango, kila ukikanyaga kwenye mlango wa mpiga kura hayo ndiyo tunayoyapata.

Sasa ni mambo madogo lakini kwa sababu sisi ni wawakilishi wa wananchi lazima tuyaongee katika Bunge hili ili yaweze kusikika na wahusika waweze kuyafanyia kazi na hivyo kupunguza kero na kuzidi kuboresha Utawala Bora na kazi kubwa tuliyofanya ya kumwendeleza Mtanzania na kupambana na umaskini na kuboresha miundombinu isije ikaonekana siyo ya maana kwa sababu ya mambo madogo madogo yaliyojitokeza na hivyo kuvuruga haki na kuwa kero kwa wananchi.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo mimi napenda niseme kwamba naunga mkono hoja na namwomba Mheshimiwa Waziri aendelee kufanya kazi yake. Lakini na Serikali kwa pamoja tusaidiane kwa sababu mambo yanagusa sekta mbalimbali

na sisi kama Wabunge tutaendelea kufanya kazi yetu ya kuwaelimisha wananchi. Kwa hayo, machache nasema naunga mkono hoja mia kwa mia. *(Makofi)*

**MHE. DR WILLIAM F. SHIJA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ili niweze kuchangia hoja hii muhimu juu ya taarifa ya Tume ya Haki za Binadamu iliyotolewa na Mheshimiwa Waziri wa Sheria na Mambo ya Katiba hivi karibuni.

Nianze kwanza kama wenzangu ambao wamepata kuzungumza hapa nitoe salaam za rambirambi kwa familia na ndugu wa Marehemu Mheshimiwa Balozi Ahmed Hassan Diria ambaye alitutoka hivi karibuni. Kusema kweli Mheshimiwa Balozi Diria na mimi nilipata kumfahamu vya kutosha, nimewahi kufanya naye kazi kama Waziri mwenzangu na tukiwa Wabunge kwenye Bunge lako Tukufu amewahi kuwa Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Kudumu ya Mambo ya Nchi za Nje na vile vile aliwahi kuwa Mjumbe wangu kwenye Kamati hiyo hiyo ya Kudumu ya Mambo ya Nchi za Nje. Kwa kweli namwombea Marehemu Balozi Ahmed Hassan Diria roho yake Mwenyezi Mungu ailaze mahali pema peponi. *Amina.*

Mheshimiwa Spika, vile vile napenda nitoe salaam za rambirambi kwa ndugu na jamaa wa Marehemu Mzee wetu Balozi Paul Bomani, ambaye alikuwa mdhamini wetu wa Chama cha Mapinduzi na vile vile tulimfahamu kama muasisi wa Ushirika hapa nchini. Sisi tunaotoka Mikoa ya Kanda ya Ziwa hususan Mkoa wa Mwanza tulifahamu Balozi Paul Bomani kama ni mtu aliyetumia sana ushirika katika harakati za kupigania uhuru wa nchi hii. Napenda niseme kwamba kwa niaba ya familia yangu na kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Sengerema, roho ya Marehemu Balozi Paul Bomani Mwenyezi Mungu aiweke mahali pema peponi. *Amina.*

Mheshimiwa Spika, hoja iliyo mbele yetu mimi naiona ni hoja nyeti na nzito kwa sababu haki za binadamu ndio msingi wa maendeleo. Kama mwananchi hapati haki ni vigumu sana kufanya kazi zake kawaida, ni vigumu sana kuishi na familia yake kawaida na kwa maana hiyo Taifa linaweza likaathirika kwa kiasi kikubwa sana kama wananchi wanakuwa hawapati haki zao za msingi ili waweze kushiriki katika maendeleo na jambo hilo limesemwa vizuri sana katika kitabu kilichoandikwa na mtu mmoja kinachoitwa katika Kiingereza *The State Law and Development.* Katika kitabu hicho mwandishi huyo alibaini vizuri sana kwamba kama mwananchi mmoja mmoja au katika vikundi hapati nafasi ya haki zake kupitia labda nchi yake au Taifa lake anaweza akaathirika sana katika kuchangia maendeleo. Kwa hiyo, mimi nasema hoja iliyo mbele yetu ni ya msingi na napenda nitoe pongezi kubwa sana kwa Tume kwa taarifa nzuri waliyotoa kwa mwanzo huu kwa suala ambalo ni kubwa katika nchi yetu. Natazamia kwamba wataendelea na kazi hiyo vizuri kadri itakavyowezekana.

Mheshimiwa Spika, kwanza nawapongeza kwa maamuzi ya kesi ya Serengeti na naungana na wenzangu walio na mawazo na usemi kwamba utekelezaji juu ya uamuzi wa Tume katika suala hilo ungefanywa na Serikali haraka iwezekanavyo. Kwa sababu hakuna anayeishi hapa nchini au kwenye Taifa letu aliye juu ya sheria na Tume yetu

nzito hii inapokuwa imetoa maamuzi ni vizuri Serikali kwa kweli ikatii na ikachukua hatua ipasavyo.

Pili, napenda nitoe kauli kwa niaba ya wananchi ambao wanaona wanaonewa kwamba Serikali ingechukua hatua kwa wastaafu wa Jumuiya ya Afrika Mashariki wamelalamika sana, wametulalamikia nje ya Bunge, wamelalamika kwa barua, wametutafuta sehemu mbalimbali wastaafu hawa wa Jumuiya ya Afrika Mashariki. Sasa asubuhi wakati wa maswali tulijibiwa kwamba suala hili linafanyiwa kazi. Lakini haitoshi kwa mtu ambaye amefanya kazi anaomba haki yake kuambiwa kwamba suala linafanyiwa kazi. Nafikiri heshima ya Serikali yetu ni kutekeleza jambo ambalo ni haki kwa mtu na haki kwa kundi hili suala hilo tuwe tumelimaliza. Mimi naomba sana Serikali itumalizie jambo hilo kabla hatujaingia mwezi ujao na kuelekea Uchaguzi Mkuu kwa sababu ni haki ya wananchi.

Mheshimiwa Spika, vile vile napenda niunge mkono na kupongeza Tume kwa suala la lililozungumzwa kwenye taarifa juu ya vyombo vyetu mbalimbali kubambikizia kesi wananchi na baadhi yao kubambikiziwa kesi za mauaji. Wananchi Vijijini tunaonana nao wanatueleza kwa malalamiko makubwa na mazito kwamba wanabambikiziwa kesi mara kwa mara ili wanaohusika wapate nafasi ya kujipatia mapato hasa kupitia rushwa. Suala hilo mimi naona Tume imelibaini vizuri, sisi tunaotoka katika maeneo ya wafugaji na wavuvi tunashuhudia malalamiko yanaletwa kwetu mara kwa mara kama Wabunge kwamba wananchi wanabambikiziwa kesi na kwa maana hiyo jambo hili Serikali ingebidi ichukue hatua madhubuti ili ituondolee kero hii nzito ya wananchi wadogo wadogo wanaojisikia mbele ya Taifa lao na Serikali yao kwamba ni wanyonge sana. Upo mchezo kabisa kwa maana ya kutafuta rushwa ya baadhi ya watendaji katika vyombo vyetu Polisi na vyombo vingine baadhi ya Polisi wabaya kubambikizia kesi wananchi wadogo wadogo hasa ikionekana mwananchi ni mfugaji mzuri mahali anaendesha maisha yake ikitokea kwamba kuna mauaji katika sehemu ya jirani yeye ndiye anabebeshwa kesi hiyo ili ng’ombe waanze kuchukuliwa mmoja, mmoja, wawili, wawili hatimaye zizi zima liwezwe kumalizwa kwa sababu wanakuwa wamelenga wale wanaotafuta fedha kupitia rushwa watumie fursa hii ya mali aliyonayo mwananchi.

Mheshimiwa Spika, jambo hilo mimi binafsi huwa linanisikitisha sana kwa sababu kama tunatafuta maendeleo kupitia mmoja mmoja au vikundi kati yetu katika Taifa isingewezekana kabisa mtu akamsonga mtu ambaye amejitahidi, amelinda mali yake amefanya kazi kwa nidhamu, ametunza na hatimaye ameweza kujijengea hali ya kujiondolea umaskini tunamsonga kwa kumbambikizia kesi. Mimi nasema jambo hilo hatuna budi kulifuatilia kwa kina ili tuweze kuliondoa kabisa.

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ni hali kwa ujumla inayozunguzwa katika taarifa ambayo inaonyesha kwamba kuna maeneo mahsusi yanayoonyesha kwamba ndio chanzo cha ukiukwaji wa haki za binadamu. La kwanza nafikiri kama takwimu zingewekwa vizuri zaidi kidogo ni rushwa. Kuna maeneo mengi sana Watanzania kwa bahati mbaya baadhi yetu wamekuwa na taamaa kabisa ya kupokea rushwa na hasa

wanapokuwa katika ngazi ya uongozi. Sasa hali hii ya rushwa lazima tukubali kwamba Tume katika taarifa yake imeibaini na lazima tuishughulikie katika mbinu mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, eneo lingine ni nidhamu kazini ambayo inafanya watu wasilipwe mafao yao, watu wasilipwe mishahara yao, watu wakawiziwe haki zao, watu wapuuzwe na hata wanyanyaswe wakati wanafuatilia malipo yao kwa mujibu wa haki walizonazo. Kwa maana hiyo kama alivyosema Mheshimiwa Rais mwaka 1995/1996 nakumbuka alituambia basi tuweke msimamo wa namna ya kushughulikia rushwa, namna ya kujenga nidhamu kazini, namna ya kuhakikisha wananchi wanalipa kodi na namna ya kuondoa uonevu na kufanya utawala wetu uwe utawala wa sheria.

Sasa uonevu ni eneo lingine ambalo linajitokeza katika taarifa ya Tume kwamba sijui kwa nini baadhi ya Watanzania tumekuwa na utamaduni au tumejenga utamaduni wa kuonea wengine kwa sababu zipi. Maana yake labda tumeishiwa maadili ya kuhakikisha kwamba tunasaidia watu wanaokuja katika hospitali zetu, tunasaidia watu wanaoendesha shughuli zao katika taasisi za elimu, tunasaidia watu ambao wanaendesha shughuli zao katika mambo ya usafirishaji, kwa nini tumeishiwa maadili haya.

Lazima nadhani tutafute sababu hizo na tujenge mfumo mpya ninavyopendekeza kupitia sekta ya elimu tuanzie tukiwa na vijana wetu wadogo wadogo katika taasisi za elimu na mashule tujenge maadili ya kuonyesha kwamba uonevu na kutokuwa na nidhamu hakuwezi kusaidia kupeana haki zetu tunapokuwa tunaishi duniani.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, hilo naliomba kama pendekezo tujenge mfumo wa elimu ambao utakuwa unazungumzia haki za binadamu ili hata Mwalimu asimwonee mwanafunzi na mwanafunzi ajue wajibu wake. Utamaduni wa haki uonekane wazi wazi kwamba tunaujenga mara kwa mara ikiwa pamoja na maadili ambayo tutakuwa tunaendelea kuyajenga. Afrika ina majonzi mengi mno kutokana na ukiukaji wa haki za binadamu. Migogoro mingi inatokea katika nchi za Afrika kutokana na hali hii na migogoro hiyo inasababisha watu kufa wasio na sababu wanakufa, watoto wanakufa, akinamama wanakufa na tunafarakana kabisa kushindwa kuwa na maendeleo yoyote na hatimaye Mabara mengine yanatudharau kwa sababu ya kutokuwa na maendeleo.

Mheshimiwa Spika, naomba nimalizie na eneo lile ambalo Tume imelizungumza vizuri katika ukurasa wa 199. Kwenye ukurasa huo Tume wameweka maombi kwa kweli. Wameonyesha kabisa kwamba Tume ina kazi nyingi lakini katika kazi nyingi hizo ina upungufu wa vitendea kazi ikiwa pamoja na fedha. Napenda kwamba Bajeti ya Tume tuiongeze ili iweze kusaidia wananchi wapate haki zao na wananchi wakipata haki zao watafanya kazi za maendeleo na Taifa hili litapanuka katika uchumi wake na maendeleo ya kijamii na tutaendelea kuishi kwa salama na amani.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hivyo nakushukuru sana kwa kunipa nafasi napenda niseme kwamba naunga mkono hoja hii na kumtakia Mheshimiwa Waziri pamoja na viongozi wa Tume kazi njema, tukumbuke kwamba Mwenyezi Mungu ndiye anayetupa kazi hizi kufanya hapa duniani kwa niaba ya wenzetu. Ahsante sana Mheshimiwa Spika.

**MHE. THOMAS NGAWAIYA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi na mimi nichangie kidogo kuhusu hiki chombo cha haki za binadamu.

Mheshimiwa Spika, madhumuni hasa ya kuweka chombo hiki ni katika hali nzima ya kutenda haki. Tofauti na wanyama, sisi binadamu tumejiwekea utaratibu kwamba tufanye haki mpaka hapa mwisho, usimwonee mwenzako, mkubwa usimpige mdogo kwa hiyo, kukawepo na vyombo mbalimbali. Lakini baada ya hivyo vyombo mbalimbali kama Mahakama na Serikali yenyewe bado wakaona kuna haja ya kuweka chombo cha juu kabisa ambacho ni hiki chombo cha haki za binadamu. Nashukuru sana kwa mawazo hayo ambayo Serikali iliunda hiki chombo ambacho sasa hivi ndiyo tunakisemea hapa.

Mheshimiwa Spika, tatizo langu kubwa katika chombo hiki ni kwamba hawana meno. Hiki chombo hakina meno na kwa kweli wananchi hawajui kwamba kuna chombo kama hiki cha haki za binadamu kwa sababu hawajaona *impact* yake. Wananchi wanajua kuna Polisi kwa sababu mtu anawekwa ndani, wanajua kuna Mahakama unahukumiwa, lakini hiki chombo mpaka leo kama tunavyosema kuhusu hili suala la Serengeti hata hilo tu ambalo ni la wazi wazi kabisa limeshindikana kutekelezwa.

Kwa hiyo, mimi nilikuwa natoa rai kwamba chombo kama hiki ni kikubwa mno. Kwa sababu baada ya kuangalia kuwa haki zinapatikana Mahakamani lakini Serikali ikaona kuna haja ya kuweka chombo kingine ambacho kitaangalia pande zote kiangalie watu wanaonewa haki za binadamu. Sasa lazima kiwe na meno, kiwe na mipaka ya kusema kwamba sasa hapa ni mwisho tunaamua hili na litendeke.

Mheshimiwa Spika, nikisoma hapa kwenye ripoti yao ukurasa 215 inaelezea vizuri sana. Ukisoma hapa ni tofauti na haya ninayoyasema, kwa sababu hapa inaonekana kuna meno lakini hawataki kuyatumia. Kwa sababu wanasema: *"Status Powers and Competence of Commission?"* Namba 15 (b) (i) wanasema kwamba: *"an aggrieved person acting in such person's own interest, (ii) an association acting in the interests of its members; or (iii) a person acting in the interest a group or class of persons."* Nimeamua kusoma hiyo kwa makusudi hasa hiki kipengele hapa *a person acting in the interest of a group or class of persons.*

Mheshimiwa Spika, kuna makundi kama Vyama vya Siasa ambayo kwa makusudi yanakiuka haki za binadamu. Hiki chombo kipo kinaona kwa sababu haifanyiki kwenye uficho, kinafanyika waziwazi. Sasa niliulize hiki chombo cha Haki za Binadamu kinangojea tu mpaka kipelekewe au kikiona hata mtu anachinjwa hapo barabarani kinaweza kikaingilia kati? Kwa sababu mtu anaweza kuwa anaonewa tu hapo na hiki chombo kiko kinaona. Je, hakiwezi kuingilia kati kikaona kwamba hapa kuna haki inavunjwa na sheria zimeruhusu hapa kwa hiyo, tuingilie kati? Nimekwishasema kwenye vyama vyetu vya siasa, kwenye makundi mbalimbali ambayo unakuta mtu anatumia *interest* zake kwa kuumiza wenzake wadogo na hiki chombo kipo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ningeomba hiki chombo kiangalie sasa kwa kutumia sheria hii niliyosoma hapa kwenye kitabu, sheria hii hapa ambayo ina-*govern* hiki chombo basi itumie kwa kuzingatia na kufuatia hayo ambayo niliyosema hapa kwamba Vyama vya Siasa vilivyoko vinaingilia uhuru wa haki za mtu na vinatoa maamuzi ambayo yanaenda kinyume na Haki za Binadamu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nataka nieleze tu hapa, wengi watafikiri labda ni kwa sababu ya Chama cha *TLP* kwa Mrema, lakini viko vyama vingine vingi. Huo ni mfano tu mmojawapo lakini viko vingine vingi ambavyo Tume inatakiwa iangalie kutokana na sheria yake yenyewe ambayo imepewa meno hapa. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, kuna haki zingine za waziwazi zinadhulumiwa. Mimi nilikuwa naangalia kwenye *television,* machozi yakawa yanatoka. Nilivyokuwa naona jinsi wazee wa pensheni wanavyokamatwa na *FFU* pale Dar es Salaam na ilionyeshwa kwenye *television* hawa viongozi wa Tume ya Haki za Binadamu wapo wanaona. Je, wamekemea? Wameuliza au wameona ni kawaida?

Sawa wameandamana lakini wale ni wazee, *FFU* ya nini wakati mzee hana silaha, sasa unampelekea *FFU* akafanye nini? Si unamsikiliza tu na unamwambia tulia, lakini kumpelekea *FFU* mzee halafu unampakia kwenye karandinga mzee, baba yako. Kwa kweli kitendo kile kiliniuma na mimi nasema kuwa ndiyo mambo ambayo nimeyasoma kwenye kitabu hiki ambayo yanatakiwa yatekelezwa kisheria na chombo hiki cha Tume ya Haki za Binadamu.

Watu wanadhulumiwa mazao yao, watu wanakwenda huko wasomi/wafanyabiashara wananunua mazao wanasema tutakupa hela *cash,* mkulima anakaa huku anasubiri hela miaka nenda rudi anasema namwachia Mungu. Chombo hiki cha Haki za Binadamu, kipo kinaona mkulima maskini ambaye hajui chochote anasema namwachia Mungu na chombo hiki kipo.

Mimi ningesema hapana, nasema sheria hii kama ni kweli ukurasa huu niliosoma wa 215 naomba muipitie kwa uangalifu ili kutekeleza sheria hii kama ilivyo. Siamini kwamba meno hakuna kwa kuzingatia sheria hii niliyoisoma hapa. Mimi naona meno yapo, labda utekelezaji unakuwa na matatizo. Kwa kuwa chombo hiki cha haki za binadamu ni kikubwa, ukiona kwamba wanatoa maagizo hayatekelezeki, unaweza kurudi kwa wananchi ukawaambia bwana, mimi nafanya hizi kazi, lakini maagizo yangu hayakutekelezeka kuliko kukaa kimya na wananchi kutoona kwamba kuna chombo ambacho kinawasaidia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nasema tena kwamba umenipa nafasi nakushukuru kwa kunisimamisha tena hapa. Mimi mwenyewe natoa mfano wa kwangu binafsi. Nimekuwa na kesi Dar es Salaam ya maandamano ilikuwa ya mwaka 2001. Kesi hiyo niliripoti na nilikwenda kwa Mheshimiwa Jaji Robert Kisanga nikampa malalamiko yangu na akasema atayafanyia kazi, lakini nataka niwahakikishie hapa leo hii ni mwaka 2005 na ndiyo tunamalizia Bunge na hiyo kesi haijaisha na sijawahi kuitwa kuulizwa ilikuwaje hata kwenye hiyo Tume pamoja na kupeleka malalamiko ili nitoe taarifa vizuri. Sasa hiyo

haki iko wapi? Kwa sababu mimi nimekwenda mwenyewe, sikuitwa kuulizwa vizuri. Je, ambaye si Mbunge wa huko kijijini au wa huko asiyejua chochote atapata wapi haki? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nataka nitoe maelezo hapa kwamba kama duniani wananchi hawapati haki ndiyo ugomvi unapotokea. Haki ndiyo msingi wa binadamu, haki ndiyo msingi wa Serikali, bila haki Serikali haiwezi ikatawala vizuri. Lakini kukiwa na haki Serikali inatawala vizuri tena inalala usingizi hakuna matatizo. Tuangalie utendaji wa chombo hiki ambacho kinatutenganisha sisi kutofautiana kati ya binadamu na wanyama. Kwa sababu mnyama mkubwa anampiga mdogo au anammeza mdogo, lakini sisi tunasema hapana hakuna hilo. Ndiyo maana narudia tena na narudia tena na tena kwamba naishukuru Serikali kufikiria kuweka chombo hiki. Lakini basi hicho chombo kiwe kazini, siyo kutuletea taarifa nzuri namna hii tu, lakini ebu angalia kesi hizi 3206 ni kesi ngapi ziliisha na hukumu zake zikatolewa? Utakuta labda kesi 3 au 4, bado kesi 3,000 je, ni ngapi zinakuja?

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, nimalizie kwa kuomba Tume hii kwamba itekeleze majukumu, iangalie haki za watu zinazopotea na isingoje kupelekewa tatizo, kama tatizo Tume imeweza kuliona yenyewe ifuatilie. Kulikuwa na Chama cha *TSP*ambacho kilikuwa kinashughulikia wanyama, ukiona mtu amebeba kuku kaning'iniza kichwa chini unamuuliza kwa nini umebeba hivyo? Kwa sababu inaku-pain, kwa sababu ni wajibu wako. Sasa kama chombo hiki cha Haki za Binadamu kipo, wewe utaona mtu anachinjwa hapa barabarani unasema ngoja kwanza walete kesi kwangu, hapana kile unachokiona naomba kifuatiliwe na hao watu wa siasa vile vile waulizwe kwa nini wanakosea hiki na hiki kutokana na kifungu hiki ambacho nimekusoma hapa.

Mheshimiwa Spika, nashukuru sana na naunga mkono hoja hii. Ahsante. *(Makofi)*

**MHE. JOHN E. SINGO:** Mheshimiwa Spika, na mimi naomba nichukue nafasi hii kukushukuru kwa kunipa nafasi ya kuchangia katika taarifa ya Haki za Binadamu na Utawala Bora ya mwaka 2001/2002.

Baada ya kukushukuru nichukue nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Waziri, pamoja na Serikali ya Awamu ya Tatu kwa juhudi ambazo imechukua katika kupambana na kuboresha Haki za Binadamu na Utawala Bora katika nchi yetu. Kiukweli hali halisi iliyokuwepo ilikuwa mbaya sana kuhusu Haki za Binadamu na Utawala Bora. Lakini Serikali hii imeweza kujitahidi sana katika kuboresha haki za binadamu kuhusu haki za wanawake, watoto, walemavu, wazee na vita dhidi ya rushwa. Mimi napenda niipongeze Serikali kwa juhudi zake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, vita dhidi ya rushwa ni vita vigumu sana katika nchi maskini. Kwa hiyo, juhudi ambazo zinafanywa na Serikali zinastahili pongezi kwa sababu rushwa imechukuliwa kama ni sehemu ya mafao ya uzeeni katika nchi yetu sasa. Watu wanaitumia rushwa kama sehemu ya kujiandaa na mafao yao ya uzeeni. Hii inatokana kwa sababu ya mfumo wa ajira ambao unaweka katika hali mbaya na yenye adha mara baada ya kustaafu.

Kwa hiyo, ukiangalia sehemu nyingi ambazo rushwa imekuwa ikitendeka, imekuwa ikitendeka kwa sababu watumishi wa ile sekta wamekuwa wakipata malipo kidogo sana. Sasa ukichukua mfano wa Mahakama, unachukua Hakimu wa Mahakama ya Mwanzo, labda na yule wa Mahakama ya Mkoa, ukalinganisha mshahara wake na wa Jaji, utaona tofauti kubwa sana. Sawa sawa na Mbingu na ardhi. Huyu Jaji akishastaafu tu anategemewa apewe mafao mazuri na gari jipya na huyu Hakimu wa Mahakama ya Mwanzo, akistaafu anategemea kurudi kijijini labda na mshahara ambao haufiki hata 100,000. Sasa hali hii imekuwa ikiwapa tamaa ya rushwa hasa kwa sababu jamii nayo imekuwa haiamini kutendewa haki bila kutoa chochote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa sababu hiyo, hii tofauti kubwa ya mishahara ni adha kubwa katika nchi yetu. Lazima wafanyakazi na watumishi wa umma walipwe kulingana na ujira wao, kulingana na kazi yao wanayofanya na hiyo itasaidia kupunguza ya kasi ya rushwa. Huko katika Mahakama zetu viko vitendo vingi ambavyo vinawanyima watu haki zao. Kwa mfano, Bunge hili limepitisha sheria ya ardhi na kupitisha yale Mabaraza ya Ardhi katika ngazi za Vijiji, Kata, Wilaya na Mkoa lakini bado kesi za ardhi zinashughulikiwa na Mahakama. Mfano mzuri ni kule kwangu Same yale mabaraza hayajaanza kufanya kazi, kwa sababu gani sijui. Bado Mahakama zinaendelea kuhukumu kesi za ardhi kwa sababu gani? Serikali iliona kesi za ardhi ziwe na mabaraza yake kwa sababu ilionekana kwamba zilikuwa zimeleta hali ambayo haina haki na usawa.

Kwa hiyo, mimi ningeomba Serikali pale inapofanya maamuzi uwepo ufuatiliaji na kuona kwamba mambo yanafanyika kama ilivyoamuliwa badala ya kwenda kinyume. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lingine kuhusu Mahakama zetu wanaomba hati ya hukumu ili wakaombe utetezi kwa sababu pale katika Mahakama ya Mwanzo, hawaruhusiwi utetezi. Sasa Serikali iweke nafasi ikiwezekana, watu wanaokwenda na kesi zao katika Mahakama za Mwanzo, waruhusiwe kupata utetezi au uwakili. Kwa sababu siyo watu wengi wenye uwezo wa kufika Mahakamani na kujitetea, wengi wanapofika pale wanapata hukumu kwa sababu ya *ignorance of the law na ignorance of the law* siyo sababu ya kuweza kutopata hukumu. Sasa watu wengi wanapata hukumu kwa sababu ya kutoijua sheria.

Mheshimiwa Spika, wakati mwingine Mahakama zinakataa kutoa hati ya hukumu kwa sababu gani? Ninafahamu kule kwangu mahali ambapo wananchi wengi wamekuwa wakidai hati za hukumu wananyimwa mpaka ule muda unakwisha wa kuomba rufaa, ndiyo apewe. Wakati huo akipewa, muda umeshakwisha kwa hiyo, hawezi kuomba rufaa. Hii ni kumnyima haki yake mwananchi.

Mheshimiwa Spika, tunakuja kwenye *PCB*. *PCB* mimi naipongeza Serikali kwamba ilikuwa na miguu huko katika Taifa, lakini sasa imekwenda mpaka katika ngazi ya Mkoa, Wilaya na ninaambiwa ngazi nyingine itakayofuata ni Kata. Lakini *PCB* yenyewe inavyokwenda haikuwezi kufaulu katika vita dhidi ya rushwa.

Mimi ningefikiri hizi sehemu ambazo ziko katika Mkoa, Wilaya na Kata itakapoundwa pawepo na Kamati ndogo ndogo za kuweza kufanya kazi na ule uongozi wa *PCB* badala ya wao wenyewe kufanya kazi peke yao. Hii inaweza ikawapelekea na wao wenyewe ambao wanahusika na kupambana na rushwa na wenyewe wakatumbukia kwenye rushwa. Lakini wakiwa na Kamati ndogo ndogo inakuwa ni jinsi moja ya kuwalinda na rushwa. Wastaafu wakimaliza kipindi chao cha kazi, kwa nini wasubiri mpaka hundi iandikwe aende, arudi, apandishe kwa sababu gani?

Kama mtumishi anamaliza kazi yake, Serikali inajua apewe hela yake pale pale. Kama ambavyo inavyotokea hapa inajulikana anamaliza kazi tarehe 21 leo basi ategemee kwamba kesho tarehe 22 anapewa hundi yake na kupewa mafao yake anaondoka kwenda zake. Vinginevyo Serikali isimwambie arudi nyumbani, arudi nyumbani kufanya nini? Serikali inajua huyu mtu alikuwa anawekewa mafao yake na inajulikana tarehe anayoondoka ni kwa nini asubiri akakae nyumbani afanye kufuata? Hii ni kumnyima haki yake ya msingi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, wastaafu wetu kule wanadhalilika sana. wanaporudi nyumbani hawana njia ya kuweza kupata huduma za kawaida katika maisha, kwa mfano maji, umeme na matibabu kwa sababu wamestaafu hawana kipato tena. Serikali za nchi zingine wamekuwa waki-*subsidize* wakitoa ruzuku kwa ajili ya kuwalipia maji, umeme na matibabu.

Mimi nafikiri watu ambao wameitumikia Serikali kwa muda mrefu na shamba lao limekuwa ajira hakuna sababu kwa nini Serikali isiweze kuwapatia ruzuku ya kuweza kuishi vizuri maisha yao badala ya kuingia katika adha ya kuweza kuwatia katika magonjwa ya *stroke,* ya *pressure* na magonjwa ya sukari. *(Makofi)*

Wastaafu wengi wanakuwa wao ni *victim* wa magonjwa hayo ya *stroke.* Akifikiri hili na lile huwezi kujumlisha ukapata jibu hatimaye anagongwa na *stroke.* Sasa tuweze kuwawekea katika hali nzuri ambayo na sisi tunaelekea kule ili waweze kuishi vizuri na waweze kupata haki yao wanayostahili.

Pale wanapodai hakuna sababu Serikali kuwaletea askari kama watu wamekuja kudai kwa nidhamu kwa nini Serikali itumie askari? Mtu anadai haki yake Serikali inamzuia kwa sababu gani? Kwa nini Serikali imchukulie hatua wakati ana madai yake? Mfano ni wale wazee wastaafu wa Afrika Mashariki, ile ilikuwa ni haki yao ya msingi lakini anabebwa aingizwe katika karandinga ili akashitakiwe kwa lipi? Mimi nafikiri Serikali ikubali kuwa na *dialogue* na watu ambao wanadai haki zao. Serikali isikubali kutumia mabavu pale ambapo watu wanadai haki zao. Kuwe na *dialogue,* kuwe na maongezi hata mtu unamwajiri kuna maongezi, hakuna mapambano ya ajira. Sasa leo hukumpa haki yake kwa nini hamuongei badala yake unatumia vyombo vya dola? Huu ni ukiukaji wa haki za binadamu. *(Makofi)*

Sehemu nyingine ni huu mfumo wa haki za binadamu wenyewe, uko huko Taifani tu, Mikoani hakuna kama ile ya *PCB* Wilayani hakuna na nafikiri nao

wangeweka *structure* mpaka katika ngazi ya Mkoa, Wilaya na Kata, ili wananchi waweze kupata hiyo elimu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lingine ni wananchi wetu hawaelewi hili somo la Haki za Binadamu na Utawala Bora. Serikali ichukue juhudi za makusudi kabisa kuwa na vitengo vya kuwaelimisha watu katika ngazi za Kata, Wilaya, Mkoa. Kwenye Taifa tumejitahidi sana katika vyombo vya habari na magazeti kuelimisha jamii. Lakini si watu wote vijijini wanapata hiyo nafasi. Sehemu nyingine ya kufikisha elimu hii ni katika mitaala ya shule zetu za msingi na sekondari. Mtoto anapokuwa shuleni aanze kujifunza haki zake za msingi za binadamu, aanze kujifunza ubaya wa rushwa.

Kule Ulaya, mtoto mdogo nilikwenda kule baba yake anataka kumpiga anasema nitapiga simu kwa Haki za Binadamu kwamba baba anataka kunipiga. Maana amefundishwa shuleni. Sasa na huku kwetu kuna kila sababu ya kufundisha katika shule zetu Haki za Binadamu, zinazohusu wanawake, zinazohusu watoto, zinazohusu walemavu, zinazohusu wazee na watu wa aina zote ili hata akiwa raia kamili wa nchi hii anajua haki zake.

Mheshimiwa Spika, Utawala Bora katika Serikali ya Awamu ya Tatu umeweza kufanya juhudi sana ya kufanya mabadiliko makubwa nikilinganisha na huko tulikotoka. Kwa hiyo, mimi napenda nichukue nafasi hii ya kumpongeza Waziri pamoja na Serikali kwa jumla kwa kazi nzuri inayofanya na iendelee kuweza kuboresha maeneo hayo hasa sehemu ya Mahakama.

Baadhi ya Mahakama ziko katika majengo ambayo yamekwisha kabisa. Lakini ninazo taarifa kwamba Serikali ina juhudi ya kujenga Mahakama ambazo zina hali mbaya kwa ajili ya kuwapatia watu haki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo mimi napenda kuunga mkono taarifa ya Mheshimiwa Waziri, pamoja na kumwomba juhudi za kuweza kufanya vizuri zaidi katika Haki za Binadamu na Utawala Bora ziweze kufaulu. Ahsante. *(Makofi)*

## MICHANGO KWA MAANDISHI

**MHE. REMIDIUS E. KISSASSI:** Mheshimiwa Spika, napenda kutoa salaam za rambirambi kwa familia za Marehemu Balozi Hassan Diria na Balozi Paul Bomani kwa misiba mikubwa iliyowapata. Mungu azilaze roho za Marehemu mahali pema peponi. *Amina.*

Mheshimiwa Spika, vile vile napenda kuipongeza Tume hii ya Haki za Binadamu na Utawala Bora kwa kazi nzuri wanazofanya katika mazingira magumu. Pamoja na hayo naomba kutoa ushauri na mapendekezo yafuatayo:-

Kwanza, Ofisi ya Tume iliyopo Zanzibar iimarishwe zaidi na kujitangaza kwa wananchi ili ieleweke na hasa kazi zake.

Pili, Tume ikae na Polisi, Magereza na Mahakama ili malalamiko ya kero za watu waliopo Magereza ambao si wafungwa, basi kadhia zao zipatiwe ufumbuzi wa haraka.

Mheshimiwa Spika, napenda kuipongeza tena Tume na iendelee na kazi nzuri inayoifanya. Ahsante.

**MHE. PONSIANO D. NYAMI:** Mheshimiwa Spika, kwanza napenda kutoa pongezi kwa Tume kwa kazi nzuri inayoifanya. Haki itendeke, polisi kama chombo cha haki. Rushwa ndiyo wimbo na sala yao. Utaingia bure polisi na kutoka kwa fedha maana ni mradi wa Serikali.

Mheshimiwa Spika, rushwa na kutotenda haki kwa Mahakama zote nchini. Asilimia 98 ya Mahakimu nchini ni wala rushwa, wanyanyasaji na wasiotenda haki. Mlalamikaji na mlalamikiwa wote huwa ni bidhaa na mtaji wa Mahakama. Ajira kwa wanawake ni burudani kwa maafisa uajiri maana miili ya wanawake hugeuka kuwa sifa ya kuajiriwa. Sifa ni ngono.

Katika baa, *bar maid* hunyanyaswa kwa baa kufungwa kati ya saa 7 hadi 9 usiku. Mshahara mdogo, kufukuzwa ovyo na bila kupewa mshahara wake. Wanabakwa na kuuawa ovyo kutokana na kufunga muda mbovu na bila kupewa usafiri. Haki haitakuwepo kamwe na ni ndoto endapo polisi na Mahakama kama vyombo vya haki kwa raia havitajirekebisha na kutenda haki waachane na rushwa. Mbona *JWTZ* hawalalamikiwi kwa ulaji wa rushwa?

**MHE. SEMINDU K. PAWA:** Mheshimiwa Spika, nampa pongezi Mheshimiwa Waziri kwa kupata hati safi. Taarifa hii ni ya mwaka 2001/2002. Kwa nini majedwali mengine ya 6.1, 6.1.2, 6.1.3 yanaonyesha kazi za mwaka 1998/99, 2000/2001, 1999/2000 kulikoni?

Mheshimiwa Spika, jedwali linaonyesha Tume, imepokea, inatoa namba inataja aina, inataja mwajibikaji lakini haitajwi hatua iliyofikiwa hadi leo mwaka 2005 hata zile za 1998/1999 ziko *intact.*

Mheshimiwa Spika, ombi, naomba wananchi wa Mikobora wanashitakiwa na Meneja wa shamba la *DAFCO* na kuhukumiwa wote 260 walipe faini 5,000/= kila mmoja. Je, hii ni sahihi kwa Mahakama ya Mwanzo? Wafanyabiashara masokoni wanapofukuzwa na kubomolewa vibanda vyao mfano soko la majengo watumie utaratibu upi kuiona Tume?

**MHE. DR JAMES M. WANYANCHA:** Mheshimiwa Spika, napenda kukushukuru kwa kunipa nafasi ili nami niweze kuchangia hoja hii.

Tume ya Haki za Binadamu imeshashughulikia kesi ya Nyamuma, Wilayani Serengeti na kutoa hukumu. Mimi ninachoomba ni maelezo ya Serikali kwa nini hadi leo hawa waliofanya makosa hawajawajibishwa kama Tume ilivyoamua? Je, lini wananchi wa Nyamuma watalipwa haki zao?

Mheshimiwa Spika, siungi mkono hii hoja mpaka nipate maelezo.

**WAZIRI WA SHERIA NA MAMBO YA KATIBA:** Mheshimiwa Spika, kwanza napenda kuchukua nafasi hii kushukuru kwa kunipa nafasi ya kuhitimisha hoja hii, inayohusu Bunge lako Tukufu kuweza kupokea na kuijadili Taarifa ya Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora kwa kipindi cha mwaka 2001/2002.

Mheshimiwa Spika, awali ya yote ningependa nichukue fursa hii kuwatambua Waheshimiwa Wabunge ambao wamechangia kwa kuzungumza nao ni wafuatao, Mheshimiwa Dr Willbrod Slaa, Mheshimiwa Dr Diodorus Kamala, Mheshimiwa Dr William Shija, Mheshimiwa Thomas Ngawaiya na Mheshimiwa John Singo. Aidha, niwashukuru waliochangia kwa maandishi nao ni Mheshimiwa Remidius Kissassi, Mheshimiwa Semindu Pawa, Mheshimiwa Dr James Wanyancha na Mheshimiwa Ponsiano Nyami.

Mheshimiwa Spika, michango imekuwa ni mingi ambayo imetolewa na Waheshimiwa Wabunge na maoni ambayo wameyatoa ni mazito. Kwa muda ambao umenipa kwa kweli haitawezekana kuweza kuyajibu yote. Lakini niseme kwamba Wizara imeyapokea mambo yote ambayo yamezungumzwa, michango yote ambayo imetolewa na Waheshimiwa Wabunge, nasema tumeyapokea sisi kama Wizara, sisi kama Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora. Makamu wa Mwenyekiti wa Tume, yupo hapa, Mtendaji Mkuu wa Tume yupo, Mkurugenzi ndani ya Wizara anaye husika na masuala ya haki za binadamu na Katiba yupo. Wote wameyasikia yote haya. Kwa hiyo, nasema tumeyapokea ni mawazo mazuri na sisi tutayafanyia kazi. *(Makofi)*

Sasa baada ya kusema hayo, labda moja tu ambalo inabidi unipe ruksa dakika mbili, tatu niweze kulisema ambalo linahusu suala hili la Serengeti. Ningependa nisome hili. Serikali imechukua hatua gani kutekeleza mapendekezo ya Tume kuhusu suala hili la Serengeti? Nikianza na jinsi Serikali inavyotekeleza mapendekezo ya Tume kwa ujumla Tume yenyewe imesema kwamba vyombo mbalimbali vilivyolalamikiwa viliondoa kero zinazozihusu kwa msukumo wa Tume. Malalamiko yanayohusu sheria yamekuwa yakishughulikiwa kwa njia ya marekebisho ya sheria hizo kupitia Bunge hili. Hata hivyo ni wazi kuwa baadhi ya malalamiko yaliyotokana na kutojua sheria na taratibu kwa upande wa walalamikaji.

Hatua nyingine za Serikali katika kutekeleza mapendekezo ya Tume, ni viongozi wanaohusika kuchukua hatua mbalimbali kama inavyowezekana ili kuondoa kero zinazohusika. Kwa malalamiko yanayotokana na uhafifu wa raslimali kama ilivyo kwa Mahakama, hatimaye Serikali imeongeza Bajeti yake. Kuhusu hili la Serengeti niseme tu kwamba Tume imewezeshwa kufanya kazi zake kule Musoma, wamekwenda kwa kipindi cha miezi mitatu wakasikiliza hoja za pande zote mbili, wale walalamikaji wananchi katika maeneo yale na kwa upande wa Serikali yenyewe nao wakaweza kutoa hoja zao. Baada ya hapo, Tume imetoa ripoti yake, kuhusu suala la Serengeti na sisi tumeipokea pale Wizarani tunaifanyia kazi na inabidi kwa kweli tutazame sisi kama

Wizara na kama Serikali, pande zote mbili, wanaolalamikiwa na walalamikaji ili tuweze kuishauri Serikali nini cha kufanya. Siyo kwamba tumekaa tu hatufanyi lolote.

watakwenda mbele ya Jaji Robert Kisanga na Makamishna wahusika kulizungumzia suala hili kwa maana ya sisi kutoa maoni yetu. Baada ya hapo tunaweza kumshauri Rais na Serikali kwa ujumla ni nini cha kufanya. Kwa hiyo, ndiyo hatua ambayo tumeifikia. Sasa nirudie tena kusema kwamba haya yote ambayo yamezungumziwa tumeyapokea na nasema tunayafanyia kazi na kuwaandikia Waheshimiwa Wabunge majibu kwa hoja hizo mbalimbali ambazo wamekuwa wakizitoa.

Baada ya kusema hayo, nakushukuru wewe binafsi na Waheshimiwa Wabunge kwa kunisikiliza na naomba kutoa hoja kwamba baada ya mjadala, sasa taarifa hii ipokelewe. Naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**WAZIRI WA ELIMU NA UTAMADUNI:** Mheshimiwa Spika, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*
*(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)*

*(Taarifa ya mwaka ya Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora Julai 2001 - Juni, 2002 ilipokelewa na kujadiliwa na Bunge)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tofauti na maazimio mengine yanayoletwa na Serikali ili yaridhiwe na Bunge hili, taarifa hii haikuletwa ili iridhiwe na Bunge. Sheria inasema taarifa hiyo itawasilishwa Bunge, ipokelewe na kujadiliwa siyo kuridhiwa.

Ndiyo maana hoja inasomeka hivyo kwenye *Order Paper.* Kwa hiyo, sasa nitawahoji ili Bunge likubali kwamba limepokea na kujadili taarifa ya mwaka ya Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora kwa kipindi cha Julai, 2001 hadi Juni, 2002.

## MAAZIMIO

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, yako Maazimio mawili yatakayowasilishwa na Waziri wa Sayansi, Teknolojia na Elimu ya Juu. Utaratibu wetu wa kawaida ni kwamba yanawasilishwa, kama ni Waziri mmoja anawasilisha yote kwa pamoja, halafu yanajadiliwa kwa pamoja baadaye. Kwa hiyo, namwita mtoa hoja atoe hotuba zake mbili kwa mfululizo. *(Makofi)*

### Azimio la Kuridhia Chuo cha Ufundi Mbeya kuwa Taasisi ya Sayansi na Teknolojia inayojitegemea *(Mbeya Institute of Science and Technology - MIST)*

### Azimio la Kuridhia Mkataba wa Kimataifa unaohusu Utunzaji na Ulinzi wa Vyanzo vya Nyuklia *(Convention on the Physical Protection of Nuclear Material)*

**WAZIRI WA SAYANSI, TEKNOLOJIA NA ELIMU YA JUU:** Mheshimiwa Spika, mbele yako kuna Maazimio mawili ambayo nawasilisha mbele ya Bunge lako Tukufu. Ninaanza na Azimio la Kuanzisha Taasisi ya Sayansi na Teknolojia Mbeya yaani *The Mbeya Institute of Science and Technology,* kwa kukipandisha hadhi Chuo hicho cha Ufundi.

Mheshimiwa Spika, mbele yako lipo Azimio hilo linalopendekeza Chuo cha Ufundi Mbeya kilichoanzishwa mwaka 1986 kipandishwe na kubadilishwa hadhi kuwa Tasisi ya Sayansi na Teknolojia Mbeya yaani *The Mbeya Institute of Science and Technology.*

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa kifungu cha 6, Ibara ndogo 1 cha Sheria Na. 9 ya mwaka 1997 iliyoanzisha Baraza la Taifa la Elimu ya Ufundi, Waziri anayeshughulikia Sayansi, Teknolojia na Elimu ya Juu amepewa mamlaka ya kukipandisha hadhi Chuo au Taasisi yoyote ya ufundi ambayo imepata ithibati kutoka Baraza la Elimu la Taifa na Elimu ya Ufundi kuwa Taasisi inayojitegemea yaani *autonomous* Chuo au Taasisi inayopandishwa hadhi kwa utaratibu huu inaruhusiwa kuendesha shughuli zake za kiutawala na pia kusimamia masuala yote ya kitaaluma ikiwa ni pamoja na kutunga mitihani yake na kutoa tuzo.

Aidha, kifungu cha 6(iii) kinamtaka Waziri anayehusika kuwasilisha mbele ya Bunge lako Tukufu Azimio la Kuridhia Amri ya kuanzisha Taasisi ya Ufundi inayojitegemea na kuanza kufanya kazi.

Mheshimiwa Spika, napenda pia kuishukuru Kamati ya Bunge ya Huduma za Jamii kwa maoni na mchango wao mkubwa ambao umewezesha liwepo mbele yako Azimio la Kuanzisha Taasisi ya Sayansi na Teknolojia Mbeya. Azimio hili limewasilishwa mbele ya Bunge lako kwa lengo la kuridhia kuanzisha kwa Taasisi hiyo.

Mheshimiwa Spika, napenda kuwashukuru wadau mbalimbali ambao kwa njia moja au nyingine wamechangia katika kuwezesha kuwasilisha kwa Azimio hili mbele yako. Aidha, naomba pia kutoa shukrani kwa wataalamu wetu kwa jitihada zao katika hatua zote za matayarisho ya Azimio hili.

Mheshimiwa Spika, Serikali katika harakati za kuondoa umaskini na kuboresha maisha ya Watanzania imeweka kipaumbele katika kuendeleza na kuimarisha sayansi na teknolojia nchini. Aidha, msisitizo umewekwa zaidi katika eneo hili ili kuweza kukabiliana na changamoto zilizopo kutokana na mabadiliko ya haraka ya kiuchumi, utandawazi, sayansi na teknolojia.

Mheshimiwa Spika, katika kukabiliana na mahitaji ya maendeleo ya haraka, Serikali pamoja na mambo mengine imeweza kuanzisha Sera ya Sayansi na Teknolojia ya mwaka 1995, Sera ya Elimu ya Juu ya mwaka 1995, Sera ya Elimu ya Ufundi na Mafunzo ya mwaka 1996, Baraza la Taifa la Elimu ya Ufundi mwaka 1997, Taasisi ya Teknolojia Dar es Salaam, mwaka huo 1997, Dira ya Maendeleo ya 2025 na mpango

kabambe yaani *master plan* ya Wizara ya Sayansi, Teknolojia na Elimu ya Juu ya kuanzia mwaka 2000 hadi kufikia mwaka 2018.

Mheshimiwa Spika, vile vile Serikali imeendelea kuimarisha elimu ya juu na ufundi kwa kuboresha vyuo mbalimbali vikiwemo vyuo vya ufundi vya Arusha, Taasisi ya Teknolojia Dar es Salaam na sasa kukipandisha hadhi Chuo cha Ufundi cha Mbeya, kwa lengo la kuwapata wataalam wenye ujuzi na stadi za kufanya kazi kwa mikono yaani *hands on.*

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo haya, naomba sasa kutoa maelezo mafupi kuhusu Chuo cha Ufundi cha Mbeya ambacho kinapendekezwa kupandishwa hadi kuwa Taasisi ya Sayansi na Teknolojia Mbeya yaani *The Mbeya Institute of Science and Technology - MIST.*

Mheshimiwa Spika, Chuo cha Ufundi Mbeya kilijengwa kwa ushirikiano baina ya iliyokuwa Serikali ya Muungano wa nchi za Kisoshalisti za Kisoviet za Urusi *(USSR)* na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Ujenzi wa Chuo ulianza mwaka 1982 na ilipofika Septemba, 1986 mafunzo ya ngazi ya cheti cha ufundi sanifu yaani *Full Technician Certificate* katika fani za ujenzi, umeme, mitambo na usanifu majengo ulianza kutolewa rasmi katika chuo hicho.

Mheshimiwa Spika, hadi sasa mafunzo katika ngazi hiyo bado yanaendelea kutolewa na Chuo na kwa sasa katika jitihada za kupanua na kuimarisha chuo hiki mwezi Septemba, 2002 mafunzo ya ngazi ya Stashahada ya Juu ya Uhandisi katika fani za ujenzi na mitambo yalianzishwa.

Mheshimiwa Spika, kwa muda mrefu Serikali imefanya jitihada za kufikia azma ya Baba wa Taifa za kukifanya Chuo cha Ufundi cha Mbeya kuwa Chuo Kikuu cha Sayansi na Teknolojia. Juhudi hizi ni pamoja na kupata eneo la ardhi lenye hekta 408 na kulipa fidia kwa wananchi waliokuwa na mali katika eneo hili.

Mheshimiwa Spika, kazi muhimu iliyofuata ni kutumia wataalam washauri yaani *Consultants* kutoka kitengo cha ushauri cha *Bureau for Industrial Corporation - BICO* cha Chuo Kikuu cha Dar es Salaam kutathmini na kutoa ushauri kwa njia bora za kukipandisha Chuo cha Ufundi cha Mbeya. Ripoti ya tathmini ya wataalam hao iliwasilishwa Wizarani mwezi Machi, 2003 na kwa sasa inaendelea kufanyiwa kazi.

Mheshimiwa Spika, dhumuni kubwa la kuanzishwa kwa Taasisi ya Sayansi na Teknolojia inayojitegemea ni kukipa chuo uwezo zaidi wa kupanga na kufanya maamuzi ya mambo yake yenyewe katika azma ya kuboresha utoaji wa elimu ya juu na ufundi. Aidha, Chuo kitakuwa katika nafasi nzuri zaidi ya kuongeza udahili wanafunzi wa jinsia zote kwa kubuni njia mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, inategemewa pia kuwa Taasisi hii itatoa huduma zaidi kwa jamii inayoizunguka Taasisi hiyo na maeneo ya Manispaa ya Mbeya kwa kutoa ushauri wa kitaalam na kufanya tafiti katika viwanda.

Mheshimiwa Spika, inatarajiwa kuwa kubadili Chuo cha Ufundi Mbeya kuwa Taasisi ya Teknolojia Mbeya inayojitegemea, ni mwanzo nzuri kwa safari ya Serikali kutekeleza majukumu yake ya kuhakikisha kuwa elimu inayotolewa kwa wananchi wake ni elimu iliyo bora yenye sifa Kitaifa na ya kiushindani Kimataifa.

Mheshimiwa Spika, kuanzishwa kwa Taasisi hii inayojitegemea kiutendaji yaani *autonomy institution* ina lengo la kukipa Chuo cha Ufundi Mbeya uwezo wa kuamua mambo yake chenyewe ili kutekeleza azma ya kuwa Chuo Kikuu cha Sayansi na Teknolojia, *(The Mbeya University of Science and Technology)* haraka iwezekanavyo na kutoa huduma bora kulingana na ongezeko la mahitahji.

Mheshimiwa Spika, kuanzishwa kwa Taasisi ya Sayansi na Teknolojia ambayo itakuwa ni ya umma kutaongeza changamoto kwa vyuo na taasisi nyingine za ufundi. Hatua hii bila shaka italeta manufaa kwa walengwa kutokana na kwa ufanisi utakaotokana na ushindani wa vyuo na taasisi ya elimu ya juu na ufundi na hata kuwawezesha walengwa kupata mafunzo katika fani mbalimbali ambazo hazipatikani katika vyuo na taasisi nyingine za ufundi nchini.

Mheshimiwa Spika, hadi sasa yafuatayo yamefanyika kuhusu maandalizi ya kukiwezesha chuo cha ufundi Mbeya kuelekea katika mageuzi yanayokusudiwa. Maabara mpya mbili zimejengwa kwa ajili ya kozi za ujenzi *Civil Engineering na mitambo Mechanical Engineering* kwa wanafunzi wa Stashahada ya Juu ya Uhandisi. Ujenzi wa bweni kwa ajili ya wasichana lipo katika hatua za awali. Mpango wa utekelezaji wa miaka mitatu umeandaliwa kuanzia mwaka wa fedha 2005/2006 hadi 2007/2008. Walimu wa Chuo cha uUfundi Mbeya wameendelea kupatiwa mafunzo ya juu katika ngazi ya Udaktari wa Falsafa tumepeleka walimu watano na katika ngazi ya *masters* tumepeleka 12.

Chuo kimepata *accreditation* kutoka Baraza la Taifa na Elimu ya Ufundi. Stashaha ya Juu ya Uhandisi imeanzishwa Septemba, 2002. Baadhi ya miundombinu muhimu imekarabatiwa ikimo barabara za ndani za chuo na majengo. Mashine na mitambo imekarabatiwa na mingine kununuliwa na kufungwa katika karakana, yote niliyoyataja hapa yameshuhudiwa na Kamati ya Bunge lako Tukufu hivi karibuni.

Mheshimiwa Spika, masuala yatakayoshughulikiwa wakati huu wa mpito kutoka hali ya sasa ya Chuo cha Ufundi Mbeya kwenda katika hali ya Taasisi ya Sayansi, Teknolojia Mbeya yaani *The Mbeya Institute of Science and Technology* ni kama ifuatavyo:-

Muundo wa uongozi wa sasa utabadilika na kuzingatiwa katika muundo mpya ambao umeelezwa katika amri niliyoitoa, mitaala itaendelea kurekebishwa ili iendane na mabadiliko ya sasa duniani na mahitaji ya soko, kuendelea kuwapatia elimu ya ngazi ya uzamili walimu waliopo katika chuo cha sasa na kuajiri wengine wenye sifa kama hizo, kuendelea kujenga miundombinu mipya na kuboresha iliyopo, kuongeza mabweni ya wavulana na wasichana, kujenga na kuimarisha maktaba inayokidhi hali ya taasisi

inayotegemewa kuanzishwa na kujenga uwezo na kuimarisha matatizo ya teknolojia ya habari na mawasiliano.

Mheshimiwa Spika, Serikali katika kukiwezesha Chuo cha Ufundi cha Mbeya kuwa Chuo Kikuu cha Sayansi na Teknolojia iliamua kupata ushauri wa kitaalam kutoka Chuo Kikuu cha Dar es Salaam kama nilivyosema. Walimu walipendekeza kuwa Chuo kinaweza kikabadilishwa kwa kufuata mojawapo ya njia mbili, kukibali Chuo Ufundi moja kwa moja kwenda Chuo Kikuu cha Sayansi au kukibadili Chuo cha Ufundi kupitia njia hii ambayo inapendekezwa sasa.

Aidha, wataalam walishauri kuwa njia ya pili yaani *NTC* na hapo baadaye *MIST* ni muafaka zaidi kuliko ile ya kwanza.

Mheshimiwa Spika, kufuatia ushauri uliotolewa na wataalam, Serikali inakusudia kukipandisha hadhi Chuo cha Ufundi Mbeya kwa kutumia kifungu cha 6(i) cha Sheria ya Baraza la Taifa na Elimu ya Ufundi ya mwaka 1997. Aidha, kifungu cha 6(iii) kinampa Waziri mwenye dhamana ya Sayansi, Teknolojia na Elimu ya Juu kutangaza katika Gazeti la Serikali Chuo chochote kile kilichopata ithibati chini ya Baraza hilo huwa Chuo kinajitegemea kutokana na dhamana hiyo nilitoa amri *Establishment Order GNN 535* katika Gazeti la Serikali la tarehe 10 Desemba, 2004 kwa lengo la kuanzisha Taasisi ya Sayansi na Teknolojia Mbeya yaani *MIST.*

Mheshimiwa Spika, kwa muhtasari, amri iliyochapishwa kwenye Gazeti la Serikali la tarehe 10 Desemba, 2004 inabainisha mambo makuu kama ifuatavyo:-

Muundo wa Taasisi, uongozi na utawala, Baraza litakalosimamia Taasisi na majukumu yake, vitivo na Idara zitakazokuwepo na aina ya programu zitakazotolewa na usimamizi na matumizi ya fedha.

Mheshimiwa Spika, kama nilivyotamka hapo awali, kuwa Chuo kinapandishwa hadhi kwa kutumia kifungu cha 6(i) cha Sheria ya Baraza la Taifa la Elimu ya Ufundi ya mwaka 1997. Aidha, kifungu cha 6(iii) kinanipa mamlaka hayo mimi Waziri mwenye dhamana ya Sayansi na Teknolojia kutangaza katika Gazeti la Serikali Chuo chochote kitapata ithbati chini ya Baraza kuwa Chuo kinajitegemea.

Mheshimiwa Spika, kwa kuzingatia Sheria hiyo na kwa kuzingatia kwamba nimekwishatia saini amri Na. 535 iliyochapishwa kwenye Gazeti la Serikali, naomba basi kuwasilisha mbele ya Bunge lako Tukufu Azimio la Chuo kukibadilisha kiwe Chuo cha Ufundi cha Mbeya kuwa Taasisi ya Sayansi na Teknolojia inayojitegemea yaani *The Mbeya Institute of Science and Technology.* Naomba ruhusa sasa nilisome azimio. *(Kicheko)*

KWA KUWA Serikali katika mikakati yake ya kuondoa umaskini na kuboresha maisha ya Watanzania imeweka kipaumbele katika kuendeleza na kuimarisha elimu ya sayansi na teknolojia nchini na kwa kuwa bado kuna mahitaji makubwa ya Wataalam

wenye elimu ya ufundi katika ngazi za cheti, stashahada na shahada zinazolenga kutoa wataalam wenye ujuzi zaidi wa vitendo nadharia;

NA KWA KUWA Sera ya elimu ya ufundi na mafunzo iliyoanza kutumika mwaka 1996 inatamka bayana kuwa Taasisi na Vyuo vya Ufundi nchini viwezeshwe kujitegemea ili viweze kubuni na kutoa maamuzi ya haraka ya utekelezaji wa mipango yake ya maendeleo kwa lengo la kupanua na kuboresha utoaji wa elimu;

NA KWA KUWA Chuo cha Ufundi Mbeya kikiwezeshwa kujitegemea kama sera inavyoelekeza kitapata nafasi nzuri na uwezo wa kubuni na kutoa maamuzi ya haraka ya utekelezaji wa mipango yake ya maendeleo kwa madhumuni ya kuboresha elimu itolewayo;

NA KWA KUWA baada ya Chuo kuboreshwa na kupanua programu zake kitaweza kutoa wataalam ambao ni wanasayansi na wanateknolojia wenye mwelekeo wa vitendo zaidi kuliko nadharia na wenye kukubalika katika soko la ajira na mfumo wa sasa wa utandawazi;

NA KWA KUWA wataalam waelekezaji walipendekeza kwamba ili Chuo cha Ufundi Mbeya kiweze kugeuzwa kuwa Chuo Kikuu cha Sayansi na Teknolojia, ni vema kwanza kikawa Taasisi ya Sayansi na Teknolojia inayojitegemea ili kuweza kujenga uwezo wa ufundishaji, kuimarisha na kuongeza miundombinu na pia kuimarisha uongozi wa chuo;

NA KWA KUWA katika kifungu cha 6(i) cha Sheria ya Baraza la Taifa la Elimu ya Ufundi ya mwaka 1997 Waziri wa Sayansi, Teknolojia na Elimu ya Juu amepewa mamlaka ya kutangaza katika Gazeti la Serikali Chuo chochote kilichopo kilichopata ithbati chini Baraza kuwa Chuo kinachojitegemea baada ya kushauriana na Baraza la Taifa la Elimu ya Ufundi kwa kuzingatia mambo mbalimbali muhimu kuhusu chuo hicho, na kwa kuwa Baraza limezingatia mambo yote muhimu ya chuo cha ufundi Mbeya ikiwa ni pamoja na uwezo wa utoaji elimu, kuthibiti viwango vya elimu, vifaa vya kufundishia watumishi na kadhalika. Kuthibitisha kuwa Chuo kinafaa kuwa chuo kinachojitegemea kiutendaji;

NA KWA KUWA kwa kuzingatia misingi hiyo, amri ya kukifanya Chuo cha Ufundi cha Mbeya kuwa Taasisi ya Sayansi na Teknolojia Mbeya imekwisha kutangazwa katika Gazeti la Serikali Namba 335 la Toleo la tarehe 10 Desemba, 2004 kwa madhumuni ya kujitegemea;

NA KWA KUWA kwa mujibu wa Sheria hii, Chuo hicho kinachotangazwa hakiwezi kuanza kutekeleza majukumu yake kama Chuo kinachojitegemea kabla ya kuridhiwa na Bunge;

KWA HIYO BASI kwa kuzingatia masharti ya kifungu cha 6(iii) cha Sheria ya Baraza la Taifa la Elimu ya Ufundi ya mwaka 1997, naomba sasa Mheshimiwa Spika, Bunge liridhie na kukubali kuwa Chuo cha Ufundi Mbeya kiwe chuo kinachojitegemea

na kupewa jina la Taasisi ya Sayansi na Teknolojia Mbeya *(The Mbeya Institute of Science and Technology - MIST)* ikiwa ni hatua ya awali ya kukifanya kuwa Chuo Kikuu cha Sayansi na Teknolojia Mbeya.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**WAZIRI WA ARDHI NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Mheshimiwa Spika, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*

**SPIKA:** Hoja hiyo ya kwanza ya Mheshimiwa Waziri imetolewa na imeungwa mkono. Sasa nampa nafasi atoe hoja ya pili.

**WAZIRI WA SAYANSI, TEKNOLOJIA NA ELIMU YA JUU:** Mheshimiwa Spika, sasa ninayo heshima kuleta mbele yako Azimio linalohusu Kuridhia Mkataba wa Kimataifa unaohusu Utunzaji na Ulinzi wa Vyanzo vya Nyuklia yaani *The Convention on the Physical Protection of Nuclear Material.*

Mheshimiwa Spika, itakumbukwa kwamba mnamo mwezi Novemba, 2004 Bunge lako Tukufu liliridhia Maazimio ya mikataba ifuatayo, Mkataba wa Kimataifa unaohusu azma ya kutokomeza au kutokuendeleza utengenezaji wa matumizi ya silaha ya nyuklia *(The Non-Proliferation of Nuclear Weapons Treaty - MPT),* Mkataba wa Kimataifa unaokusudia Kutumia Nishati ya Nyuklia kwa Shughuli za Amani tu yaani *Safeguard agreement,* Itifaki ya Nyongeza *(Additional Protocol)* ya Mkataba wa Kimataifa ya Usimamizi Madhubuti yaani *Safe guards agreement,* Mkataba unaohusu misaada ya kushughulikia ajali za nyuklia au dharura ya kiji-*redioloje convention on assistance on the case over nuclear extent of radiological emegency,* Mkataba wa Kimataifa unaohusu Utoaji Taarifa mapema Juu ya Ajali ya *Nuclear and the Convention on early notification of nuclear accident.*

Mheshimiwa Spika, mkataba ulio mbele yako unahusu utunzaji wa vyanzo vya nyuklia yaani *The Convention on the Physical Protection of Nuclear Material* ambao ni moja ya utaratibu mzima wa Kimataifa wa kuhakikisha matumizi salama ya amani ya teknolojia za nyuklia.

Mkataba wa Kimataifa unaohusu utunzaji wa ulinzi wa vyanzo vya nyuklia ulipitishwa na Baraza la Umoja wa Mataifa na kufunguliwa rasmi kwa ajili ya kutiwa saini tarehe 3 Machi,1980 katika miji ya New York, Marekani na Vienna, Austria.

Mkataba huu ulianza kutumika yaani *it entered into force* tarehe 8 Februari, 1987 yaani siku 30 baada ya kuhifadhi tamko la 21 la kuridhia Mkataba wa Shirika la Kimataifa ya nguvu za *Atomic* kulingana na Ibara ya 19(i) ya mkataba huo. Kupitishwa kwa mkataba huu ni mojawapo ya juhudi za Kimataifa katika kutambua umuhimu wa kuweka misingi imara ya ulinzi na uthibiti wa vyanzo vya nyuklia vinavyoweza

kutumiwa na watu wasiopenda amani katika utengenezaji wa silaha ya maangamizi ya nyuklia.

Kwa mfano, kutengeneza mabomu kama yale yaliyotumika kulipua Ofisi za Ubalozi Marekani na kwingineko. *Nuclear Material* ni vyanzo vya mionzi au mauzi na mifano yake ni *Uranium 233, uranium* inayokuwa na *isotops* zenye uzito tofauti 233 na 235 au zikiwa pamoja.

Mheshimiwa Spika, Tanzania inahusika na matumizi pamoja na usafirishaji wa vyanzo hivyo kutoka bandarini au uwanja wa ndege wa Kimataifa hadi sehemu inapotakiwa kutumika katika shughuli za utafiti kama vile kwenye Chuo Kikuu cha Dar es Salaam au pale hospitali ya *Ocean Road.* Tangu mkataba huu upitishwe jumla ya nchi 76 tayari zimeshatia saini mkataba huo.

Kati ya hizo nchi, 11 ni za Kiafrika. Mifano ya baadhi ya nchi za Kiafrika zilizokwisharidhia mkataba huu ni Kenya, Zimbabwe, Afrika Kusini, Niger, Ghana na Msumbiji. Tanzania bado haijasaini wala kuridhia mkataba huu. Chimbuko la mkataba huu limeelezwa katika ibara ya 18.2. Kwa vile Tanzania ni nchi mwanachama wa Umoja wa Mataifa na vile vile ni mwanachama wa Shirika la Kimataifa la Nguvu za Atomiki yaani *The International Atomic Energy Agency* inao wajibu wa kuridhia mkataba huu ili kulingana na nchi nyingine duniani katika kusimamia ulinzi, utunzaji na udhibiti, pamoja na usafirishaji wa vyanzo vya mionzi ya nyuklia.

Hivyo basi, ni vema nchi yetu ikubali kuridhia mkataba huu ili kuimarisha mfumo na mtandao wa kudhibiti usafirishaji wa vyanzo vya mionzi duniani kote.

Mheshimiwa Spika, kuna vipengele kama ifuatavyo katika mkataba huu, navyo ni ibara ya kwanza ambayo inatoa madhumuni ya mkataba huu pamoja na maana ya maneno na mifano husika. Kwa mfano, *nuclear material* maana yake ni vyanzo vya mionzi au mauzi na mifano yake kama nilivyosema *Uranium 233. Uranium* inakuwa *isotops* yenye uzito wa 233 na 235 zikiwa pamoja. Ibara ya pili inatoa maelezo kuhusu madhumuni yake. Mkataba huu unahusika na vyanzo vya mionzi ambavyo vitatumika kwa shughuli za amani wakati tukisafirishwa kutoka nchi moja hadi nyingine. Pia utatumika wakati vyanzo hivyo vikitumika ndani ya nchi husika mfano, vyuoni na hospitalini.

Uhifadhi wake na usafishaji wake, Ibara ya tatu, tano na sita zinatoa maelezo kuhusu hatua muhimu zinazopaswa kuchukuliwa na nchi wanachama katika kulinda usafirishaji wa vyanzo vya mionzi. Nchi husika kutotoa kibali kwa waagizaji cha kutoa au kuingiza ndani ya nchi vyanzo vya *nuclear* pasipo usimamizi madhubuti. Hii inaelezwa katika ibara ya 4.1.

Mheshimiwa Spika, nchi zinazotia saini mkataba huu hazipasi kuruhusu au kupitisha vyanzo vya mionzi kwa njia yoyote ile pasipo kibali maalum na kuthibitika kwamba vyanzo hivyo vitasimamiwa ipasavyo hasa kwa nchi zile ambazo hazijasaini mkataba huu. Inaelezwa katika ibara 4.3. Nchi itakayopokea kibali maalum *(assurances)*

kwamba vyanzo hivyo vitatunzwa vizuri itapaswavyo kutambua na kutoa taarifa kwa nchi zinazotarajia kupitisha vyanzo hivyo kwa njia yoyote ile yaani angani, majini au nchi kavu na kama ni bahari, bandari, gari vitaingilia au uwanja upi wa ndege utahusika.

Mheshimiwa Spika, kwa kupitia *Internatinal Agency of Atomic Energy,* mwanachama anatakiwa kukitambulisha chombo hicho kitakachohusika na utaratibu na utunzaji wa vyanzo vya nyuklia ili uporaji na matumizi mabaya ya vyanzo hivyo yasitokee. Pindi utakapokea wizi au ujambazi au uporaji au uchukuaji wa vyanzo wa mionzi kinyume cha Sheria nchi nyingine mwanachama kulingana na Sheria za kitaifa zitapaswa kutoa ushirikiano.

Ibara ya 7 inahusika na kila nchi mwanachama kuweka adhabu kali watakaobainika kufanya makosa ya makusudi kulingana na vifungu mbalimbali vya mkataba na uzito wa kosa lenyewe. Hatua muhimu za ushirikiano zimeelezwa katika ibara ya 11. Hatua muhimu za usuluhishi wa migogoro zimeelezwa katika ibara ya 17.

Mheshimiwa Spika, utaratibu wa kuridhia mkataba. Nchi inayotaka kuridhia mkataba huu haina budi kufuata utaratibu iliyojiwekea katika nchi yake Kikatiba. Utaratibu wa kuridhia mikataba Kimataifa hauna budi ufuatwe na Serikali kwa kupitia Wizara husika. Utaratibu wetu katika nchi yetu hoja itapelekwa Bungeni ili Bunge liweze kutoa tamko la kuridhia *ratification declaration* kulingana na Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ibara ya 63(e) na kuufanya mkataba huu kuwa sehemu ya sheria yake.

Tamko hili hupitishwa kisheria kwa kitu kinaitwa *ratification instrument* na hati ya ridhaa kuandaliwa na baadaye kupelekwa katika kile chombo cha Kimataifa kinachodhibiti matumizi ya atomiki ambaye ndiye mhifadhi wa nyaraka hizo ambaye anaitwa *The Depot Institution,* huo ndio utaratibu ambao unafuatwa. Baada ya maelezo hayo ninayo heshima Mheshimiwa Spika, sasa kulisoma mbele yako na kuliwasilisha Azimio la Kuridhia Mkataba huu.

KWA KUWA Mkataba wa Kimataifa unaohusu Utunzaji wa Ulinzi wa Vyanzo vya Nyuklia *(Convention on the Physical Protection of Nuclear Material)* ulipitishwa na Baraza la Umoja wa Mataifa tarehe 3 Machi, 1980;

KWA KUWA Mkataba huu ulisainiwa kwa mara ya kwanza mnamo tarehe 3 Machi, 1980 katika miji ya New York, Marekani na Vienna, Australia. Mkataba huu ulianza kutumika tarehe 8 Februari, 1987 yaani siku 30 baada ya kuhifadhi tamko la 21 la kuridhia mkataba kwa Mhifadhi Mkuu ambaye ni Mkurugenzi Mkuu wa Shirika la Kimataifa la Nguvu za Atomiki kulingana na ibara ya 19 kifungu kidogo la Mkataba huu;

KWA KUWA jumuiya ya Kimataifa inatilia mkazo suala la ulinzi na udhibiti wa vyanzo vya nyuklia vinavyoweza kutumiwa na watu wasiopenda amani katika utengenezaji wa silaha za maangamizi ya kinyuklia, kwa mfano utengenezaji mabomu ambayo hutumika kuleta maafa kwa wanadamu, na rasilimali za Kitaifa; hivyo basi, mkataba huu utazilazimisha nchi wanachama kutoruhusu vyanzo vya mionzi

kusafirishwa kwa njia yoyote ile kama vile angani, majini au nchi kavu bila kibali maalum;

KWA KUWA mkataba huu ni moja ya hatua muhimu katika kuungana na nchi nyingine duniani zenye kupenda amani kwa kusimamia ulinzi, utunzaji na udhibiti pamoja na usafirishaji wa vyanzo vya mionzi vya nyuklia hadi kufikia tarehe 7 Januari, 2005 nchi 10 zimekwisha kusaini na kuridhia mkataba huu;

KWA KUWA Tanzania bado haijasaini wala kuridhia mkataba huu, hivyo ni muhimu kuitaka Serikali ya Tanzania iungane na nchi nyingine duniani zenye kupenda amani kwa kuridhia mkataba huu. Mifano ya nchi hizi za Kiafrika zilizokwisha ridhia mkataba ni Afrika Kusini, Botswana, Ghana, Kenya, Mali, Morocco, Msumbiji, Namibia, Niger, Sudan na Tunisia;

KWA KUWA ibara ya kwanza na ya pili za mkataba zinaeleza madhumuni yake mkataba huu unahusika na vyanzo vya mionzi ambavyo vitatumika kwa shughuli za amani wakati wa kusafirishwa kutoka nchi moja hadi nyingine, siyo utatumika kwa wakati vyanzo vya mionzi au mauzi na mifano yake yaani *uranium* inayokuwa *isotops* yenye uzito wa 233 na 235 zikiwa pamoja zikitumika ndani ya nchi husika uhifadhi na usafirishaji wake;

KWA KUWA Ibara za 3, 4, 5 na 6 za mkataba huu zinatoa maelezo kuhusu hatua muhimu zinazopaswa kufuatwa na nchi wanachama katika kulinda usafirishaji wa vyanzo vya mionzi, hatua hizo ni pamoja na nchi wanachama haziruhusiwi kutoa kibali kwa waagizaji kutoa/kuingiza vyanzo vya *nuclear* pasipo usimamizi madhubuti. Nchi zilizotia saini hazipaswi kuruhusu au kupitisha vyanzo vya mionzi kwa njia yoyote ile pasipo na kibali maalum na kuthibitisha kwamba vyanzo hivyo vitasimamiwa kwa utunzaji hasa kwa nchi zile ambazo zina wanachama. Na nchi itakayopata kibali cha maalum cha utunzaji wa vyanzo vya mionzi, itapaswa kutoa taarifa kwa Shirika la Kimataifa la nguvu za *atomic* kuhusu nchi zinazotarajiwa kupitisha vyanzo hivyo kwa njia ya anga, majini au nchi kavu katika nchi hiyo;

KWA KUWA nchi wanachama zitapaswa kutoa ushirikiano pindi wizi au ujambazi uchukuaji wa vyanzo vya mionzi kwa nchi nyingine ambazo siyo mwanachama;

KWA KUWA Ibara ya 7 ya mkataba huu inaelezea umuhimu wa nchi mwanachama kuweka adhabu kali kwa nchi inayobainika kufanya makosa ya makusudi kulingana na vifungu mbalimbali vya mkataba na uzito wa kosa hilo adhabu itatolewa kulingana na kosa;

KWA KUWA Ibara ya 11 na 17 za mkataba huu, zinaelezea hatua muhimu za ushirikiano wa kufanya usuluhishi wa mgogoro nchi wanachama zinapaswa kuzingatia maelezo husika;

KWA KUWA hakuna mahitaji yoyote ya fedha zaidi ya michango ya kawaida ya kila mwaka ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa Shirika la Nguvu za Atomiki, nchi haitakuwa na gharama za ziada;

NA KWA KUWA kuridhia mkataba huu kutaiwezesha Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kushirikiana na Jumuiya ya Kimataifa katika utunzaji na usimamizi wa usafirishaji wa vyanzo vya mionzi *(nuclear)* kutoka sehemu moja hadi nyingine ili kudumisha usalama na imani duniani;

KWA HIYO BASI, kwa kuzingatia wanachama wa Tanzania katika Shirika la Nguvu za Atomiki duniani na umuhimu wa manufaa ya mkataba huu kwa Tanzania, Bunge hili katika Mkutano wake wa Kumi na Tisa na kwa mujibu wa Ibara 63 kifungu kidogo cha (3)(a) cha Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania cha mwaka 1979, sasa Bunge lako Tukufu linaanzimia kuridhia wa Mkataba wa Kimataifa unaohusu Utunzaji na Ulinzi wa Vyanzo vya Nyuklia yaani *The Convention on the Physical Protection of Nuclear Material.*

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**WAZIRI WA ELIMU NA UTAMADUNI:** Mheshimiwa Spika, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, hoja ya pili ya Mheshimiwa Waziri imetolewa na imeungwa mkono. Kwa hiyo, kabla sijamwita msemaji wa Kamati niwajulishe waliojiandikisha kusema ili wajiandae wako sita. Nao ni Mheshimiwa Eliachim Simpasa, Mheshimiwa Professa David Mwakyusa, Mheshimiwa Jackson Makwetta, Mheshimiwa Benson Mpesya, Mheshimiwa Dr Willliam Shija na Mheshimiwa Omar Mjaka Ali.

Baada ya hapo nadhani Mheshimiwa ataombwa kuhitimisha hoja yake. Sasa namwita Mheshimiwa Dr Haji Mwita Haji ambaye nimearifiwa ndiye atakayewasilisha maoni ya Kamati ya Huduma za Jamii. *(Makofi)*

**MHE. DR HAJI MWITA HAJI (k.n.y MWENYEKITI WA KAMATI YA HUDUMA ZA JAMII):** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa fursa hii ili niweze kuwasilisha maoni ya Kamati ya Bunge ya Huduma za Jamii kuhusu Azimio la Bunge Kuridhia Chuo cha Ufundi Mbeya kuwa Taasisi ya Sayansi na Teknolojia inayojitegemea. Kamati yangu imetembelea Chuo cha Ufundi Mbeya mwezi Aprili, 2004 na kuona miundombinu ya Chuo hiki ikiwa ni pamoja na vyumba vya madarasa, mihadhara, karakana za ufundi na umeme na mitambo pamoja na mabweni.

Aidha, Kamati ilielezwa kuwa uongozi wa chuo ukisaidiwa na Wizara ulikuwa unaendelea kuboresha miundombinu ya chuo hicho ambacho ujenzi wake ulikuwa unafadhiliwa na iliyokuwa Serikali ya Muungano wa nchi za Kisoviet, *USSR* kwa lengo

la kuwa na chuo cha kisasa cha ufundi. Kamati inatoa pongezi kwa Serikali na uongozi wa chuo kwa kukarabati na kuboresha majengo ya chuo hicho.

Aidha, Kamati inakipongeza chuo kwa kutunza mazingira vizuri, kutengeneza samani za chuo na kutenga maeneo maalum kama hatua muhimu sana ya usalama katika mabweni ya wanafunzi kwa ajili ya huduma mbalimbali kama kupiga pasi, kuchemsha maji, chai, kahawa, kupumzika, kusikiliza redio na kuangalia luninga. *(Makofi)*

Mpaka sasa chuo hiki kimepata ardhi ya kutosha kiasi cha hekta 1000 ambayo inatoa nafasi ya kupanua miundombinu yake hata kitakapofikia hatua ya kuwa Chuo Kikuu cha Sayansi na Teknolojia bado kitakuwa na nafasi ya kutosha kwa shughuli mbalimbali za kitaalam na utafiti. Baada ya Kamati kuona hali halisi ya Chuo cha Ufundi Mbeya, inaipongeza Serikali kwa kuleta Azimio hili na kukiongezea ardhi chuo hiki. Kwa kuwa mazingira na miundombinu iliyopo ipo tayari kupokea haya mabadiliko. Umuhimu wa kuendeleza na kuimarisha masuala yanayohusu sayansi na teknolojia hapa nchini unaonyesha kuwa uamuzi wa Serikali ni wa busara. *(Makofi)*

Aidha, katika zama hizi za utandawazi, masuala ya sayansi na teknolojia hayana budi kupewa kipaumbele kwa kuanzisha Taasisi za Sayansi na Teknolojia na kuimarisha taasisi zilizopo kwa lengo la kuwapatia Watanzania maarifa na uwezo wa kutumia nyenzo zinazoendana na mabadiliko ya sayansi na teknolojia.

Mheshimiwa Spika, Azimio hili litakiwezesha chuo hiki kujitegemea kwa mujibu wa sera za ufundi sayansi na teknolojia. Kitakuwa na uwezo wa kubuni na kutoa maamuzi ya namna ya kutekeleza mipango yake ya maendeleo kwa madhumuni ya kuboresha viwango na ubora wa *course* na elimu itolewayo. Aidha, Azimio hili litawezesha chuo kutoa wataalam ambao ni wanasayansi na wanateknolojia wenye mwelekeo wa vitendo zaidi kuliko nadharia na wenye kukubalika katika soko la ajira na mfumo wa sasa wa utandawazi.

Mheshimiwa Spika, Azimio la kukifanya chuo hiki kuwa Taasisi ya Sayansi na Teknolojia, iwe ni ngazi ya kukifikisha kuwa Chuo Kikuu cha Sayansi na Teknolojia ambacho kitajenga na kuimarisha uwezo wa kutoa taaluma, ushauri na kufanya utafiti katika nyanja za sayansi na teknolojia pamoja na kuimarisha na kuongeza miundombinu.

Katika sehemu ya tatu ya Azimio hili Ibara ya 7 Kamati inashauri kuwe na bodi ya utawala yaani *Governing Board* badala ya Baraza au *Council,* kama ilivyo kwenye Taasisi zingine zenye hadhi kama hii.

Mheshimiwa Spika, vile vile Ibara ya 8(2) iboreshwe ili Waziri alazimike kisheria kuteua Wajumbe wa Baraza kwa kuzingatia usawa wa kijinsia. Kwa kuwa chuo hiki kinapandishwa hadhi, Serikali ifanye juhudi za makusudi kuboresha miundombinu ikiwemo barabara inayoelekea chuoni kutoka barabara kuu na kutoa Hatimiliki ya ardhi inayomilikiwa na chuo hiki. Vile vile Kamati yangu inashauri chuo kiwe na mipango kabambe ya kuendeleza na kutumia kikamilifu ardhi yake kama ambavyo Vyuo Vikuu

vya Dar es Salaam na Chuo Kikuu cha Kilimo cha Sokoine *(SUA)* walivyokuwa na mipango kabambe ya kutumia ardhi yao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Serikali ifanye maandalizi ya kutosha kutekeleza azma yake kwa Chuo kupata wataalam wenye sifa za kufundisha na kuzingatia mahitaji ya wataalam katika soko la ajira yanayobadilika kufuatana na mabadiliko yanayoendelea katika nyanja za sayansi na teknolojia.*(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mwisho napenda kumpongeza Mheshimiwa Balozi Dr Pius Ng'wandu, Mheshimiwa Naibu Waziri, Katibu Mkuu wa Sayansi, Teknolojia na Elimu ya Juu, pamoja na maafisa wa Wizara hiyo kwa kuwasilisha mbele ya Kamati yetu Azimio hili kwa ufanisi mkubwa.

Aidha, nawapongeza Waheshimiwa Wajumbe wa Kamati ya Huduma za Jamii, kwa kulitafakari Azimio hili kwa kina na umakini mkubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo haya, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, haya yalikuwa ni maoni ya Kamati kuhusu Chuo cha Mbeya. Sasa maoni ya Kamati kuhusu Mkataba wa *Nuclear* namwita Mheshimiwa Dr Aisha Kigoda, awasilishe maoni hayo. *(Makofi)*

**MHE. DR AISHA O. KIGODA ( k.n.y . MWENYEKITI WA KAMATI YA HUDUMA ZA JAMII):** Maoni ya Kamati ya Bunge ya Huduma za Jamii kuhusu Azimio la Bunge na Kuridhia mkataba wa Kimataifa unaohusu Utunzaji na Ulinzi wa Vyanzo vya Nyuklia.

Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa fursa hii ili niweze kuwasilisha maoni ya Kamati ya Bunge la Huduma za Jamii kuhusu Azimio la Bunge la Kuridhia Mkataba Kimataifa unaohusu Utunzaji na Ulinzi wa Vyanzo vya Nyuklia *(The convention on the Physical Protection on Nuclear Material).*

Mheshimiwa Spika, Tanzania ni nchi ambayo imekuwa na historia ya kuwa nchi ya amani tangu kupata uhuru wake. Amani hii imejengeka kwa muda mrefu kutokana na uongozi thabiti wa waasisi wa Taifa hili. Kwa kujua umuhimu wa amani, waliimarisha umoja wa Kitaifa kwa kuondoa mambo yote ambayo yanaweza kuhatarisha umoja wa Watanzania na hatimaye kuhatarisha amani nchini.

Mambo yaliyoondolewa ni pamoja na udini, ujimbo, uchifu, ubaguzi ya rangi na matabaka mbalimbali yaliyokuwepo wakati wa ukoloni na aidha, lugha ya Kiswahili imeendelea kuwa mhimili wa umoja wetu. Katika kuimarisha amani, Serikali ya Tanzania ilitunga sheria mbalimbali ili kudhibiti umilikaji wa aina zote za silaha ikiwemo bunduki, bastola, mabomu na aina zote za milipuko. Aidha, vyanzo vyote vya mionzi ya *nuclear* vimekuwa vikidhibitiwa kwa sheria mbalimbali kwa minajili ya kuimarisha amani na usalama wa raia wa nchi hii.

Mheshimiwa Spika, katika zama hizi za utandawazi na kupanuka na sayansi na teknolojia ni muhimu sana kushirikiana na Mataifa mengine duniani ili kudhibiti masuala mbalimbali yanayoweza kutishia amani ikiwemo udhibiti wa silaha za aina zote ikiwemo vyanzo vyote vya *nuclear.* Katika ulimwengu wa sasa unaotishiwa na masuala ya ugaidi, vyanzo vya *nuclear* vinaweza kutumiwa na watu wasiopenda amani katika utengenezaji wa silaha ya maangamizi ya ki-*nuclear.*

Mheshimiwa Spika, ni vema Tanzania ikaungana na nchi nyingine zenye kupenda amani kwa kusimamia ulinzi, udhibiti pamoja na usafirishaji wa vyanzo vya mionzi ya *nuclear.* Mkataba huu ndio utakaoiwezesha nchi yetu kushiriki katika suala hili muhimu la kulinda amani duniani. Katika kushiriki ulinzi wa amani duniani, Tanzania imetia saini na kuridhia mikataba kadhaa inayohusu masuala ya *nuclear* duniani ikiwemo Azimio la Kuridhia Mkataba wa Kimataifa wa Udhibiti wa Majaribio ya Silaha za *Nuclear,* Azimio la Kuridhia Itifaki ya Kimataifa Kuhusu Ufunguzi wa Kituo cha Kupima na Kufuatilia mionzi ya aionisha katika mazingira chini ya Tume ya Kimataifa ya Udhibiti wa Majaribio ya Silaha za *nuclear,* Azimio la Kuridhia Mkataba wa Kimataifa unaohusu Azma ya Kutokomeza au Kutoendeleza Utengenezaji wa Matumizi ya Silaha za *Nuclear.*

Azimio la Mkataba wa Kimataifa unaokusudia kutumia nishati ya *Nuclear* kwa shughuli za amani tu na siyo kwa kutengeneza silaha za *nuclear,* Azimio la Kuridhia Mkataba unaohusu Itifaki ya Nyongeza ya Mkataba wa Kimataifa wa Usimamizi Madhubuti wa *Nuclear,* Azimio la Kuridhia Mkataba wa Kimataifa unaohusu Utoaji wa Taarifa mapema juu ya ajali za *nuclear* na Azimio la Kuridhia Mkataba wa Kimataifa unaohusu misaada ya kushughulikia ajali ya *nuclear* au dharura ya kiradiolojia.

Mheshimiwa Spika, kuridhiwa kwa mikataba michache niliyoitaja ni ushahidi tosha kuwa Tanzania imedhamiria kudumisha amani na umoja nchini na kote ulimwengu. Hivyo kuridhia mkataba huu nchi yetu itapata manufaa mengi ikiwemo kushirikiana na nchi nyingine katika utunzaji na ulinzi wa vyanzo vya *nuclear.*

Tanzania inatarajia kupata misaada mbalimbali katika usimamizi, ulinzi utafiti na utabibu wa kutumia mionzi. Aidha, hakuna mahitaji yoyote ya kifedha ambayo nchi yetu italazimika kugharamia kwa kuingia katika mkataba huu.

Mheshimiwa Spika, pamoja na maelezo haya tunaishauri Serikali ichukue tahadhari ili mkataba usije ukaizuia nchi yetu kutumia raslimali yake hasa madini ya *uranium* yaliyopo nchini kwa kuwa ndio chanzo kuu cha nishati ya *nuclear.*

Pili, vile vile tunaishauri Serikali iendelee kufanya utafiti kufahamu kwa undani kama kuna baadhi ya nchi zinasita kuridhia na sababu za kusita huko ili kujua zaidi juu ya faida au athari na hasara zinazoweza kujitokeza kufuatia mkataba huu.

Mheshimiwa Spika baada ya Kamati yangu kuunga mkono Azimio hili, napenda kumpongeza Mheshimiwa Dr Pius Ng'wandu, Mbunge na Waziri wa Sayansi, Teknolojia na Elimu ya Juu, Naibu Waziri Mheshimiwa Zabein Mhita, Katibu Mkuu pamoja na

maafisa wa Wizara hiyo kwa kuwasilisha mbele ya Kamati Azimio hili kwa ufanisi mkubwa. Pia nawapongeza Waheshimiwa Wabunge wa Kamati ya Huduma za Jamii kwa kulitafakari Azimio hili kwa kina na umakini mkubwa.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo haya naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, kabla hatujaendelea, napenda kuchukua nafasi hii kutambulisha *delegation* ya wageni wa Kimataifa wamewasili Dar es Salaam asubuhi hii wakitokea Ulaya na wameendelea na safari yao kuja Dodoma kututembelea hapa Bungeni.

Sasa nitamwomba Afisa wetu anayefuatana nao awaambie wasimame nitakapowatambulisha. Hawa ni Waheshimiwa Wabunge kutoka Bunge la Finland kule Ulaya, tunawakaribisha Bungeni na katika nchi yetu ya Tanzania. *(Makofi)*

Sasa Mheshimiwa Papa Benedicto aah! Mheshimiwa Benedicto Mutungirehi, Msemaji wa Kambi ya Upinzani sijui nafasi iliyobaki inakutosha au utawasilisha mchana. Kwa Azimio moja inatosha, sasa namwita Mheshimiwa ili awasilishe maoni ya Kambi ya Upinzani kuhusu Chuo cha Mbeya. *(Kicheko/Makofi)*

**MHE. BENEDICTO M. MUTUNGIREHI - MSEMAJI WA UPINZANI KWA WIZARA YA SAYANSI TEKNOLOJIA NA ELIMU YA JUU:** Mheshimiwa Spika, kabla sijaendelea niwapongeze na kuwatakia kila la kheri wakristo wenzangu kwa kupata Papa mpya ambaye anaitwa Benedicto. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii ili niweze kutoa maoni ya Kambi ya Upinzani Bungeni kuhusu Azimio la Bunge la Kuridhia Chuo cha Ufundi Mbeya kubadilishwa kuwa Taasisi ya Sayansi na Teknolojia inayojitegemea.

Mheshimiwa Spika, tangu kuanzishwa kwa Chuo cha Ufundi Mbeya kumekuwepo na miito mbalimbali iliyotolewa na watu mbalimbali kuhusu kukifanya Chuo cha Ufundi Mbeya kuwa Chuo Kikuu cha Sayansi na Teknolojia. Wito wa kwanza ulitolewa na Hayati Baba wa Taifa Mwalimu Julius Kambarage Nyerere, pia kwa nyakati tofauti tofauti Wabunge wamekuwa wakiiomba Serikali kuharakisha Chuo cha Ufundi Mbeya kuwa Chuo Kikuu cha Sayansi na Teknolojia.

Mheshimiwa Spika, kambi ya Upinzani inaelewa kuwa si jambo rahisi mno kuanzisha Chuo cha Sayansi na Teknolojia kwa haraka bila kuanza kuweka msingi katika miundombinu, vifaa, majengo, wataalam na mitaala bora ili kutoa ujuzi na utaalamu unaotarajiwa katika chuo hicho. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kama alivyoeleza Mheshimiwa Waziri wa Sayansi, Teknolojia na Elimu ya Juu leo hii asubuhi kuwa wataalam waelekezaji walipendekeza kwamba ili Chuo cha Ufundi Mbeya kiweze kigeuzwa Chuo Kikuu cha Sayansi na Teknolojia, ni vema kwanza kikawa Taasisi ya Sayansi na Teknolojia inayojitegemea ili

kiweze kujenga uwezo wa ufundishaji. Kuimarisha na kuongeza miundombinu na pia uongozi wa chuo.

Mheshimiwa Spika, Kambi ya Upinzani inaunga mkono ushauri huu wa wataalam waelekezaji na uamuzi wa Waziri wa Sayansi, Teknolojia na Elimu ya Juu kukubali na kuleta Azimio hili hapa. Kabla ya kutoa mapendekezo ya jumla kutoka Kambi ya Upinzani Bungeni, kwanza ninaomba nitoe maoni yafuatayo katika sehemu za amri au *order* ya mwaka 2004 ya kuanzisha Taasisi ya Sayansi na Teknolojia Mbeya *(The Mbeya Institute of Science and Technology). (Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naelewa utaratibu kuhusu *subsidiary registration,* lakini si vibaya na wala siyo msahafu kwamba hatuwezi tukazungumzia kile kilichomo ndani ya *registration* hiyo na baadaye tutaendelea na Azimio lenyewe.

Mheshimiwa Spika, tunapendeza kuwa katika sehemu ya kwanza ya amri yenyewe kuna maneno pale ya tafsiri kuhusu neno *Council* ambayo inasema *Council means the Council of the Institute establish under section paragraph seven.* Tunaomba neno *Council* lifutwe mpaka hapo tutakapofanya marekebisho huko baadaye tutapokwenda siyo hapa Bungeni. Angaweza kuweka pale maneno *Governing Board* na bahati nzuri imependekezwa vile vile kama Kamati ya Huduma za Jamii. Sambamba na kufutwa neno hilo *Council* katika sehemu hiyo ya tafsiri neno hilo hilo lifutwe katika kila linapojitokeza katika amri husika.

Mheshimiwa Spika, na vivyo hivyo maneno *Governing Board* yawekwe katika kila eneo yalipofutwa neno *Council.* Tunapendekeza hivyo kwa sababu mbili:-

(1) Hadhi yenyewe ya Taasisi inayoanzishwa na pia kwamba Wajumbe wa Taasisi hiyo ni wachache mno wala hawazidi hata kumi.

(2) Mheshimiwa Spika, katika sehemu ya pili, ibara ya 5(2)(c) katika ile *subsidiary decision* anasema kwamba *faculty of management,* tunapendekeza kifutwe vile vile. Tunapendekeza katika Ibara ya 5(3)(g) kinachosomeka *General studies,* (l) kinachosomeka *Business Studies and Management,* (n) kinachosomeka *Human resources Management,* vifutwe.

Mheshimiwa Spika, mapendekezo ya kufuta vipengele vyote hivyo katika Ibara ya 5(2)(c) na Ibara ya 5(3)(a) na Ibara ya 2(n) yanatolewa kwa sababu zifuatazo:-

(1) Kutokana na sababu na madhumuni ya kuanzishwa kwa Taasisi ya Sayansi na Teknolojia.

(2) Hali halisi ya Taasisi ya Elimu ya Juu katika nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, chuo tunachokibadilisha kinaitwa *Mbeya Technical College* na neno *College* limeelezwa katika lugha ya kiingereza kama ifuatavyo, *College is a society of scholars incorporated within or in connection with a university or other ways*

*formed for the purpose of study and his instruction.* Kutokana na maana hiyo, Chuo cha Ufundi Mbeya kilianzishwa kwa madhumuni ya kutoa elimu na mafunzo ya ufundi. Hivi sasa katika amri inayoonyesha Taasisi ya Sayansi na Teknolojia Mbeya yaani *Mbeya Institute for Science and Technology* badala ya neno *College* limetumika neno *Institute.*

Mheshimiwa Spika, neno *Institute* limeelezwa kwa kiingereza kuwa; *Institute is a society or an organisation instituted to promote literature, science, art, education or the like one of them.* Katika tofauti ya *College* au chuo na *Institute* kwa maana ya Taasisi ni dhahiri kuwa Taasisi lengo kuu lake ni kukuza ujuzi na maarifa maalum. Wakati katika *College* ni kujifunza elimu kwa ujumla.

Mheshimiwa Spika, tunataka Taasisi ya Sayansi na Teknolojia Mbeya ishughulikie sayansi asilia *(Natural Science)* na teknolojia tu na wala siyo kuchanganya na mafunzo ya sayansi za jamii. Katika karne hii ya sayansi na teknolojia, matumizi ya sayansi asilia yanahitajika sana katika nchi yetu na ndio maana tukasema kutokana na hali halisi ya nchi yetu kuna vyuo vingi vya elimu ya juu ambamo masomo ya sayansi za jamii yanatolewa.

Kwa mfano, Chuo Kikuu cha Mzumbe, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam na tumeanzisha na Chuo cha Kumbukumbu Mwalimu Nyerere. Hivyo tunadhani vyuo vilivyopo kwa sayansi ya jamii, kwa sasa vinamudu kazi hiyo japokuwa hatusemi vinatosha.

Mtaalam mmoja wa masuala ya *methods of social science research* aliwahi kusema; eleza *I doubt the scientific of our social science subject I hold the scientific of the natural science subject.* Kwa mtazamo huu, tunaomba Taasisi iimarishwe ili kushughulikia masuala ya kisayansi na teknolojia tu.

Tumeeleza hayo maelezo yote kwa sababu katika ile sheria anayoiweka, anaweka kuanzisha vitengo ambavyo vitahusu masuala ya sayansi za jamii. Katika Ibara ya 29(2), amri ya kuanzisha Taasisi ya Sayansi Mbeya imetoa maelezo mafupi au ya jumla kuhusu jinsi ya kushughulikia mafao na hatima ya wafanyakazi wa kilichokuwa Chuo Kikuu cha Ufundi Mbeya. Tunamwomba Mheshimiwa Waziri alihakikishie Bunge kuwa katika Kanuni na maelekezo atakayoyatoa kwa uongozi wa Taasisi ya Sayansi na Teknolojia Mbeya, yazingatia maoni yafuatayo:-

(a) Kipaumbele kiwe katika kuwaendeleza kitaaluma wafanyakazi waliyopo katika Chuo cha Ufundi Mbeya ili waweze kuendelea na ajira zao katika Taasisi mpya.

(b) Katika kuajri wafanyakazi wa Taasisi mpya, wafanyakazi wa chuo kinachobadilishwa wapewe uwezo wa kuamua kuacha au kuendelea na ajira kwa masharti watayokubaliana na mwajiri wao.

Mheshimiwa Spika, Kambi ya Upinzani inayo mapendekezo kuwa ili Taasisi inayoanzishwa iweze kufanya kazi zake za utafiti katika Sayansi na teknolojia, lazima ipewe fedha za kutosha na siyo kutelekezwa kama ilivyo kwa sasa na uzoefu mbaya au

mzuri uliopatikana katika Taasisi ya Teknolojia Dar es Salaam *(The Dar es Salaam Institute of Technology)* utumike katika kutafuta njia sahihi za kuendeleza Taasisi ya Sayansi na Teknolojia Mbeya.

Mheshimiwa Spika, tunasema hivyo kwa sababu katika Taasisi inayoshughulikia teknolojia, tungetegemea kukuta miundombinu na vifaa vya kisasa. Lakini kinyume chake mfano, katika Taasisi ya Teknolojia Dar es Salaam, mitambo mingi iliyopo ni ile iliyoachwa na Wajerumani mwaka 1918. Hivyo hivyo hata kwenye Chuo cha Ufundi Mbeya, vifaa vingi vilivyopo ni vile walivyoviacha Warusi wa Russia ya Kisoviet.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha na ninaunga mkono hoja. *(Makofi)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, mpaka hapo ndio tumefikia mwisho wa kipindi cha asubuhi. Nilishasoma watakaochangia hoja hizi mbili kipindi cha mchana kwa sababu bado tunalo Azimio lingine linahitaji kuridhiwa na naona orodha hii imefungwa sasa.

Waheshimiwa Wabunge, hao sita ndio watakaochangia halafu tutamwita mtoa hoja ahitimishe hoja yake ili tuweze kuendelea na lile Azimio lingine la Wizara ya Nishati na Madini.

Baada ya maelezo hayo, sasa nasitisha shughuli za Bunge hadi saa kumi na moja jioni.

*(Saa 06.57 mchana Bunge lilifungwa mpaka saa 11.00 jioni)*

*(Saa 11:00 jioni Bunge lilirudia)*

*Hapa Naibu Spika (Mhe. Juma J. Akukweti) Alikalia Kiti*

**NAIBU SPIKA:** Sasa namwita Msemaji wa Kambi ya Upinzani wa hoja hii. Hayupo, basi kama hayupo namwita mchangiaji wetu wa kwanza Mheshimiwa Eliachim Simpasa, simwoni; Mheshimiwa Prof. David Mwakyusa, simwoni; Mheshimiwa Jackson Makwetta. *(Makofi)*

**MHE. JACKSON M. MAKWETTA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa nakushukuru kwa kunipatia nafasi hii ili niweze kuchangia katika kupitisha ruksa ya kuendelea kwa Taasisi hii mpya ya Mbeya. Lakini kabla ya yote ningependa kutoa ushauri.

Katika taaluma na utaalam wa kisasa kuna uwiano kati ya wataalam wa ngazi za juu, wale wanaomaliza katika Vyuo Vikuu na kupata shahada au *degree* na wale ma-*technician* wa katikati wanaotoka kwenye *Colleges* na wale Mafundi Mchundo wanaotoka kwenye Vyuo kama vya *VETA* na uwiano huu ni mtaalam mmoja kwa wataalam wa katikati watano na kwa watano kwa uhusiano wa Mafundi Mchundo 45. Sasa huu mwelekeo wetu wa kujaribu kuchukua Vyuo tulivyonavyo unaua utaratibu huu

wa *one to five to forty five*. Kwa sababu, kwa mfano chuo cha Dar es Salaam, Chuo cha Ufundi hivi sasa kina hadhi ya Chuo Kikuu, Mzumbe ni Chuo Kikuu, na sasa Mbeya kitakuwa na hadhi ya Chuo Kikuu na baadaye tutachukua Arusha na Vyuo vingine vyote vitakwisha hapa katikati.

Kwa hiyo tutakuwa na Vyuo Vikuu na tunakwenda chini kwenye Vyuo vya Ufundi Mchundo. Tunavuruga hii *pyramid* na uwiano huu katika nchi yetu. Napendekeza kwamba kuwe na utaratibu, basi pamoja na hatua hizi kuwa na utaratibu wa kujenga Vyuo vingine na mwelekeo wa dunia au wananchi hii ni kwamba Wahisani wengi hawajengi hivi Vyuo vya Ufundi kwa sababu ya gharama kubwa. Wako tayari kutujengea Sekondari kwa sababu zile ni rahisi kidogo.

Lakini hakuna Vyuo vya kati ukiacha Vyuo Vikuu, hakuna Vyuo vya kati vipya vinavyojengwa. Ukiangalia vyote vilijengwa wakati wa ukoloni, Arusha, *Dar es Salaam Technical*, labda hiki cha Mbeya tu ambacho sasa tunataka tukibatize kiwe Chuo cha ngazi ya juu kidogo. Mimi naunga mkono pendekezo hili. Ninachosema ni kwamba, katika kuendeleza Chuo hiki, ni vizuri tukaheshimu na tukajaribu kuwa na *both* upande wa ngazi za juu ya shahada na upande huu wa mafundi wa kati ili ku-*maintain* huu uwiano wa moja kwa tano kwa arobaini na tano. Ama sivyo, tutavunja hii *pyramid,* tutakuwa na watu wa ngazi za juu bila ya hao mafundi wa katikati ambao ndio wanaosimamia wale Mafundi Mchundo.

Tujaribu kuangalia huu mwelekeo wa *degree,* yaani sasa Vyuo *Moshi Comparative Colleg*e, Mweka, Mzumbe, Mbeya, Dar es Saalam *Technical* vyote vinapelekwa kwenye *degree*. Hapa katikati kuwe na makakati maana upande wa Sekondari kuna mkakati wa *MMESS*, upande wa *Primary* kuna mkakati ule *MMEM*. Lakini Hili eneo la Elimu ya Ufundi, hakuna. Tungeomba kuwa na mkakati wa namna hiyo kwa sababu tunaweza kuwa na Watanzania wote wenye *degree* hizi za jumla jumla, lakini bila Elimu ya Ufundi hatuwezi kwenda popote pale.

Kwa hiyo nilikuwa napendekeza Serikali kwa makusudi iwe na mkakati wa kujenga Vyuo hivi vya Ufundi wa kati kwa sababu upande wa Sekondari hata wananchi wanaweza. Lakini upande wa Vyuo vya Ufundi ni mgumu sana, ni lazima Serikali ijiingize katika eneo hili. Nilikuwa napendekeza Wizara hii inayohusika kwa kweli iwe na mkakati huo, iombe Wahisani Benki ya Dunia kusudi tuwe na utaalam kwa sababu bila utaalam hatuwezi tukafika popote pale.

Pia nilikuwa napendekeza ukurasa wa tano pale ilipopendekezwa kwamba Wajumbe wa Bodi, wengine wanasema Bodi au *Council;* nilikuwa napendekeza Mbunge wa eneo lile ambako Chuo kinatoka au kimependekezwa awe ni *member* wa ile Bodi hii. Mwelekeo wa kujaribu kuwakwepa Wabunge kila mahali, mimi sioni sababu. Matatizo ya Mbeya yatamhusu ndugu yetu Mbunge wa eneo lile na lazima aende apale akasikilize, lakini hakuna Mbunge katika Bodi! Naomba kwa makusudi tupendekeze kwamba Mbunge wa eneo lile awe ni *member* wa Bodi ya Chuo kile, kusudi aweze kujua matatizo ya mahali pale na vile vile iwe kwa Vyuo vyote nchini.

Nilikuwa nashangaa kwa nini Chuo cha Uyole pale hakikutazamwa, kwa sababu ni Chuo kilicho jirani na hiki Chuo tunachokizungumza hapa. Kwa nini visiungane na kufanya hiki Chuo kiwe kimoja, kwani pale ni mabingwa wa mambo ya kilimo na wangeweza wakaingiza kitu kinaitwa *biotech* ambayo nayo ni sayansi na kuondoa yale mawazo mengine yaliyo ya Menejimenti za kawaida kama walivyopendekeza wenzetu.

Mimi katika hili naunga mkono pendekezo la Msemaji Mkuu wa Upinzani waziwazi kwamba mambo haya ya Menejiment na mambo ya makanda kanda haya yaachwe Mzumbe na kwingine. Hapa iwe *Pure Technology Science* yaani sayansi asilia badala ya kuingiza na haya mambo mengine ambayo tayari kuna Vyuo vyake.

Kwa hiyo nilikuwa nauliza, kwanini katika hamkuona umuhimu wa kuingiza Uyole? Nilidokeza nikamwuliza Waziri muhusika, tunaomba radhi hatukuliaona hilo mapema. Sio huyo wa Kilimo, nikasema kwa nini hukuingiza Uyole iwe pamoja na Chuo hiki? Akasema, hatukuliona, lakini tunalifanyia kazi. Natumaini watalifanyia kazi ili somo hili mafunzo ya biotech yaingizwe katika sayansi na teknolojia na hakuna ugumu wakawa chini ya mwavuli mmoja.

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine ni suala la ardhi na nalijua hili kwa sababu nimehusika nikiwa Waziri katika eneo hili, lakini naomba kwa makusudi Wizara na Serikali ilipie zile eka 1000 zilizosemwa hapa. Maana mpaka sasa ambazo mmelipia ni hekta 400, lakini zile nyingine bado hamjalipia, kama mmelipia nitashukuru. Lakini hofu yangu ni kwamba wananchi wa eneo lile kila mwaka wanapanda miti kwa wingi na kusababisha gharama kuzidi kuwa kubwa zaidi. Wamepanda miti mingi na inakuwa kila eneo tunajaribu utaalam, kwa hiyo inajaa miti na unatakiwa ulipie kila mti. Kwa hiyo, nashauri Wizara husika itafute pesa ya kuweza kununua eneo lote kwa mara moja kusudi mgogoro usiendelee. Vinginevyo, fedha nyingi zinaishia kuwalipia fidia watu ambao wanazidi kuwa wajanja kupita hata sisi wenyewe.

La mwisho naomba Wizara pamoja na nia nzuri ya kukibatiza Chuo hiki, kwa kweli vile vifaa mle ndani bado havirizishi. Ndio, tulipewa misaada na Warusi, majengo ni mazuri lakini vile vifaa mle ndani kuwe na mkakati wa kukarabati na kujaza vifaa vya kisasa ili Chuo kilingane na sifa hizi na majukumu haya ambayo tunataka kukipa. Vinginevyo, tutakuwa na jina nzuri wakati shughuli zenyewe ni zile zile ni *new wine in old bottles* au *old bottle* zikiwa zina *new wine.*

Kwa hiyo nilikuwa napendekeza kwa makusudi ili kujenga hadhi ya Chuo hiki kiweze kutoa watu wanaofanana na malengo haya, tui-*equip* na tuwe na mkakati huo. Kama alivyosema Mheshimiwa Waziri kufundisha watu, haitoshi, haiwezekani wapate sayansi na teknolojia kwa *bio-osmosis simply because* wako kwenye majengo yameandikwa majina haya, basi wakawa na elimu ya juu, hapana. Kwa makusudi tu-*equip* watu wale na mahali pa kujivunia kwamba ukisoma Mbeya utatoka na utaalam ambao unatambulika popote katika nchi hii. Vinginevyo, vile vifaa kwa kweli bado havifanani na lengo letu hili.

Wazo la mwisho nililolisema kwa upande wa *Department* kama ilivyoonyeshwa kwenye ukurasa ule wa nne, mimi nafurahi kwamba ile (p) ya mwisho wameruhusu vile vile kuongeza *departments* nyingine na ndio pale nilikuwa napendekeza kwamba suala la Uyole ambayo imekuwa imeachwa hivi karibuni, miaka mitano haitumiki vizuri ingeweza ikaingizwa hapa na kufanya mambo yakaenda vizuri sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, namalizia kwa kusema kwamba naunga mkono pendekezo la Muswada huu. Lakini hili wazo la wanawake nadhani mngekuwa mna-*qualify* tusije tukaonekana tukisema wanawake, basi tutapigiwa makofi tuseme *woman who has relevant qualifications.* Vinginevyo si vizuri kuendelea tu *as if* lengo ni wanawake. Ahsante sana. *(Makofi/Kicheko)*

**MHE. BENSON M. MPESYA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa naomba nikushukuru kwa kunipa nafasi hii ili na mimi niweze kuchangia katika Azimio lililoko mbele yetu leo hii.

Kwanza kabisa naomba na mimi nitumie fursa hii kuungana na Wabunge wenzangu katika kutoa rambirambi zangu za dhati kwa ndugu, jamaa wa Marehemu Balozi Ahmed Hassan Diria ambaye mimi binafsi nilikuwa naye karibu sana kwa sababu alikuwa ni mjumbe mwenzangu wa Kamati ya Bunge ya Mambo ya Nchi za Nje. Naomba Mungu ailaze roho ya Marehemu mahali pema peponi.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nitumie wasaa huu kwanza kabisa kuliunga mkono Azimio hili la Kuridhia Chuo cha Ufundi cha Mbeya kuwa Taasisi ya Sayansi na Teknolojia. Imenichukua karibu miaka mitatu nazungumzia juu ya kukibadilishi Chuo cha Ufundi cha Mbeya na kuwa Chuo Kikuu cha Sayansi na Teknolojia, kama agizo tulilowahi kuachwa na Baba wa Taifa. Kuna wakati nilikuwa na wasiwasi kwamba nisije nikakosana na Mwalimu wangu Mheshimiwa Dr Pius Ng'wandu ambaye amenifundisha darasani, lakini nashukuru sasa kumbe bado alikuwa anaendelea kunifundisha kwamba tunajali hali hiyo, lakini inatakiwa iende kwa taratibu na kanuni ambazo zitatusaidia hatimaye tupate Chuo cha Sayansi na Teknolojia. Naomba nitumie fursa hii kumpongeza sana kwanza Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu, Wakurugenzi wote bila kumsahau *Principal* wangu wa Chuo cha Ufundi cha Mbeya ambaye amekuwa msaada na karibu sana kwangu ambaye hapa namwona yupo na mimi nafarijika kumwona yupo na *mission* yetu inakamilika, inaelekea kukamilika.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kwanza niingie katika hatua ya kwanza kwenye hii sheria yenyewe. Nianzie pale ukurasa wa tano wenzangu wamezungumzia, Mheshimiwa Jackson Makwetta, amezungumzia. Lakini naomba na mimi niongeze tu kwa sababu pengine sasa tunakibadilisha Chuo hiki kiwe cha Kitaifa si lazima sana awe Mbunge wa mahali pale, lakini hoja ya kuwepo Mbunge katika Bodi ile ni muhimu, ni muhimu sana kwa sababu ndio mwakilishi na hata kukisukuma chuo hiki nafikiri Wabunge wenzangu pamoja na Mwenyekiti wa Kamati ya Huduma za Jamii wamefanya kazi ya ziada.

Kwa hiyo, ninaafiki kabisa kwamba wazo la kuwa na Mbunge kama mwakilishi ndani ya chuo hii ni muhimu sana, si lazima atoke pale kwa sababu tunajenga kitu ambacho ni cha Kitaifa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, la pili katika ukurasa huo huo wa tano, kwa sababu tunakibadilisha chuo kuwa Taasisi ambayo itakuwa kubwa na nzito, ni vyema tukaanza kujitayarisha mapema kwa sababu uelekeo wetu ni kuwa Chuo Kikuu. Napendekeza nafasi ya mwakilishi wa wafanyakazi *RAAWU* naye apewe nafasi katika wajumbe hawa, itatusaidia kupunguza matatizo na migogoro mbalimbali ya mahali pa kazi.

Sehemu nyingine katika upande huo huo labda nieleweshwe tu labda ni suala tu la *Semantics* katika sehemu ya pili inazungumzia juu ya *The Minister shall in Appointing Members Under Sub Paragraph One, Insure Priority is Given to Women.*

Mimi kidogo hili hili limenikwaza, nilifikiri labda lugha ya kutumia hapa tungesema tu kwamba suala zima la kuwa *gender sensitive* lizingatiwe. Lakini tunaposema *priority is given to women, specifically women.* Sasa mimi sina mgogoro na wanawake kwa sababu mimi mwenyewe ni *product* ya mwanamke, nimezaliwa na mwanamke. *(Makofi)*

Lakini ninachohoji ni hii *trend* kwa sababu nafikiri kinachotakiwa kizingatiwe pale ni sifa zaidi. Kama tutaamua kupeana peana hivi hivi tu ili mradi ni mwanamke basi si ajabu ukatukuta na wengine sasa tumeamua kwenda hospitali tujibadilishe jinsia ili tu ziweze kufaidi haya mambo. Lakini mimi nafikiri kwamba zaidi iwe ni sifa, tunampeleka mtu ambaye tutahakikisha kwamba atajenga pale. Maana hata wenzetu, mtaniwia radhi akinamama maana yake na ninyi tukiwasema kidogo mnatukimbilia majimboni. *(Kicheko)*

Lakini ninachozungumza ni kwamba sisi wote ni kitu kimoja, lakini tunazungumza ni kwamba *priority* apewe mtu ambaye anaweza akafanya kazi na anasifa za kuwepo pale, tusipeleke tu ili mradi ni mwanamke hiyo ndio hoja yangu ya msingi.

Mheshimiwa Naibu Spika, niende sasa ukurasa wa saba, sasa huyu *Principal* tunabadilisha kuwa Taasisi, kwanza nashukuru sana, leo tutakuwa tumetatua mgogoro ambao ulijitokeza, Mkuu wa Chuo anajua nilifuatwa na vijana waliokuwa wanachukua *Bachelor of Engineering* ambao walibadilishiwa kwamba warudi kwenye *ADE,* kwenye *Advance Diploma in Engineering* kwa sababu ya taratibu zilizokuwepo. Ulikuwa ni mgogoro lakini nashukuru sana kwamba *Principal* na wenzake, pamoja na mimi mwenyewe tulisaidiana kuhakikisha kwamba hiyo hali tunaituliza. *(Makofi)*

Lakini leo hii nafikiri tumepata suluhisho la kudumu, sina mgogoro tena katika hili. Lakini naomba nizungumze tu kwamba kwa sababu Mkuu wa Chuo sasa anakuwa mtu mkubwa ni vema tumwekee wasaidizi wawili awepo *Director of Studies* na *Director of Administration.* Kwa sababu tunakipa hadhi na naamini kabisa *Principal* atakuwa ni mtu ambaye sasa atakuwa anakwenda huku huku kwa ajili ya mambo ya kuzungukia, kushughulikia mambo ya chuo. Sasa tukimwekea watu wawili hawa hata ile dhamira ya

dhati kwamba sasa tunaki-*transform* kuwa Chuo Kikuu itakuwepo nilikuwa naomba tumwekee watu wawili hao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niende sasa katika mambo mengine, ushauri wangu kwa ujumla. Ningeomba kwa sababu sasa tunakibadilisha Chuo kwa ajili ya kutoa *Bachelor of Engineering* na kozi zingine zingine kwa ajili ya kuimarisha stadi za kazi, naamini hapa sasa tunatayarisha watu ambao *purely for applied technology.* Ambao watakuwa wanatutatulia matatizo yetu wakulima, wafanyabiashara, viwanda, matatizo sasa yatakuwa yanapata ufumbuzi kwa kutumia hawa. Nilikuwa naomba na napendekeza kwamba elimu yao ya mafunzo kwa vitendo iongezwe, badala ya wiki nane iwe wiki kumi. Nimeshaona matatizo yamejitokeza kwenye Chuo Kikuu cha Dar es Salaam badala ya wiki nane wanakwenda wiki sita, lakini hawa sasa tunawatayarisha kabisa kwa ajili ya stadi za kazi. Ni vema muda wa vitendo ukawa mwingi zaidi kuliko nadharia kwa sababu hawa kazi yao kubwa ni kuibadilisha nadharia na kuwa kwa vitendo na hatimaye kumkomboa Mtanzania katika sayansi na teknolojia.

Mheshimiwa Naibu Spika, ushauri wangu mwingine ni juu ya mpango thabiti kabisa wa kuwaanda walimu ndani ya chuo hiki. Nimefarijika kuona zipo juhudi kubwa sana zilizofanywa na Wizara, na zinaendelea kufanywa na Wizara.

Lakini nilifikiri ni vema tukawa na mpango kabisa kwa sababu nafikiri ni mwaka jana waliomba kupata walimu lakini nafikiri katika usaili walioufanya alipatikana mwalimu mmoja tu, naye ana *Master of Business of Administration,* ambaye kwa chuo kama hiki sidhani kama atakuwa *relevant* sana kwa sababu kama walivyoshauri Waheshimiwa Wabunge wenzangu tunahitaji kabisa chuo hiki kizame katika sayansi asilia. Ili kumpatia Mtanzania kumtatulia matatizo yake ya kiteknolojia.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunaingia katika utandawazi, tunaingia katika shirikisho la Afrika Mashariki, wenzetu wa Kenya, wa Uganda wako mbele na sasa sisi tusipofanya jitihada ya kuhakikisha kwamba tunatoa wataalam watakaokuwa wanawapatia wakulima utatuzi, tutaishia vijana wetu wengi kuwa ni ma-*house boy,* tutakapoanzisha shirikisho. Badala ya kuwa wafanyakazi na nalitoa hili kwa sababu ukiangalia sasa hivi karibu hoteli nyingi za ufukweni Zanzibar na Tanzania, vijana wanaohudumia hoteli zile ni wa kutoka nchi jirani, sasa hii ni hatari kabisa, lazima tuliangalie hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ushauri wangu mwingine ni juu ya vifaa, ingawa ndugu yangu Mheshimiwa Benedicto Mutungirehi alizungumza hapa akasema vifaa vingi ni vya mwaka 1918, lakini nataka nimhakikishie tu kwamba juhudi zilizofanywa na Wizara ni nzuri sana, mimi mwenyewe nimejitahidi kutembelea na nimeona kwa kweli wanakwenda kisasa. Lakini nafikiri kikubwa alichotaka kuzungumza Mheshimiwa Benedicto Mutungirehi, ni kwamba alikuwa anasisitiza tu kwamba chuo hiki kwa sababu tunakitegemea basi kiendane na karne hii ya 21. Tujitahidi kukipatia fedha, rasilimali zitakazotusaidia kiwe na vifaa vya kutosha.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho kabisa naomba nitoe angalizo juu ya ardhi, tunalo tatizo, nakushukuru Mheshimiwa Jackson Makwetta umelizungumza, lakini sio tatizo kubwa sana Serikali imejitahidi tumewalipa fidia. Lakini yapo yale maeneo ambayo wananchi mpaka sasa hivi hawajalipwa fidia yao na wafanyakazi wa chuo hiki wanawafukuza wananchi wale wasiendeleze ardhi yao bila sababu za msingi kwa sababu kama hawajalipwa fidia ni vema wananchi wakaheshimiwa wakabaki kwenye maeneo yao mpaka watakapokuwa wamelipwa fidia na bahati nzuri na wao wenyewe wameshajua kwamba sisi ni wakuondoka, tutaondoka hapa, wanachongoja ni kupewa kifuta jasho waondoke na bahati nzuri si wengi sana ni wachache. Upo mgogoro wa watumishi wachache ambao wanawafukuza hawa wananchi wasiendeleze mashamba yao wakati wananchi hawa Serikali imekiri kabisa kwamba haijawalipa fidia.

Kwa hiyo, nilikuwa naomba na si jukumu la Wizara peke yake na sisi tutazidi kupiga kelele bila shaka katika Bajeti ya safari hii hilo lita-*reflect* kwamba tuwaondolee hao ili kusiwe na mgogoro chuo kiwe na ardhi yake.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nirudie tena kwa dhati ya moyo wangu na katika siku pengine nitalala nimefarijika ni siku ya leo kukiona Chuo cha Ufundi Mbeya kinabadilika na kuwa *MIST*.

Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana na kuipongeza Serikali. *(Makofi)*

**MHE. DR WILLIAM F. SHIJA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi tena niweze kuchangia hoja ya Azimio hili la kuanzisha Taasisi ya Sayansi na Teknolojia kule Mbeya, kwa mwelekeo wa kuanzisha Chuo Kikuu cha Sayansi na Teknolojia hapa nchini.

Kwa ujumla kwanza napenda nimpongeze Mheshimiwa Waziri pamoja na wale wote wanaomsaidia kwa kutengeneza sera mbalimbali ambazo na sisi wengine tulioanzia kwenye Wizara hiyo katika miaka ya 1990 mapema tulikuwa tumependekeza. Kwa hiyo, nimefarijika kusikia kwamba tulikamilisha sera ya elimu ya juu, tukakamilisha sera ya ufundi na sera zingine ambazo zimeandaliwa na hata hivi sasa tuna maeneo katika sheria na katika usimamizi wa kawaida ambayo yamekuwa yakiendelezwa.

Mhehsimiwa Naibu Spika, mimi nasema hivyo kwa moyo mkunjufu kwa sababu ni kweli kabisa kwamba wale wote wanaomsaidia Mheshimiwa Waziri wa Sayansi na Teknolojia na Elimu ya Juu kwa upande wa wataalam tulianza nao mwaka 1990 na 1991 tuliweza kupata nafasi ya kuangalia maeneo yote kuanzia Dar es Salaam mpaka Arusha mpaka Mbeya na tulianza na matumaini kwamba hatimaye lazima tutaanzisha chuo chetu cha Sayansi na Teknolojia kule Mbeya na wenzangu wamenikumbusha vile vile kwamba Baba wa Taifa aliwahi kulisema hili jambo katika miaka ya 1970 na nakumbuka hata nilipomtembelea Butiama mwaka 1991mwezi kama wa tano hivi, aliweza kukumbusha tena kwamba ili Taifa liweze kuwa na uimara zaidi lazima tujiimarishe katika sayansi na teknolojia.

Kwa hiyo, mimi napongeza sana Wizara kwa kupiga hatua hii na naunga mkono kwamba Azimio hili tulipitishe ili kusudi kazi ianze. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda nipendekeze tu kwamba suala la sayansi na teknolojia halianzii katika ngazi ya juu. Mheshimiwa Jackson Makwetta amenitangulia katika wazo hili na nasema kwamba ni vizuri wakati tunataka kukamilisha sasa kuwa na Chuo Kikuu na Taasisi basi tufuatilie vile vile katika shule zetu za msingi na sekondari. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, utamaduni na utaratibu wa sayansi na teknolojia tunauandaa namna gani. Ni lazima tuwe na mitaala ambayo tunaifuatilia kwa makini, mara kwa mara na kuboresha katika suala zima la mafunzo na elimu ya sayansi kwa vijana, na lazima tuendelee kuandaa walimu, ambao watakidhi katika kuandaa vijana wakuingia katika chuo kikuu hiki, kuanzia na Taasisi hii. Usipokuwa na walimu wazuri au walimu wanaopaswa kuwepo katika elimu ya msingi na sekondari, basi matokeo yako hayatakuwa mazuri katika Chuo Kikuu hiki au Taasisi hii.

Kwa hiyo, nashauri kwamba pamoja na nia hii naomba sisi Watanzania tuendelee kuwa wazi katika kuitazama kwa pamoja sekta nzima ya elimu ili tuhakikishe kwamba tuna walimu, tuna vifaa na tunaendesha mambo katika usawa ili kutoa fursa sawa kwa Watanzania ambao wanajifunza mambo mbalimbali na hasa ya sayansi na teknolojia na wanapenda kuwa mabingwa baadaye katika maeneo haya.

Mheshimiwa Naibu Spika, hivi karibuni ninapozungumza suala la usawa nilikumbana na swali la mtu mmoja huko Kiomboi wakati naenda kutafuta kuomba wadhamini katika kugombea nafasi ya urais kwa uteuzi wa Chama cha Mapinduzi na nasema yale yaliyo haki tu yaliyofanyika. Akaniuliza yule kijana kwamba anafikiria kwamba pameanza kukosekana na usawa katika kutoa elimu kwa Watanzania, yeye aliwaza hivyo kwamba kuna baadhi ya maeneo yanaonekana kama yanapata au yanafaidi zaidi katika kupata elimu bora na maeneo mengine yameanza kukosa elimu bora. Utofauti huu mimi nilifikiri baadaye kwamba lazima tuufanyie utafiti ili turudi katika miaka ya nyuma ambapo vijana wetu kutoka sehemu mbalimbali ziwe za vijijini na sehemu zingine ambazo tunaweza tukaziita pembezoni wapate usawa katika huduma ya elimu. *(Makofi)*

Hasa fursa sawa katika kufuatilia mambo ya Sayansi kwa sababu vipaji katika akili ya binadamu Mwenyezi Mungu peke yake ndio anavitoa, na sisi wote ni mashahidi kwamba unaweza ukampata Mwanasayansi mzuri kabisa kutoka ndani ya vijiji vyetu mbali kabisa na maeneo ya vifaa vya kisasa au mazingira ya kisasa. Eneo hili nilikuwa nadhani Watanzania tuwe na ujasiri wa kulitazama kama kweli pameanza kujitokeza kukosekana kwa usawa katika elimu ili kusudi tulirekebishe na tulifanyie kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo la pili linalofanana na hilo ni eneo zima la Sayansi na Teknolojia na nguvu kazi ya Taifa. Mimi nasema nafarijika kuona kwamba Taasisi kama hii ikiwa inasaidiwa na Taasisi zingine ndogo ndogo chini yake, itaweza kupanua ujuzi wa Watanzania Kitaifa kwa ujumla. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Taifa tunaona kwa Mataifa mengine linajitegemea zaidi likipata ujuzi wa namna mbalimbali, mathalani tunavyoeneza maji vijijini lazima pawepo na mafundi wa mabomba kuweza kuhudumia pale ambapo panatokea uharibifu wa kawaida. Haiwezekani ukaweka mtandao wa mabomba na ukategemea kwamba uwe na mfumo mzuri wa maji kama huna fundi bomba wa kuweza kuhudumia kwa matatizo madogo madogo ambayo yatajitokeza pale kijijini.

Halikadhalika katika mambo ya vifaa vingine, viwe vifaa vya simu, viwe vifaa vya luninga, viwe vifaa vya redio, viwe vifaa vingine katika ujumla wa kupata huduma ya kiteknolojia, lazima tuendelee kuandaa kada ya namna hiyo ambayo nadhani *VETA* wenzetu wanaifanya vizuri. Lakini lazima tuimarishe maeneo chini kidogo ya Taasisi kama hii ya Mbeya tuweze kuwa na kada ya namna hiyo na Mheshimiwa Jackson Makwetta umerudia tena, aliizungumza vizuri zaidi sehemu hii pengine kuliko mimi.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninasema vile vile kwamba ili tuweze kujiimarisha katika maendeleo lazima ujuzi huu tuufananishe na nchi kama India, China na Malyasia ambao wamekuwa wakiendesha mafunzo ya Sayansi na Teknolojia hata usiku. Sasa hivi ili kuukabili utandawazi, tunaambiwa wenzetu wa China wanaendesha mafunzo usiku kwa watu wanaowaita wamachinga wa Kichina. *(Makofi)*

Maana yake wanajaribu kukabili hali iliyopo ya kiutandawazi kuwapatia ujuzi vijana wao, mchana wanaweza kuuza bidhaa zao wanaweza, wanaendesha biashara zao. Lakini usiku wanapata nafasi ya kuwaongezea maarifa zaidi ya namna ya kufanya na kuikabili hali ya utandawazi ilivyo na tunapata taarifa kwamba wanafanikiwa.

Lakini hata ukirejea India, kwa watu ambao wamekaa India kama mimi, ukifika India utaona kuna vifaa vingi vidogo vidogo vya kumsaidia mtu binafsi kwa maisha yake ya kila siku ya kiufundi ambayo hayana gharama kwa sababu wana mafundi wa kutengeneza maeneo hayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, nadhani na sisi tukijibidiisha namna hiyo tunaweza hatimaye tukakomaa kabisa katika utamaduni mzima wa Sayansi na Teknolojia, tukiwa tunaongozwa na Taasisi kama hizi na nyingine ambazo zitaanzishwa kwa ajili ya kusaidiana na hali hii ya Elimu ya Juu.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine ambalo nilitaka niliseme ni kwa kituo kama hiki au Taasisi au Wizara kwa ujumla kutafuta namna ya kufikisha utamaduni huu katika ngazi ya Wilaya, Mkoa, Tarafa, Kijiji ili wote tujaribu kwenda pamoja katika utamaduni wa kiufundi, utamaduni wa kiteknolojia. Mheshimiwa Waziri anaweza akakumbuka, kuna pendekezo kwenye Wizara yake ambalo tulijaribu kulianza hapo zamani la kusema kwamba, basi ni vizuri hii taarifa ya ubora, ujuzi wa Sayansi na Teknolojia tukaufikisha katika ngazi ya Wilaya ili sote tufahamu kwamba unapozungumza Sayansi na Teknolojia inatuhusu wote. Inatuhusu Watanzania wote tuweze kuboresha namna ya kupata utamaduni wa kisayansi. Suala hili nadhani lina nafasi ya kufuatiliwa na likifuatiliwa vizuri litatusaidia sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, sambamba na wazo hilo na Azimio zima hili la kuanzisha Taasisi ya Sayansi na Teknolojia kule Mbeya, mimi naomba vile vile tuhakikishe kwamba wanafunzi na wahitimu baadaye wanakuwa na uwezo wa mawasiliano. Wengine katika kuangalia, tumeona kwamba udhaifu mmojawapo mkubwa katika Vyuo Vikuu vyetu au Taasisi za Elimu za Juu ni kukosa uwezo wa mawasiliano. Wanafunzi na wahitimu kukosa, kwa Kiingereza tunaita *Communication Skills* yaani uwezo wa kujieleza kwamba anajua nini na anaweza akaeleza mtu mwingine kitu gani, iwe kwenye Mkutano, iwe kwenye Kongamano au kwa wenzake.

Mheshimiwa Naibu Spika, udhaifu huu ni mkubwa na hatuna budi kukiri na tuufanyie kazi. Kwa mfano, tofauti iliyopo kati ya wanafunzi wanaomaliza Vyuo Vikuu vya Tanzania, Kenya na Uganda kwa maana ya kutafuta ajira ni katika eneo hili la uwezo wa mawasiliano. Sio katika uwezo wa kujua masomo yenyewe, uwezo wa kujua masomo vijana wetu wanajua vizuri sana na tunafundisha vizuri sana. Lakini kufanya mawasiliano inakuwa ni tatizo. Kwa hiyo, mtu anashindwa kufanya *interview* tu ya kawaida kwa sababu anakuwa hakujiandaa na hakuandaliwa kuwa na uwezo wa kuwasiliana na binadamu wenzake katika lugha ya Kiingereza.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini la mwisho kabisa niseme kwamba, Waafrika sisi pamoja na Tanzania bado tuna nafasi katika eneo hili la Sayansi na Teknolojia ya kuweza kuimarisha uchumi wetu kwa kuwa mafundi wa aina mbalimbali au wa kupata mafundi wa aina mbalimbali. Kwa hiyo, mimi ninapongeza sana juhudi hizi na juhudi nyingine ziongezwe ili tuhakikishe kwamba katika Sayansi na Teknolojia Tanzania inajikomboa, Afrika nzima inajikomboa na tunaendelea kushirikiana na wenzetu katika nchi za majirani na Afrika kwa ujumla ili tuweze kuwa na Mataifa na Bara lenye ufundi.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hivyo nasema tena kwamba naunga mkono hoja, nawatakia kila la kheri Mheshimiwa Waziri katika utekelezaji huo na wataalam wetu tunawatakia juhudi njema, nidhamu nzuri ili kuweza kutiza azma hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, kabla sijamwita mchangiaji anayefuata, nitoe tu ufafanuzi mdogo. Kwanza juu ya mchangiaji anayefuata ameomba achangie Azimio hili na linalofuata. Kwa hiyo, kwa sababu yote yanajadiliwa kwa pamoja, tunakupa nafasi moja ili uchangie yote kwa pamoja. Lakini la pili, Msemaji wa Kambi ya Upinzani, kwa hoja ile ya pili, Azimio la pili hakupata nafasi, alikuwa na dharula nje. Kwa hiyo, baada ya kuchangia wote, nitampa nafasi ili atoe maelezo yake kutoka Kambi ya Upinzani.

**MHE. OMAR MJAKA ALI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa na mimi nafasi hii ya kuchangia Azimio hili muhimu.

Mheshimiwa Naibu Spika, moja kwa moja na mimi naunga mkono Azimio hili asilimia mia kwa mia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kilichonisababisha nisimame hapa ni kutokana na misingi ambayo imeelezwa kwenye Azimio hili. Mimi nataka niiombe Serikali yetu ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, pamoja na hali yetu ya umaskini wa Taifa letu na ukubwa wa Taifa letu, lakini sasa hivi imefikia ipo haja ya kuweza kubadilisha mfumo wetu wa utoaji wa elimu ya lazima kwa vijana wetu wa Tanzania, kuondoka pale Darasa la Saba kufikia angalau Sekondari, kama haitafika Kidato cha Nne, basi angalau iwe hata Kidato cha Pili.

Mheshimiwa Naibu Spika, nazungumza hili kwa dhati kabisa kwa sababu sasa hivi suala la elimu ndio msingi kwa ajili ya maendeleo ya mtu na Taifa kwa jumla.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Azimio hili, nasema, kwa kuwa Serikali katika mikakati yake ya kuondoa umaskini na kuboresha maisha ya Watanzania imeweka kipaumbele katika kuendeleza na kuimarisha elimu ya Sayansi na Teknolojia hapa nchini, tuangalie huu umuhimu sasa kwa vijana wetu ambao wanamaliza Darasa la Saba na wanakuwa katika umri mdogo sana wapi wataweza kukidhi, kupambana na matatizo kama haya, kupambana na umaskini na kuboresha hali za maisha za wananchi wetu wa Tanzania. Kwa hiyo, hapa ndipo nilipothubutu kuiomba Serikali yetu ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kuangalia mfumo wake wa utoaji elimu wa lazima kwa vijana wetu katika nchi yetu ya Tanzania. Sasa imefika wakati ifanye opesheni ya lazima ili tuanze kutoa elimu ya lazima mpaka Kidato angalau cha Pili kama haitawezekana kufika mpaka Kidato cha Nne.

Mheshimiwa Naibu Spika, Azimio hili ni muhimu sana na kwa kweli linagusa Chuo hiki ambacho kipo Mbeya. Tunasema kiko Mbeya tu lakini kitawagusa Watanzania wote. Mimi nataka niungane na wenzangu kwamba kusiwe na mgawanyiko fulani kwamba labda kuchukua jinsia fulani tu kwenda, ni vizuri Chuo chetu hiki tukakiimarisha na kuweza kutoa elimu kwa Watanzania wote ambao watastahili kuingia katika Chuo hiki. Kwa hiyo, niiombe Wizara kwa kweli ikiboreshe na iweze kukifanikisha ili kuleta faida kubwa kwa Taifa letu hili la Tanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, huwezi kuzungumzia uchumi ulio katika dunia bila kugusia masuala ya teknolojia. Mfumo huu wa teknolojia ndio ambao sasa hivi wenzetu unaowapeleka mbele na mifano inaonekana. Kama hatukuwa makini katika masuala kama haya, itafikia wakati Watanzania tutagawanyika katika sehemu mbili kama ambavyo inavyogawa watu wa Mijini na walioko Vijijini, lakini suala la maendeleo linazidi kuchangia kwenye suala la elimu. Mimi naamini elimu inayopatikana katika Mijini ni tofauti na Vijijini.

Kwa hiyo, ni vizuri kuweza kufungua vifaa vya kutosha katika Shule hii na kuweza kuwapatia wananchi wote ambao wanastahili bila kugawa kwamba labda kwa jinsia maalum, kwa sababu tunachotarajia hapa ni wataalam kwa ajili ya maendeleo ya Taifa letu hili la Tanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kuthibitisha nini umuhimu wa Sayansi na Teknolojia, Azimio linatuambia kwamba baada ya Chuo kuboresha na kupanua program

zake, kitaweza kutoa wataalam ambao ni wanasayansi na wanateknolojia wenye muelekeo wa vitendo zaidi kuliko nadharia na wenye kukubalika katika soko la ajira na mfumo wa sasa wa utandawazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa hivi utandawazi umesaliti nchi nyingi sana duniani. Kama dhana iko hivi, ni lazima Serikali ichukue juhudi za lazima katika kufanikisha haya malengo, si kuwasilisha tu hili Azimio kwa ajili ya kwamba tumelichangia, ni lazima tuhakikishe kwamba yale malengo tuliyoyakusudia kwa faida ya Taifa hili, kwa faida ya watu wa nchi hii ni yaweze kufutiliwa. Kwa hiyo, nimtake Mheshimiwa Waziri kwamba suala hili alisimamie na tukute mabadiliko makubwa kwa ajili ya mambo ya Sayansi na Teknolojia kwa vijana wetu na Taifa letu kwa ujumla.

Mheshimiwa Naibu Spika, nikiacha kwenye Chuo hiki, nataka niende kwenye lile Azimio la pili ambalo linasema: "Kuridhia Mkataba wa Kimataifa Unaohusu Utunzaji na Ulinzi wa Vyombo vya Nyuklia." Ni Azimio muhimu na sasa hivi dunia imesalitika kwa mambo kama haya, tumeona Marekani alivyoishambulia Iraq kwa sababu ya silaha za nyuklia; tumeiona sasa hivi Korea ya Kaskazini ambavyo inataka kuishughulikia na Iran. Kwa hiyo, haya Maazimio mazito ambayo tunayaridhia lazima tuwe waangalifu yasije kutuathiri hapo baadaye. Hili tunalazimika tuliangalie kwa mapana kabisa na kwa sababu linasema kwamba Mkataba huu wa Kimataifa tunazuia namna gani katika kuingiza vifaa hivi? Lakini je, tutakuwa ana uwezo kweli? Mimi naona uwezo haupo. Ushahidi sahihi ni kwamba sisi zaidi ya miaka mingi sasa hivi Zanzibar tunakutana na milipuko hii ambayo tunalifanyia hofu na zinatumika baruti hizi hizi. Sasa leo tunaridhia Maazimio kama haya, je, tutakuwa na uwezo wa kuweza kuzuia? Kama itabainika kwamba wako watu walioruhusu yakaweza kuingia na ikatokea athari katika eneo moja la nchi hizi, ni adhabu gani iliyowekwa?

Mheshimiwa Naibu Spika, ni hatari. Juzi juzi Zanzibar tulisikia, tuachilie ile ya miaka ya nyuma kule Pemba. Kwa hiyo, mimi nimwombe sana Mheshimiwa Waziri kwamba tunaridhia Azimio hili, lakini ni vizuri tukawa wakweli. Ni vizuri vile vile tukaimarisha vyombo vyetu vya ulinzi na usalama katika maeneo yote ya Bandari, angani na maeneo mengine yote.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi imenitia hofu kwasababu nafikiria ni namna gani tuna vyombo vya kuweza kupekua ile mizigo ambayo tunaipeleka katika makontena yanayokwenda nje. Tutakuwa na uhakika gani kama baruti hizi zitakuwa hazimo katika *parking* ya ile mizigo? Kwa hiyo, ni vizuri tunaporidhia Maazimio kama haya, vile vile tukaweza ku-*broke* zile njia na kuweza kujua ni namna gani hizi baruti zitakuwa zinaingia.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama tutaweza kufanikisha hilo, nataka niseme kwamba Azimio letu litaweza kufanya kazi. Lakini sasa hivi kwa mfumo wa dunia unavyokwenda, hali ya matukio ya dunia mimi naona hili Azimio litaweza kutusumbua sana na litatuweka katika matatizo makubwa sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kumalizia, mimi naishukuru sana kazi ya Azimio hili. Kwa kuridhia Mkataba huu, kutaiwezesha Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kushirikiana na Jumuiya ya Kimataifa katika utunzaji, usimamizi wa usafirishaji kwenye vyanzo vya mionzi ya nyuklia kutoka sehemu moja hadi nyingine ili kudumisha usalama na amani duniani. Hivi kweli tunaweza kupatikana? Iraq sasa hivi kila siku ukifungua *CNN* unakuta watu wamelipuliwa.

Kwa hiyo, ningeomba hizi nchi wanachama na kwa sababu hili suala tunalijadili katika Bunge na kitu ambacho kinapitishwa katika Bunge ni kitu kizito, tuhakikishe kwamba dunia imeweza ku-*control* suala hili. Watu wengi wanapoteza maisha yao, watu wengi wanarudi kwenye umaskini kwa ulipuaji kama huo ambapo baruti zinatumika na bahati mbaya haturidhii kwa Tanzania tu kwamba kwa usalama na amani ya dunia, sasa hivi dunia haina amani. Hayo yanafanyika huko nje ndio ambayo sasa hivi yanafika mpaka kwetu sisi Tanzania. Kwa hiyo, ni vizuri tunaporidhia Maazimio kama haya, dunia na hasa wakubwa wa dunia kweli wasituingize kwenye kuridhia masuala ambayo hatutakuwa na uwezo wa kuweza kuya-*control*.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya hayo yangu machache, namwomba sana Mheshimiwa Waziri ayaangalie haya na kama Serikali, iangalie vya kutosha na ilipokuwa haiwezekani, bora iseme haiwezekani kuliko kuridhia tu masuala ambayo yanaweza kuturudisha nyuma.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono asilimia mia kwa mia Maazimio yote mawili. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. ELIACHIM J. SIMPASA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi na mimi nichangie katika hoja hii ya Azimio la Chuo cha Sayansi na Teknolojia Mbeya. Maana ni vizuri nitaje sio tunachangia hivi hivi, kumbe mtu yuko kwenye nyuklia, basi watu wanachangia mambo ya Mbeya kumbe ni Azimio lingine. Kwa hiyo, mimi nasema nachangia Azimio la Chuo cha Sayansi na Teknolojia Mbeya.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza samahani, nilichelewa kidogo uliponiita lakini nashukuru kwa nafasi hii, kwa sababu tulikuwa tunajua kwamba atawakilisha mwenzetu kitu fulani halafu baadaye tutaendelea kuchangia. Jambo la kwanza nataka niseme, nawapongeza sana walioleta Azimio hili au hoja hii, Mheshimiwa Waziri na Naibu wake. Kwanza kwa sababu ya kazi nzuri ambayo ameifanya, Chuo kimeanza mwaka 1982 na kwa kweli ni miaka mingi imepata kama zaidi ya miaka 22 imepita. Marehemu Nyerere na ile Serikali ya Urusi ilisaidia sana katika kujenga Chuo hiki. Ni Chuo ambacho kimejengwa vizuri na majengo mazuri na kusudio lilikuwa iwe ni Chuo Kikuu. Lakini katikati kilidorora sana na baada ya Wizara kuona kwamba kimedorora, basi walikwenda kusaidia kukarabati.

Hivyo, nawashukuru sana, nawapongeza na hatimaye wao wenyewe pamoja na sisi Wabunge kadhaa humu tumeona yale majengo pamoja na nia ya Mwalimu ilikuwa ni kujenga Chuo Kikuu cha Sayansi na Teknolojia. Kwa hiyo tukapiga kelele sana hapa na

tukakubaliana na ikasemekana imekubalika kwamba sasa Wizara itakuwa inashughulikia ujenzi wa Chuo Kikuu cha Sayansi na Teknolojia Mbeya.

Mimi nafanya hivi kwa sababu nataka nieleweke sipigi historia lakini nataka niseme nilishasema hapa kwamba kama una kanguo kadogo kale kanaitwa *mpetee*, kakuficha tu eneo maalum, halafu mtu akakupa kaptura badala ya suruali unamshukuru. Kwa hiyo mimi nawashukuru sana. Kilichokuwa kinatakiwa pale ni suruali, (ni Chuo Kikuu cha Sayansi ya Teknoloji kule Mbeya), sasa leo tunaambiwa tutapewa kaptura. Kwa hiyo, nasema si kitu, ingawa sijaridhika sana. Kwa sababu jambo hili limeongelewa kwa muda mrefu na kwa kweli bahati mbaya sana mimi Dr. Pius Ng'wandu ni Mwalimu wangu, kwa hiyo, lazima niongee kwa adabu kidogo. Nasikitika sana kwa kuwa ndio yeye amekaa pale mbele, halafu ningeongea tofauti kidogo.

Sasa tulianza kuwaza kwamba labda hawa wana nia mbaya na Mkoa wa Mbeya kutojenga kile Chuo. Kwa sababu baadaye vilianza kujengwa Vyuo Vikuu vingi pale pale sehemu nyingine tu, nataka nim-*quote* Dr. Willium Shija aliposema, ni lazima tuanze kusambaza mambo makubwa nchi nzima. Tusiendelee kulundika mambo yote mahali pamoja tu, kama una *SUA* hapo hapo, una Mzumbe hapo hapo, vyote ni Vyuo Vikuu. Lakini sehemu nyingine hata kidogo wanachokihitaji, nafasi zipo ni kuongeza tu, unawapa kaptura badala ya suruali. Wananchi wa Mbeya sisi Wabunge ingawa naona Mheshimiwa Benson Mpesya amefurahia lakini hiyo imepita kidogo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sababu ikishakuwa Taasisi hii sasa itachukua muda mrefu tena kuwa Chuo Kikuu. Huku ni kupooza tu makali. Tumepooza makali ingawa wengine wanafurahia, lakini tumepoozwa tu. Wananchi walipoambiwa ni Chuo Kikuu, watu ni wagumu kuacha mashamba yao ya kahawa, fidia ya nini zile hela wameshazimaliza zamani, mashamba yangekuwepo bado. Lakini waliposikia ni Chuo Kikuu na siasa zikapigwa walijitoa kweli, ndio ekari hizi elfu moja zikapatikana. *(Makofi)*

Sasa leo unawaambia nini, kwanza hawajui kitu kinachoitwa Sayansi na Teknolojia Chuo Kikuu wanajua na mambo mengine sisi wengine ambao ni walimu na yeye Mheshimiwa Naibu Spika ni Mwalimu, siku zote tunapoongea mambo ya *terminology* hiki ni lazima tuwaeleze watu tunaongea juu ya nini. Watu wengine neno teknolojia watu hawaelewi. Kwa hiyo, kumwambia Mnyakyusa au Mnyamwanga pale kusema kimekuwa Chuo Kikuu, kimekuwa Taasisi ya Sayansi na Teknolojia, kwanza hawawezi kutamka halafu wanasema ndio kitu gani? Sisi tulitoa mashamba kwa Chuo Kikuu, Chuo Kikuu wanajua.

Kwa kweli itabidi Mheshimiwa Mpesya, pamoja na kuunga mkono sana, tukaanze kueleza upya kwamba hii ni sawa sawa na kama Chuo Kikuu, ni Chuo Kikuu tu ila inaelekeaelekea. Itabidi tutafute lugha ya kwenda kueleza sawasawa kinidhamu. Itabidi ujitahidi sana ndugu yangu maana tulitegemea tutapata suruali, lakini leo tumepata kaptura, lakini sio *mpetee*. Mimi sikufurahishwa, lakini nashukuru kuwa nia ni njema, tujifunze kusambaza Vyuo Vikuu hadi Lindi, Kigoma na Mbeya. Isiwe eneo moja tu Vyuo Vikuu vimekaa pale kama vile wengine hawapo duniani na hizi *differences* ndizo zinazoleta migogoro ya kisiasa baadaye.

Mheshimiwa Naibu Spika, nia ni njema, lakini sasa tumefungwa miguu kuwa Chuo Kikuu itachukua miaka mingine tena na *unless* na Mwalimu wangu ataniambia ni lini basi wata-*speed up* angalau sisi tukione kabla ya siku zetu. Lakini vinginevyo mimi nimeona tumevutwa shati kidogo na tulianza kuwaza vibaya, lakini kwa sababu tunajua Dr. Pius Ng'wandu hawezi kuwa anasema uongo, tulifikia mahali tukasema, huyu hana nia njema na kwetu. Tulikuwa tunanon'gona pembeni Mwalimu. Kabisa, mimi sitaki kusema uongo, mimi mtoto wa *Pastor*. Tulianze kusema huyu hana nia njema maana Vyuo vingine vimezuka tu hapa hapa juzi juzi majengo mengine sawasawa na ya kwetu, lakini Mzumbe *University*, wapi *University*. *Why not* Mbeya?

Halafu una bahati mbaya kuna wakati fulani Waheshimiwa hapa walikuwa wakipiga kelele, unajua nyie wengine hamjawahi kwenda Mbeya kwa ndege. Ukifika pale Mbeya unatafuta Kiwanja cha kutua, hakuna hata *turn way,* unatua tu kwenye nyasi. Halafu unajua Mji wa Mbeya japokuwa ni mkubwa kwa jina na utajiri mkubwa, lakini hakuna Kiwanja cha Ndege! Kwa hiyo, tunatua kwenye nyasi tu, unakuta ng'ombe, siku nyingine wanakuta mpaka watu waswage kwanza ng'ombe watoke, sasa tukapiga kelele hapa, wakasema watajenga *International Airport* pale Songwe, nayo inasuasua. *What's wrong?* Tatizo ni nini?

Mheshimiwa Naibu Spika, unajua watu waki-*collect* vitu vingi pamoja na kwamba *they can make a conclusion,* ndio Sayansi katika *processes* unakusanya hiki, unakusanya hiki *if the result are repetitive* unafanya ndio *results* zenyewe, ndio *conclusion* yenyewe. Sasa sisi huku tunaambiwa hiki chenyewe hata hakifai. Hiki Chuo Kikuu chenyewe tulisema watu tutakamata hapa itakuwa Taasisi, tunashukuru kwa kupata kaptura kwa sababu ya Mwalimu wangu.

La mwisho, Sayansi ndio inayotawala dunia na mwanasayansi wa kwanza ni Mungu mwenyewe. Mimi nachukua muda wangu sana kusoma vitabu vya *Space Organization System*, unakuta kweli Sayansi Mungu ameweka hivi, tunavyoongea tunaelea tuko angani a*nd people don't take time to see that* tuko kwenye *revolution* tunaendelea. Mwanasayansi Mungu mwenyewe amepanga jua ambalo ni kitu huwezi kugusa, lakini vile vile ana sayari zake zile amezipanga kwa *system* na ame-*computerize* kiasi ambacho haziwezi kuanguka. Kuna wanasayansi walisema sayari zitakaa pamoja, zitakuwa mstari mmoja, kwa hiyo kutakuwa na *pull,* lakini alishafanya Sayansi. Kwa hiyo hakukuwa na tatizo lolote.

Sayansi ndio inayotawala dunia. Wajapani walipopigwa sana, walipoanza, walipoji-*organize* kurudi pale, wakasema acha masomo ya historia na mambo mengine *let us go to* Sayansi, wakaenda na wanasayansi. Sasa hivi unaona, jana tulikuwa pale tunaangalia Nissan zile, vile ni vichwa, pale unaona *brain* ya watu wanafanya kazi na wale huwezi kukuta wanasengenyana kwa sababu *time* ya kusengenyana haipo. Utapata saa ngapi kutengeneza kitu kama kile wakati wewe ni mtu wa kuandika mambo ya ajabu ajabu na kusengenya tu watu?

**MBUNGE FULANI:** Huwezi!

**MHE. ELIACHIM J. SIMPASA:** Huwezi! Ila kama huna shughuli, utafanya mambo ya ajabu sana, *"an idle mind is the devils workshop".* Shetani anahamia kichwani, anasema fanya na hili, sema na hili, teta na hili, nena na hili kwa sababu kichwa chako hakina shughuli ya maana. *(Kicheko)*

Lakini jana Waheshimiwa Wabunge tuliokwenda pale tumeona yale ma-*nissan* yaliyokuja sasa hivi unashangaa moja unaweza kuendesha *automatic* lakini vile vile unaweza ukafanya *manual* kama unataka. Sasa wale huwezi kukuta siku moja wanazungumza juu ya mtu, wanaongea juu ya vitu, *how do we go,* hawaongei juu ya watu! Hiyo wameandaliwa kwa maana vifaa vya maana vimepatikana, kwa maana wataalam wamepatikana, kwa maaana masomo yao ni ya vitendo. Tunaomba Chuo kile kiwe cha vitendo, sayansi iwe ya vitendo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini wale Wajapan wameji-*organize themselves* mpaka Korea wameiga. Wanapomsomesha mtu wa sayansi hamwachii aende hivi hivi kienyeji bila ku-*tress* anakwenda wapi, lazima wamrekodi yuko wapi wamtumie, tena wamtumie vilivyo. Sisi unatoa watu wa sayansi pale *University of Dar es Salaam* hata ukiwauliza wametoa wangapi, wamekwenda wapi *nobody knows, nobody's business.* Hatuwezi kujikomboa katika hali ya namna hiyo.

Mhehimiwa Naibu Spika, Waingereza na Wakoloni walipokuja katika Afrika wali-*insist on history,* sawa *history* nayo ni nzuri sana ina mambo makubwa katika mambo ya utawala, lakini wakasema Waafrika wape historia zaidi, wape *literature*. Ndio maana Waandishi wazuri sana wa vitabu vya *African Writers* wako Nigeria, maana *Universities* zao zote zilikuwa za *arts* tu, akina Chinua Achebe, akina Soyinka wanaandika *arts* tu. Sasa sisi hatutaki hiyo, tunataka *history*, tunataka masomo mengine, lakini sayansi iwe ya vitendo, vifaa viende kwenye Chuo kile, masuala yote yaende pale, Walimu wawepo pale na kwenye Vyuo vyote vya sayansi na teknolojia. Lakini vile vile tuwa-*tress* tunawaweka wapi, tunawa-*motivate* vipi waweze kubaki ili wafanye kazi kwa maendeleo yetu. Lakini mtu anakwenda tu, tena siku hizi wanakopa hela sijui kama wamerudisha, mimi nilikopa zamani lakini sijarudisha hata senti moja. *(Kicheko/Makofi)*

**WABUNGE FULANI:** Ahaaa!

**MHE. ELICHIAM J. SIMPASA:** Kweli kabisa! Ni utaratibu tu, lakini tunashukuru labda utaratibu utakaokuja utakuwa mzuri. *How do you tress them?*

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Sasa namwita Msemaji wa Kambi ya Upinzani, Mheshimiwa Mutungirehi alikuwa hajatoa hoja yake kwa upande wa Upinzani.

**MHE. BENEDICTO M. MUTUNGIREHI - MSEMAJI MKUU WA KAMBI YA UPINZANI KWA WIZARA YA SAYANSI, TEKNOLOJIA NA ELIMU YA JUU:** Mheshimiwa Naibu Spika, niombe radhi tu kwamba kwa sababu za kisayansi, vile

vile hotuba yangu ilikwama kwenye *computer*, utaratibu ulivunjika. Kwa hiyo nizungumzie hapa badala ya kwenda pale kwa sababu wakati wake umeshapita.

**NAIBU SPIKA:** Hiyo wakati usijali, sema unaamua tu. *(Kicheko)*

**MHE. BENEDICTO M. MUTUNGIREHI - MSEMAJI MKUU WA KAMBI YA UPINZANI KWA WIZARA YA SAYANSI, TEKNOLOJIA NA ELIMU YA JUU:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii kutoa maoni ya Kambi ya Upinzani kuhusu Azimio la Bunge la Kuridhia Mkataba wa Kimataifa unaohusu Utunzaji na Ulinzi wa Vyanzo vya Nyuklia.

Kabla sijaendelea, niombe radhi kwamba hotuba yangu ilikwama kwenye *computer* lakini nadhani ndio utaratibu ulivyokuwa, niliamini kwamba kanuni zinasema kama Waziri ana Maazimio mawili, matatu yanayohusiana kidogo, atayatoa kwa wakati mmoja. Sasa bahati mbaya ni kwamba Maazimio yale mawili moja lilikuwa ni la Mambo ya Ndani ya Nchi na lilihusu Chuo Kikuu na lingine lilikuwa ni la Kimataifa vitu ambavyo ni tofauti, lakini vilitolewa kwa wakati mmoja. Sasa sio tatizo tutajaribu kutoa maoni hayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, pili, sio kazi yangu kumjibia Mheshimiwa Waziri kwa hoja zilizotolewa na Waheshimiwa Wabunge, lakini nadhani Mheshimiwa Mpesya arekebishe kidogo kwamba katika hotuba yangu ya awali sikusema vile vifaa katika Chuo cha Mbeya ni vya karne iliyopita kwa maana ya mwaka 1918. Nilichosema ni kwamba viliachwa na Warusi wa Russia ya Kisovieti na ukweli ndio huo kwa sababu tulifika pale tukaona kilichopo kipya ni *computer* za kawaida. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, Kambi ya Upinzani inaunga mkono Azimio lililoletwa na Mheshimiwa Waziri la kuhakikisha kwamba tunakuwa kati ya waliotia saini na kuuridhia Mkataba wa Kimataifa kuhusu Utunzaji na Ulinzi wa Vyanzo vya Nyuklia.

Mheshimiwa Naibu Spika, wakati tukiunga mkono Azimio hili tunataka kutoa angalizo kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, asubuhi ilitolewa orodha ya Maazimio ambayo yanahusu mambo ya nyuklia ambayo Bunge hili limeyaridhia katika uhai wa Bunge hili kuanzia mwaka 2000 mpaka mwaka huu. Nadhani hili ni Azimio ambalo linakaribia kuwa la mwisho.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi ya Upinzani tunaelewa na Mheshimiwa Waziri amelieleza Bunge kwamba Azimio tunaloridhia kwa kweli Mkataba wenyewe haujawekwa saini na Rais. Tunataka labda Mheshimiwa Waziri atufafanulie, inakuwaje. Tunaridhia kwanza ndio unawekwa saini au wanasaini kwanza ndio tunaridhia kwa utaratibu wa uendeshaji wa mambo?

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa tumeshaunga mkono na tulikwishaeleza madhara ambayo yanatokana na nguvu za nyuklia zinapotumika katika kutengeneza silaha, kwa leo tuna angalizo kidogo.

Mheshimiwa Naibu Spika, angalizo letu linasema kwamba kadri dunia inavyokwenda Azimio hili limeanzishwa kwa miaka ya 1980 na bahati nzuri halikuridhiwa na Uongozi wa Awamu ya Kwanza, Awamu ya Pili mpaka sasa tunaridhia katika Awamu ya Tatu, hatuwezi kujua sababu ilikuwa ni nini.

Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa zilizopo ni kwamba kuna nchi ambazo zimekuwa haziridhii Maazimio yanayohusu masuala ya nyuklia nchi kama Pakistan, India ambazo kwa kweli zimeweza kutengeneza silaha za nyuklia na kiranja mkuu wa dunia katika masuala hayo akiwa ni Marekani anazikumbatia na hajatoa hata adhabu kama anavyozikimbilia nchi za Iran pamoja na Korea ya Kaskazini. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na hiyo, tunapenda kutoa angalizo pia kwamba wakati sisi Wabunge tukiridhia, tuelewe kwamba kuna nchi ambazo zimechukua jukumu zenyewe kuwa nchi ambazo zimethibitishwa kumiliki silaha za nyuklia, kutumia teknolojia ya nyuklia katika silaha na katika kuzalisha nishati kwa ajili ya matumizi ya amani na salama.

Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na Mkataba huu, inafika mahali tunajenga hisia katika vichwa vyetu sisi Watanzania kwamba tunaweza kabisa tukaepuka suala zima la nguvu za nyuklia kwa matumizi ya salama kwa sababu ya hofu tunayokuwa nayo. Ushahidi wa hilo ni hapa majuzi tu ambapo zilikuwepo taarifa za kushtua kwamba Tanzania inalalamikiwa kwa kutaka kutengeneza kiwanda cha silaha. Katika hilo, tunampongeza Waziri wa Ulinzi, Mheshimiwa Profesa Phillemon Sarungi kwa msimamo alioutoa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tunasisitiza kwamba suala la ulinzi haliwezi kuwa na itikadi kwa sababu hata Marekani kwenyewe ikiwepo *Democratic* na *Congress Republic* hoja ni moja tu katika masuala ya ulinzi wa Taifa. Kwa hiyo, tunasisitiza kwamba hii isije ikatuzuia sisi kufikiri na kujiwekea utaratibu wa kuilinda nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, itakumbukwa kwamba, historia inatuonyesha kuwa wakati wa kupigania uhuru, nchi ya Tanzania ilikuwa ndio kiongozi wa nchi zilizokuwa katika mstari wa mbele katika ukombozi wa Afrika. Pamoja na umaskini wetu, pamoja na uchanga wa uchumi wetu kwa sababu ya mfumo imara wa ulinzi wa nchi yetu, nchi za Msumbiji, Angola ziliweza kusumbuliwa na Afrika ya Kusini wakati ule lakini hawakuweza kutukaribia sisi wala kutusumbua kufuatana na mfumo wa ulinzi wetu. Ndio maana tunampongeza Mheshimiwa Sarungi kwa hatua aliyoichukua. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninamwomba Mheshimiwa Waziri wa Sayansi na Teknolojia kama akiweza, ziko taarifa zinazohusu masuala ya jinsi ya kutumia nishati ya nyuklia katika masuala ya amani na hususani kuzalisha umeme, aweze kufanya Semina katika Bunge hili ili kuweza kuonyesha ni gharama kiasi gani zinahitajika katika

kuzalisha umeme wa maji, gesi, mafuta, makaa na umeme unaotokana na madini ya *uranium* na hii inaweza ikatufanya fikra zetu zisije zikafungwa na namna ya kuweza kutumia teknolojia ya kisasa ya nyuklia.

Mheshimiwa Naibu Spika, Azimio la leo limekumbana na Azimio lingine ambalo lilikuwa linaanzisha Taasisi ya Teknolojia na Sayansi, Mbeya. Tunadhani katika masuala haya, wakati umefika na ni wakati muafaka wa kuanzisha nyuklia sayansi katika chuo hicho. Sasa katika masuala haya ambayo tunaridhia, kama hatuwezi kuwa na msimamo na uamuzi wa pamoja huenda hata huo mtaala wa jinsi ya kujifunza masuala ya teknolojia ya nyuklia na yenyewe isiwekwe kwenye mitaala hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kutoa angalizo hilo, tunaomba Waheshimiwa Wabunge kwamba tunaporidhia masuala haya yanayohusu nyuklia wakati mwingine tuweze kupaza sauti na kuziambia nchi zilizoendelea kwamba kuna mambo mengine yanatatiza hasa inapofika kwamba wengine wanaruhusiwa kumiliki silaha hizo na wengine wanawatisha wengine wasiweze kumiliki silaha hizo na wasiweze hata kutumia teknolojia ya nyuklia kwa masuala yao. Nina uhakika kwamba tukipaza sauti hivyo, hakuna Taifa linaweza kuwaita Wabunge ambao ndio sauti ya watu likamchapa kila Mbunge viboko viwili kwa sababu tu amepaza sauti hivyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kuyasema hayo, tunaunga mkono hoja. Ahsante. Nawasilisha. *(Makofi)*

**WAZIRI WA SAYANSI, TEKNOLOJIA NA ELIMU YA JUU:** Mheshimiwa Naibu Spika, nitajaribu kutumia muda wangu vizuri ili mwenzangu ambaye naye ana Azimio aweze kupata nafasi.

Mheshimiwa Naibu Spika, naanza kwanza kwa kuwashukuru wachangiaji wote waliochangia kwenye hoja za Maazimio yetu yote mawili. Nitaanza kwanza na yule ambaye hamkumsikia naye ni Waziri wa Ulinzi, Profesa Phillemon Sarungi, ambaye ametushauri kwamba tuwe na kiungo kati ya sayansi, teknolojia tangu Elimu ya Awali mpaka kufikia Chuo Kikuu. Yeye ameshauri tuanzishe Vituo vinavyoitwa *Polytechnics. (Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la *Polytechnic* limejadiliwa sana katika nchi hii tangu mwaka 1980, mimi nililikuta linajadiliwa na linazingatiwa. Katika Sera ya Taifa ya Sayansi na Teknolojia, suala hili limetiliwa maanani.

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka nijumuishe na wale wote waliozungumza kwa kauli kwamba kwa kweli tunakiri sayansi inaanzia tangu kijana anapozaliwa, anaanza kupambana na sayansi. Kama wasemaji waliotangulia walivyosema, nadhani ni Mheshimiwa Mbunge mwanafunzi wangu wa Mbozi yeye amesema kwamba palipo na sayansi hakuna majungu. Ni kweli kabisa kwamba ukiwa na sayansi kubwa huna nafasi ya majungu wala huna nafasi ya kuteta kwa sababu umezidiwa na mambo ya kisayansi. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sayansi hii ambayo tumeitafakari katika Sera ya Sayansi na Teknolojia tunaihuisha tena, tunarudia tena tuwe na sera ambayo ni muafaka ambayo inafuatana na hali yenyewe ilivyo sasa hivi. Katika mipango yetu, mnaita kabambe au kamambe, tumezingatia, tumeangalia matendo gani yafanyike tangu Elimu ya Msingi mpaka Chuo Kikuu na tumetenga fedha. Kutenga fedha sio kwamba fedha umeipata unatenga kabisa kwamba vitendo hivi vitahitaji kugharamiwa kiasi fulani, si chini ya US$ milioni 68 ambayo tumetenga katika miaka 15 ihusishwe katika uendelezaji wa sayansi na teknolojia. Kwa hiyo, suala hili tumelizingatia kwa makini. Namshukuru Mheshimiwa Profesa Sarungi kwa mawazo yake na tutayazingatia katika utekelezaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, waliozungumza kwa maneno, ninao hapa ambao napenda kuwashukuru kabisa, nao ni Mheshimiwa Dr. Mwita Haji Mwita. Namshukuru sana yeye kwa niaba ya Kamati ametoa mawazo na ushauri mzuri tumeuzingatia. Mheshimiwa Benedicto Mutungurehi, ametoa ushauri mzuri kabisa ambao tumeuzingatia katika maazimio yote mawili kwenye Azimio la *Mbeya Institute of Technology* na hasa lile Azimio la Matumizi ya Vifaa na Vyombo vya Nyuklia. *(Makofi)*

Wengine ni Mheshimiwa Simpasa, Mheshimiwa Makwetta, Mheshimiwa Dr. Shija, Mheshimiwa Mpesya na Mheshimiwa Mutungirehi tena. Tunawashukuru sana kwa yote ambayo wameyazungumzia. Pamoja na ndugu yangu Mjaka Ali ambaye yeye vile vile amejikita katika sehemu zote mbili, Azimio la kwanza na Azimio la pili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka niende haraka haraka ili niweze kuwapatia majibu wote ambao wamezungumza kwa sababu yote yamezungumzwa vizuri sana. Kwanza, ni kuhusu mabadiliko ambayo yanapendekezwa. Nashukuru sana Mheshimiwa Mutungirehi aliweka *caution* kidogo kwamba anafahamu utaratibu wa kuridhia Maazimio ya namna hii hasa inapokuja *subsidiary legislation* ambapo Bunge mnakasimu madaraka yenu kwangu. Kwa hiyo, masuala ya kubadilisha hapa hayapo kwa utaratibu ambao tumejiwekea ila tunakubali kwamba ushauri huo mlionipatia nitauzingatia. Nashukuru sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mfano *governed board,* hiyo sio tatizo mimi mwenyewe niliona kwamba linafaa lakini nikaongeza vile vile kwamba hakuna haja kusema *Academic Committee* inakuwa ni *Academic Board* ile hadhi iwe kubwa ya ki-*institute, institute*, hiyo vile vile nimekubaliana nayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu sayansi, Mheshimiwa Mutungirehi ambaye naweza kumwita mwanafunzi wangu, ninamkaribisha tu kwa ruksa yako baada ya Bunge maana yake hapa huna muda huo, lakini kwa sababu mara nyingi Mutungerehi huwa tunazungumza naye tuingie kwenye *epistemology* na *history of science* lakini hapa hatutaki kuwapotezea muda. Ningependa kumwelekeza kwenye *encyclopedia wikipedia, free encyclopidea* ambayo inaweka *definition* halisi ya sayansi ni nini.Vile vile, akiangalia mtiririko wa historia ya sayansi, tulikotoka *from cosmology,* falsafa, sayansi yote hiyo inaingiza mambo yote *natural sciences and social sciences.*

Lakini leo mimi sio wakati wangu hapa wa kuweka *dissertation* kuhusu *science* ni kitu gani, itawapotezea muda wenu bure tu. Lakini yeye ninamkaribisha, nimeweka *notice* hapa za kumsaidia ndugu Mutungerehi ambazo zitamsaidia sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vile ningependa nimwelekeza hasa wale ambao wanataka kuendelea na Digrii za Falsafa, msome kwa makini sana Joseph Kun *on scientific revolutions* na *history of science,* hayo yatawasaidia sana. Kama unasoma historia na kama unasoma *physical science* lazima ukisome kitabu hicho ili uelewe kujadili kisayansi, kifalsafa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mantiki hiyo, Chuo chetu cha Mbeya ili kiwe Chuo ambacho kweli ni Chuo Kikuu lazima kiwe na fani zote. Hatutoi *degree* za fani za sayansi ya jamii lakini kwenye fani za sayansi na teknolojia ni muhimu ukafahamu mambo ya fani za sayansi za jamii. Wewe ni fundi hujui kuandika *project* yako, matendo yako ya kiufundi utayatekeleza namna gani? Kwa hiyo, *project write-up, project evaluation* lazima uifanye. Hiyo inafanywa katika masomo ya *entrepreneurship* na fundi hasa anapaswa ajue ujasiriamali ni kitu gani. Mafundi ambao hawajui ujasiriamali hawatakuwa na faida yoyote katika nchi hii, ni muhimu ukafahamu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Dr. Shija amesaidia vile vile. Huwezi kuelewa ufundi kama hujui lugha hizi mbili kuu. Lugha ya kwanza ni lugha hii tunayoizungumzia hii Kiswahili au Kiingereza, maana yake ndio sasa chombo chako cha kujieleza au kupokea maelezo. Kwa hiyo, ni muhimu lugha ikafundishwa. Lugha ya pili ni hesabu. Hesabu ni lugha ya mkato ambayo inaeleza *relationships,* ndio maana yake. Lugha hii ndefu unazungumza kwa maneno mengi, unaweka *relationships* kwa maneno mengi, hii unaweka *relationships* katika *formula*, ni hesabu. Hizo lugha mbili ni muhimu ukazifahamu, ndizo zinafundishwa. Kwa hiyo, haya mambo hayakaniki katika utaalam wa ufundishaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya hapo, ninakwenda kwa Mheshimiwa Makwetta. Ninakubaliana naye, amenikumbusha utaratibu wa siku nyingi tangu Waroma labda tangu Wakigiriki walilitambua kwenye sayansi ya vita wamejipanga vizuri watu 11, watu 25, watu 100 inakamilika kampuni, siyo? Halikadhalika katika kufundisha tumejua hata Wanyamwezi na Wasukuma hata Wasambaa na Wazigua wanafahamu akina mama hasa wanapofundisha namna ya kupika na Wazaramo wanajua unaweza kuhutubia watu 100 wakaelewa juu ya kupika mboga za majani au kisamvu; watu 50 wanaelewa zaidi, watu 16 wanaelewa mno, siyo? Basi wa-*span* hiyo katika mambo ya ufundi. Inajulikana kwamba fundi mahiri kabisa lazima umwekee watu wasiopungua 25 hata 30, yeye ameongeza mpaka 45. Lakini kwa utaratibu wa sasa ni kati ya 25 na 30 na ndio sababu madarasa ya ufundi hayazidi watu 30 kwa sababu *span of control* ya watu wako lazima uwe karibu nao na lile *desk* la kupigia randa huwa ni watu wanane tu na *laboratory* hivyo hivyo isizidi 16, maana yake jicho lako linaweza kuona na kuweza kuwadhibiti sio zaidi ya watu 16.

Ndio maana hiyo kwamba fundi mmoja yaani mahiri, anafuatiwa na fundi wa kati. Hiyo ndiyo *foremen* anakuwa na mafundi wengine sasa ambao ni 25. *A degree or*

*professional* mmoja au *Doctor* mmoja, manesi 25, 30 na wale mafundi wengine zaidi, ndio utaratibu ulivyo, tunakubali na huu hautaondolewa. Tunataka katika Vyuo vyetu hivi vya Dar es Salaam *(DIT)* na Mbeya wale mafundi wa aina hiyo wasiondoke wabaki pale ili kama wanavyofanya kazi pamoja katika hali ya kawaida katika kazi na katika mafunzo yao wajifunze hivyo hivyo.

Wajifunze kushirikiana tangu katika mafunzo yao kama mahospitali Madaktari wanafundishwa pamoja na manesi na wengine ili waweze kuelewana tangu katika mafunzo yao. Kwa hiyo, hili la Mheshimiwa Makwetta tunakubali.

Mheshimiwa Naibu Spika, *degree manic,* ni kweli lakini haya ni mambo ya kisiasa, lakini wananchi wanataka *degree.* Sisi viongozi kazi yetu ni kuongoza na kuratibu vizuri hizo *degree* na *degree* kweli katika nchi yetu bado ni chache zinahitajika hatujazamia kwamba sasa tumelowa na kuzama katika digrii tuna uhaba wa digrii ni muhimu zikiwepo. La msingi ni kwamba kama alivyosema Profesa Sarungi ni kuongeza mafunzo ya kada za katikati na kada za kawaida ziweze kulingana na uwiano ule ambao Mheshimiwa Makwetta alikuwa ametushauri. Kwa hiyo *degree manic* hiyo itakuwa imepungua.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda hapa kuchukua nafasi hii kusema kwamba Chuo hiki kitaanzishwa sio kwa utaratibu wa sheria tuliyopitisha, Sheria ya Vyuo Vikuu, Chuo hiki kinapitishwa kwa sheria ambayo nimeitaja ya ufundi, *enacted* ambayo *degree* zake ni za kiufundi, za kiutendaji, *technological degree.*

Mheshimiwa Naibu Spika, bahati nzuri na mimi ningeomba bahati hii muipate Waheshimiwa Wabunge vile vile muende hapa karibu panaitwa Kigali hapo Rwanda kina kitu kinaitwa *KIST (The Kigali Institute Science and Technology)* ukifika pale sio mchezo bwana! Wala hatudharau kwamba hiyo ni kaptura pale ni *institute of science and technology.* Kutengeneza kitu kama hicho unahitaji muda ili upate kitu cha thamani ya juu.

Leo kweli Serikali yetu ni bahati nzuri imewaomba ushauri tukapata ushauri kutoka kwenye Chuo Kikuu kwamba kwanza tuimarishe tupate Chuo ambacho kina hadhi ya kutosha katika maeneo machache ndio tofauti ya *University* na *institute. Institute* ina maeneo machache, *University* inachukua *Universal,* maeneo mengi, ndio tofauti hiyo tu. Ningeomba Wabunge tukipata nafasi tuende pale, Profesa Lwakabamba ambaye ametoka Chuo Kikuu chetu cha Dar es Salaam ndio *lecture* wa pale na anakuja pole pole.

Mheshimiwa Naibu Spika, unakwenda sasa Marekani kuna Vyuo Vikuu vya aina hii viwili tu na kila mtu hawezi kuingia katika Vyuo hivyo viwili. *Massachusetts Institute of Technology* sio kila mtu anaingia *A, A, A* na *proven A* ndio unakwenda pale. Unaweza kuingia *Harvard* lakini *Massachusetts Institute of Technology* huingii na kingine *CAIT (Calfornia Institutite of Technology)* ambao ndio wanao wataalam kwenda mwezini. Kwa hiyo, majina haya yasitubabaishe kwamba moja ni kaptura, ingine ni suruali, hata kidogo! Hii ni hatua kubwa mno wananchi wa Tanzania wanaipata katika sehemu yetu inayoitwa Mbeya maana Chuo hiki kilichoko Mbeya ni Chuo cha Taifa zima. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naona anapenda nisiendelee kujibu hoja zenu, anasema muda umekwisha. Lakini hili lilikuwa ni muhimu kuliweka wazi wananchi wa Mbeya wasione kwamba ni wanyonge, ni hatua muhimu sana kwamba tunaimarisha maeneo machache kwanza yanakuwa imara na sio dhaifu na mmeona katika s*taff development* kwamba tunafundisha watu wengi wasome wapate *Ph.D*, wapate sifa za kufundisha Chuo Kikuu kwa sababu wasipopata sifa hizo huwezi kuandikishwa kuwa Chuo Kikuu.

Chuo Kikuu sio majengo, nakubali kabisa. Popote pale unaweza kupata Chuo Kikuu majengo hafifu zaidi kuzidi hata ya Chuo cha Ufundi cha Mbeya ila cha maana una Wakufunzi wangapi wenye sifa za kufundisha kwenye Chuo Kikuu, una vifaa na vyombo kiasi gani, hayo ndio muhimu ambayo mmetutuma tufanye. Mtoto huanza kwa kupiga hatua kwanza anatambaa, halafu anyanyuka anatembea, sasa sisi tumeanza kunyanyuka tutembee, tutatembea na tutafika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nadhani mengine yote nimeyajumuisha, niende kwenye hili la nyuklia. La *MIST*, nashukuru tu kwamba mmetuunga mkono. La nyuklia napenda kuwatoa wasiwasi na wengi kweli mlikuwa hamna wasiwasi kwa sababu suala hili tumelijadili sana tulipoleta Maazimo yale mengine matano. Ni muhimu kabisa Tanzania ikawa sehemu ya dunia yote. Hatuwezi kushinda kwa kujitenga. Hata ile mifano ya kusema Iraq na wapi hawa wangekuwemo wangeridhia au kutoridhia Mataifa makubwa yangewaingilia tu wala sio kwamba umepata sasa kinga kwa sababu wewe hukuweka saini. Ingia mle ndani ushughulike nao.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kutoa shukrani hapa leo kwa mwana wa Afrika na mwana wa Dunia anayeitwa Koffi Annan, Katibu Mkuu wa Umoja wa Mataifa ambaye anataka kuleta makubwa sana katika Umoja wa Mataifa na hasa katika *Security Council* ambayo ilikuwa imejiweka vibaya sana katika mtindo na mfumo wa kibepari na wa kiimla sasa anataka ubadilike. Tuwemo humo ndani na tuwemo katika mashirika mbalimbali, sauti yetu na kauli yetu kama alivyosema Mutungirehi itasikilizwa ukiwa nje sauti yako ni batili, husikilizwi! Ingia mle ndani, *join them* wakusikilize, piga kelele humo ndani utakuwa sasa wewe sio haramu ni halali. Ndio maana napenda kuwaomba ndugu zangu mwondoe wasiwasi na wala hatutapata shida kama nilivyoeleza tutapata misaada mikubwa, ajali ikitokea tunaposafirisha vifaa hivi ndani ya nchi yetu, uwezo hatuna ndio sababu yake kwamba lazima tujiunge na wenzetu tupate uwezo huo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa maelezo haya, kwa unyenyekevu na heshima kubwa, naomba sasa kutoa hoja kwamba Maazimio yote mawili ambayo nimetoa mbele ya Bunge lako Tukufu yaweze kuridhiwa na Bunge lako Tukufu.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Naomba radhi sana. Mheshimiwa Waziri najua huo ni uwanja wako, ungekuwa na muda mrefu ungetujibu vizuri zaidi, lakini tuna Azimio moja lingine linatufuata na wasemaji ni wengi. Sasa baada ya hoja hizo mbili kutolewa, nitawahoji moja moja.

*Azimio la Kuridhia Chuo cha Ufundi Mbeya kuwa Taasisi ya Sayansina na Teknolojia Inayojitegemea liliridhiwa na Bunge*

**Azimio la Kuridhia Makubaliano ya Nchi Wanachama wa *Southern and Eastern Africa Mineral Centre (SEAMIC)* Kuhusu Mkataba wa Wanahisa wa *SEAMIC***

**NAIBU WAZIRI WIZARA YA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Nishati na Madini naomba kuchukua nafasi hii kuwasilisha Azimio la Bunge la Kuridhia Makubaliano ya Nchi Wanachama wa Kusini na Afrika Mashariki au wa *Southern and Eastern Africa Minerals Centre* kuhusu Mkataba wa Uanahisa, kwa ufupi Chuo hiki au Kituo hiki unaweza ukasema kama *SEAMIC*.

Mheshimiwa Naibu Spika, kabla ya kutoa maelezo mafupi kuhusu Azimio lililo mbele ya Bunge lako Tukufu, ningependa kutoa shukrani zangu za dhati kwa Mheshimiwa William Shellukindo, Mwenyekiti wa Kamati ya Biashara na Uwekezaji pamoja na Wajumbe wote wa Kamati hiyo kwa jinsi walivyolichambua Azimio na Mkataba husika kwa makini kabisa. *(Makofi)*

Ninamshukuru pia Mheshimiwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali na wataalam wake kwa mchango wake katika kuboresha Azimio hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kituo hiki ambacho kwa kifupi nakiita *SEAMIC* kipo Kunduchi Dar es Salaam. Kituo hiki kinamilikiwa kwa pamoja na nchi zifuatazo za Angola, Ethiopia, Msumbiji, Tanzania, Uganda na Visiwa vya Comoro. Nchi nyingine ambazo zimeonyesha nia ya kujiunga na *SEAMIC* ni Kenya, Afrika Kusini, Zimbabwe, Rwanda na Burundi. *(Makofi)*

Kituo kilianzishwa mwaka 1977 ili kutekeleza Mpango wa Maendeleo wa Afrika uliopewa jina la Mji wa Lagosi (*Lagos Plan of Action)* chini ya usimamizi wa Taasisi ya Umoja wa Mataifa au *United Nations Economical Mission for Africa.*

Mheshimiwa Naibu Spika, lengo kuu la kuanzishwa Kituo hiki ni kuunganisha nguvu za nchi wanachama katika kuendeleza Sekta za Madini za nchi hizo ili ziweze kuleta maendeleo kwa wananchi wao. Mambo yaliyotekelezwa na Kituo cha *SEAMIC*, tangu Kituo hicho kianzishwe kama nilivyoeleza awali kwa Mkataba wa 1977 Kituo hicho kimekuwa kikitekeleza majukumu yafuatayo:-

Kuendesha mafunzo kwa wataalam katika nyanja mbalimbali zinazohusu madini ikiwa ni pamoja na uchambuzi wa taarifa za kijiofizikia kwa kutumia *computer* na uchoraji wa ramani, kufanya utafiti wa kuendeleza madini yanayotumika viwandani

yaani *Industrial Minerals,* kufanya uchunguzi wa miamba kwa kutumia Maabara ya kisasa iliyopo Kituoni hapo kujua viwango vya madini ndani ya miamba na njia bora za uzalishaji wa bidhaa hizo, kutambua na kuyatathmini madini ya vito na kutoa mafunzo ya uchambuzi wa madini hasa kwa wachimbaji wadogowadogo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu uendeshaji wa Kituo, Kituo hiki kimekuwa kikiendeshwa kwa michango ya wanachama ambapo kila nchi huchangia Dola za Marekani 62,000 kwa mwaka. Hata hivyo, baadhi ya nchi zimekuwa hazichangii na nyingine zimekuwa zikichelewa katika kutoa michango yao na baadhi hutoa sehemu tu ya michango hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kwamba Tanzania imetoa michango yake kikamilifu kama mwenyeji wa Kituo hicho. *(Makofi)*

Kwa upande mwingine, Kituo kimekuwa kikipata misaada mbalimbali kutoka Umoja wa Mataifa na Taasisi zake kama nilivyosema mwanzo *ECA*, *UNIDO*, Umoja wa Nchi za Ulaya na baadhi ya nchi zikiwemo Ujerumani, Canada na Ubelgiji na kwa kweli ningependa kuchukua nafasi hii kuzishukuru nchi hizo rafiki kwa michango kwa Kituo hicho.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu chimbuko la kuanzishwa kwa Kituo hiki, kama nilivyosema awali, utajiri mkubwa wa madini uliopo kwenye nchi za Afrika ambao unahitaji kuendelezwa ambao haujaendelezwa ipasavyo imefanya madini hayo yasitumike kikamilifu katika kuleta maendeleo kwa wananchi wake. Hivyo basi, nchi husika ziliona ni muhimu kuanzisha Kituo hiki ili kuendeleza sekta hii muhimu ya madini katika kuleta maendeleo ya nchi zetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, juu ya Mkataba wa nchi wananchama. Baada ya mfumo wa kundesha uchumi katika nchi zetu kubadilika na kutoa kipaumbele katika sekta binafsi na ili kutekeleza uendeshaji wa Kituo mwaka 2002, nchi wananchama wa Kituo hiki zilikubaliana kuingia Mkataba wa Wanahisa, yaani *Shareholders Agreement.*

Mkataba huu una vipengele muhimu vifuatavyo: Kwanza, michango yote ya Serikali kwenye Kituo hicho kuanzia mwaka 2000 itakuwa ni ya hisa za nchi kwenye umiliki wa Kituo. Pili, mchango wa Dola 62,000 kwa mwaka mmoja uliolipwa utakuwa sawa na hisa moja. Tatu, uwezo wa kupiga kura utalingana na wingi wa hisa za wananchama. Nne, wadau wengine wa Sekta Binafsi, yaani Watu Binafsi na Makampuni wamepewa nafasiya kuwa na hisa kwenye Kituo hicho. Tano, uwezo wa kifedha wa Kituo unategemewa kuongezeka na Kituo kutekeleza kwa urahisi mikakati ya kujiendesha. Sita, kila nchi mwanachama itakuwa na haki ya kuwa na hisa na pia kuwa na haki ya kunufaika na huduma zitolewazo na Kituo hicho.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu matokeo ya utekelezaji, Mwelekeo wa sasa unatoa kipaumbele kwa Sekta Binafsi kuwa na hisa kwenye Kituo hiki. Mategemeo makubwa ni kukiwezesha Chuo kuongeza uwezo wake wa kujiendesha na kutoa huduma za kitaalam ipasavyo.

Aidha, kwa kutumia hisa, Kituo kinategemea kujipatia mapato, Kituo pia kinategemea kwamba kitavutia nchi nyingine kujiunga nacho na pia kitavutia misaada zaidi kutoka kwa wafadhili mbalimbali.

Mheshimiwa Naibu Spika, juu ya Ratiba ya Utekelezaji, Utekelezwaji wa yaliyomo kwenye Mkataba huu utaanza mara tu baada ya nchi kuridhia Mkataba huu, nchi wanachama ziliombwa kuridhia Mkataba huu tangu mwishoni mwa mwaka 2002 na hadi sasa Msumbiji imesharidhia na nchi nyingine karibu zinatarajia kuridhia. Ni vyema basi, Tanzania kama nchi mwenyeji au *host country* iridhie Mkataba huu.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya Serikali na Kamati ya Bunge ya Biashara na Uwekezaji kuridhika na Mkataba huu, sasa naomba kuwasilisha pendekezo lifuatalo ili Bunge liliridhie kuanzishwa kwa Mkataba wa wanahisa wa *SEAMIC*.

KWA KUWA tangu kuanzishwa kwa Shirika la *SEAMIC* mwaka 1977 kumekuwepo na makubaliano mbalimbali kati ya nchi wanachama wa Shirika hilo;

NA KWA KUWA mojawapo ya makubaliano hayo ni yale yanayohusu utaratibu wa umilikaji wa Shirika la *SEAMIC* kwa njia ya hisa.

NA KWA KUWA ni nia ya nchi wanachama wa *SEAMIC* ni kuweka misingi ya kisheria, yaani *Legal Framework* itakayosaidia katika kuruhusu ushiriki wa Sekta Binafsi na hivyo kuboresha huduma mbalimbali zinazotolewa na Shirika hili kwa kufuata sheria, kanuni na taratibu kama zilivyoainishwa katika makubaliano;

NA KWA KUWA Serikali za nchi wanachama wa *SEAMIC* zimeazimia kutekeleza matakwa ya kifungu cha 10 cha Mkataba ulioanzishwa, yaani *Agreement Establishing the Centre;*

NA KWA KUWA utaratibu wa umilikaji wa Shirika hilo hadi sasa aumekuwa ni wa kwa kwa utaratibu wa michango wa kila mwaka wa Dola 62,000 toka kila nchi mwanachama ambayo haikidhi mahitaji ya kifedha ya kuendesha Shirika hilo;

NA KWA KUWA matokeo ya kuridhiwa kwa Mkataba huu ni kuruhusu Sekta Binafsi kujiunga na Shirika kwa kuwa na hisa na hivyo kuongeza uwezo wa kifedha wa Shirika hilo;

KWA HIYO BASI, kwa kuzingatia umuhimu wa manufaa ya Mkataba huu na kwa mujibu wa ibara ya 63, sehemu ya 3(a) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania mwaka 1977, Bunge hili katika Mkutano wake wa 19 sasa linaazimia Tanzania kuridhia makubaliano ya nchi wanachama wa *SEAMIC* kuhusu Mkataba wa wanahisa wa mwaka 2002, yaani *The SEAMIC Shareholders Agreement 2002.*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**WAZIRI WA USHIRIKA NA MASOKO:** Mheshimia Naibu Spika, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*
*(Hapa umeme ulikatika na kuwaka baada ya muda mfupi)*

**MHE. HERBERT J. MNTANGI - (K.n.y MWENYEKITI WA KAMATI YA UWEKEZAJI NA BIASHARA):** Mheshimiwa Naibu Spika, yafuatayo ni maoni ya Uwekezaji na Biashara kuhusu Azimio la Bunge la Kuridhia Makubaliano ya Nchi Wanachama wa *Southern and Eastern African Mineral Centre (SEAMIC),* kuhusu Mkataba wa Wanahisa wa *SEAMIC*.

Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote, napenda kukushukuru kwa kunipa nafasi hii ili niweze kuwasilisha maoni ya Kamati kuhusu Azimio la Bunge la Kuridhia Makubaliano ya Nchi Wanachama wa *The Southern East African Mineral Centre (SEAMIC).*

Mheshimiwa Naibu Spika, kabla ya kutekeleza masharti ya kanuni Na.43 fungu dogo la 5(b) ya kanuni za Bunge la mwaka 2004, napenda kuchukua nafasi hii kumshukuru Mheshimiwa William Shellukindo, Mbunge na Mwenyekiti wa Kamati ya Uwekezaji na Biashara na Wajumbe wa Kamati hii kwa kunipa heshima ya kusimama mbele ya Bunge lako Tukufu siku hii ya leo kutoa maoni ya Kamati kwa niaba yao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuwatambua Wajumbe wafuatao wa Kamati husika. Mheshimiwa William H. Shellukindo - Mwenyekiti, Mheshimiwa Salome J. Mbatia - Makamu Mwenyekiti, Mheshimiwa Mbaruku Kassim Mwandoro - Mjumbe, Mheshimiwa Dr. Aaron Chiduo - Mjumbe, Mheshimiwa Dr. James Wanyancha - Mjumbe, Mheshimiwa Dr. Lucy S. Nkya - Mjumbe, Mheshimiwa Freeman Mbowe - Mjumbe, Mheshimiwa Hamis Awesu Aboud - Mjumbe, Mheshimiwa Mohamed Abdulaziz - Mjumbe, Mheshimiwa Christopher Wegga - Mjumbe na Mheshimiwa Abou Kiwanga - Mjumbe. *(Makofi)*

Wengine ni Mheshimiwa Margareth J. Bwana - Mjumbe, Mheshimiwa Nazir Mustafa Karamagi - Mjumbe, Mheshimiwa Sthephen Masaba Kazi - Mjumbe, Mheshimiwa Aisha P. Magina - Mjumbe, Mheshimiwa Mohamed Ali Saidi - Mjumbe, Mheshimiwa Semindu Pawa - Mjumbe, Mheshimiwa Sumri S. Mohamed - Mjumbe, Mheshimiwa Ismail Ywvata - Mjumbe, Mheshimiwa Ali Machano Musa - Mjumbe, Mheshimiwa Fatma Saidi Ali Mchumo - Mjumbe, Mheshimiwa Omar E. Chubi - Mjumbe na mimi mwenyewe Hertbert S. Mntangi - Mjumbe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mujibu wa kanuni hiyo ya 45 fungu la Nne, toleo la mwaka 2004, Kamati ya Uwekezaji na Biashara ilikutana Jumanne tarehe 01Februari, 2005 na kuchambua Azimio la Bunge la Kuridhia Makubaliano ya nchi wanachama wa *Southern and Eastern African Mineral Centre* kuhusu Mkataba wa Wanahisa wa *SEAMIC* na kutoa maoni kama ifuatavyo:

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati ya Uwekezaji na Biashara inaunga mkono hoja ya Mheshimiwa Waziri wa Nishati na Madini ya kuliomba Bunge lako Tukufu Kuridhia Azimio hilo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati imeafiki hoja hii kwa misingi ifuatayo:-

Nchi yetu imejaaliwa kuwa na raslimali nyingi za madini. Hata hivyo mchango wa raslimali hii katika pato la Taifa bado ni mdogo sana, hivyo kuimarishwa kwa Kituo hiki, kutatoa fursa kwa Tanzania kunufaika na raslimali hiyo kwa kubadilishana uzoefu, teknolojia na mafunzo hasa na nchi wanahisa wa Kituo hicho pamoja na kunufaika na utafiti katika Sekta ya Madini kwa ujumla.

Mheshimiwa Naibu Spika, Tanzania pia imepata heshima ya kuwa Makao Makuu

*(Hapa umeme ulikatika na kuwaka baada ya muda mfupi)*

**MHE. HERBERT J. MNTANGI - (k.n.y MWENYEKITI WA KAMATI YA UWEKEZAJI NA BIASHARA):** Mheshimiwa Naibu Spika, samahani sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, Tanzania pia imepata heshima ya kuwa Makao Makuu ya *SEAMIC* huko Kunduchi Jijini Dar es Salaam. Hii itasaidia nchi kutambuliwa zaidi kikanda na kimataifa. Hali hii inatoa changamoto kwetu kuimarisha sekta hii ili iweze kuchangia ipasavyo juhudi zetu za kuinua uchumi na kupiga vita umaskini.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati pia imefurahi kuona kuwa Azimio hili linatambua mchango wa Sekta Binafsi katika sekta hii ambayo ina nafasi kubwa katika maendeleo ya uchumi wa nchi yetu, hivyo ni wazi kuwa ushiriki wa Sekta Binafsi utaongeza mtaji wa kuendesha *SEAMIC* na pia kuingiza teknolojia ya kisasa na kuendesha Kituo hiki kwa ufanisi zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho, naomba kuchukua fursa hii kumpongeza Mheshimiwa Waziri Daniel Yona - Mbunge na Waziri wa Nishati na Madini, Mheshimiwa Naibu Waziri wake, Mheshimiwa Ibrahim Msabaha - Mbunge, kwa ushirikiano na ufafanuzi walioipa Kamati yangu wakati inajadili Azimio hili.

Aidha nawashukuru Watendaji wa Wizara hiyo kwa kushirikiana kwa karibu na Kamati wakati wa utekelezaji wa jukumu hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, naunga mkono Azimio hili na ninaomba kuwasilisha. *(Makofi)*

**MHE. ISAACK M. CHEYO - MSEMAJI WA UPINZANI KWA WIZARA YA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kitendo cha umeme kukatika kinanikumbusha mwaka 1997 wakati Bunge liko *in session* Waziri wa Nishati na yeye aliyekuwa anazungumza kama leo, sasa kama hii ni kwa sababu *net work solution* au ama kitu gani ama teknolojia mpya, hatuelewi! *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Kituo hiki tunaomba Waheshimiwa Wabunge turidhie. Nilitaka tu niseme kwa mara ya kwanza kwamba kumetolewa Azimio ambalo limeletwa ndani ya Bunge kwa haraka sana kuliko maazimio mengine yote. Azimio ambalo limepita ni la mwaka 1980 na ni kawaida hili Bunge kuridhia Mikataba ya miaka 10, 20, 40 iliyopita. Kwa hili, natumaini Serikali imeona umuhimu wake ndiyo maana ikalileta liweze kuridhiwa na Waheshimiwa Wabunge tangu wakati ule ambao waliweza kutia saini mwaka 2003. Natumaini kwa *speed* hii na *spirit* hiyo hiyo, Kambi ya Upinzani hatuoni sababu yoyote ile ya kutounga mkono hoja iliyoko mbele yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuzingatia utajiri wa nchi yetu kwenye Sekta ya Madini, tunadhani hili ni jambo zuri kuendeleza sekta hii muhimu katika ukuaji wa uchumi wa nchi yetu. Hivyo basi, hatuna budi kwa manufaa ya nchi kukubali kuridhia Azimio hili kwa kuzingatia kuwa Dar es Salaam itakuwa ndiyo Ofisi Kuu kwa wanahisa wa madini kwa nchi za Mashariki na Kusini mwa Afrika.

Mheshimiwa Naibu Spika, *article (1) sub section (2)* vipengele vingi vilivyomo ni muhimu kwa maendeleo ya Sekta nzima ya Madini kwa kuwa nchi yetu inakosa vifaa na taaluma ya kisasa. Kwa hiyo, kukiwa na *collective efforts* na watu wengine mnabadilishana teknolojia, mnabadilishana elimu na vitu vingine, tunaona itasaidia sana katika utafiti wa maeneo na *exploration* na uanzishaji pia na upimaji wa madini.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kiwango kikubwa kuridhiwa kwa Mkataba huu kutasaidia kurekebisha sheria za madini zilizopitwa na wakati hapa kwa kulinganisha na Mataifa mengine ambayo ni wanahisa wa Kituo hiki. Hii katika *article* (1) fasili ya 2 (f) inazungumzia: *"To promote indigineous mineral based industrialization."* Tunaishauri Serikali ihakikishe uanzishwaji wa Kituo hiki ambacho kinatakiwa kujengwa hapa Tanzania. Kipengele hiki kinaweza kuwa ndiyo mkombozi kwa wazawa wanaojishughulisha katika Sekta hii ya Madini ambao mpaka sasa bado hawajanufaika na utajiri wa madini waliyopewa na Mwenyezi Mungu, badala yake Makampuni makubwa toka nje ya nchi, yanahodhi hata maeneo yatumiwayo na wazawa katika kupata riziki zao za kila siku. Mifano ni mingi na inaeleweka katika ngazi zote za Serikali.

Kitu ambacho hakijaeleweka kwa Watanzania wengi ni kuwa madini ya *tanzanite* na almasi wazawa hawawezi kuyauza popote pale isipokuwa kwa kupitia mtu mwingine kama *AFGEM* au *DE BEERS* kwa ajili ya almasi Makampuni ambayo yamehodhi biashara ya madini hayo hapa nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala hili ni hatari kwa maisha ya jamii inayotegemea madini, kama vile vijana wetu wanaochimba pale Mwadui kila siku wanaswagwa, wanafukuzwa, wanakwenda wapi! Lakini kama wangeweza kuyakusanya madini wangeweza kuyauza *else where.* Lakini kuna tatizo kubwa ambalo lipo, natumaini katika kubadilishana uzoefu na mawazo, tunaamini kabisa sasa ni nafasi nzuri kwa watu wengine wadogo wadogo kuweza kuyauza madini yao.

Mheshimiwa Naibu Spika, sisi tunaamini kwamba Kituo hiki kwa sababu kinahusisha nchi nyingi, kinasaidia pia katika kuwa na sauti ya pamoja ya watu wote ambao ni wanahisa wa machimbo. Mnapokuwa na sauti ya pamoja mna uwezo wa kuweza kufanya *marketing*, mna uwezo wa kuweza kufanya *process* na kuweza kuhakikisha kwamba madini yenu mnayauza katika hali ambayo ni *processed* ikapata *added value*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tungewashauri sasa Waheshimiwa Wabunge, bila kusita muiunge mkono Serikali na Azimio hili muweze kupitisha Azimio hili. Ahsanteni sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Wachangiaji wakuu watatu wamemaliza. Sasa ninao wachangiaji watatu hapa, Mheshimiwa Mbaruku Mwandoro, Mheshimiwa Talala Mbise na Mheshimiwa Semindu Pawa. Sasa Mheshimiwa Mbaruk Mwandoro ataanza.

**MHE. MBARUK K. MWANDORO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ili nichangie juu ya Kuridhia Kituo hiki cha *SEAMIC*.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kituo hiki cha *SEAMIC* ni Kituo muhimu sana. Ni Kituo ambacho kinafanya kazi kubwa kama vile ambavyo ameeleza Naibu Waziri na wasemaji waliopita. Kwa bahati mbaya, Kituo hiki hakifahamiki kwa wengi, hata sisi watu tuliokuwa katika Kamati ya Uwekezaji na Biashara, wengi wetu tulikuwa hatukifahamu. Lakini Kituo hiki, kinafanya kazi muhimu ya kuchambua madini, kazi muhimu ya kufundisha, kazi muhimu ya kutoa ushauri kwa nchi husika. Hiki Kituo ni muhimu sana kwetu sasa hivi, tukizingatia mipango yetu tuliyonayo kama vile *MKUKUTA*, kitaweza kusaidia sana wananchi wetu wadogo wadogo kuweza kuingia katika biashara ya madini na kutumia rasilimali madini kwa faida kubwa zaidi kuliko ambavyo imekuwa hivi sasa.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni bahati mbaya kwamba Kituo hiki kinashindwa kutekeleza majukumu ipasavyo, kina vyombo na vifaa vingi sana, lakini kutokana na hali hafifu ya kutochangiwa vya kutosha, Kituo hiki hakiwezi kufanya kazi yake inavyotakiwa. Mimi nashukuru na kufurahi sana kwamba Serikali yetu imeona umuhimu wa Kituo hiki na Serikali yetu imekuwa ikitoa mchango kamili.

Hiki Kituo kama nilivyosema, kinahitaji msaada mkubwa sana. Kazi zake kusema kweli zitaweza kusaidia sana nchi zetu hizi kuendeleza Sekta yetu ya Madini. Bahati mbaya hakifahamiki siyo ndani ya nchi hii, lakini hakifahamiki sehemu nyingi duniani. Kwa hiyo, kinahitaji msaada mkubwa wa fedha ili kiweze kufahamika zaidi ili kiweze kutumika vizuri zaidi. *(Makofi)*

Sasa mimi nashukuru kwamba nchi yetu ambayo ndiyo *host country* yaani mwenyeji wa Kituo hicho zaidi ya kufanya jitihada ya kuridhia, zaidi ya kulipa michango yake, nafikiri Serikali yetu iwe na kazi kubwa sana ya kujaribu kushawishi wananchi wengine au nchi nyingine wanachama kuweza kushiriki kikamilifu kwa kulipia michango

yao kwa Kituo hicho ipasavyo. Vile vile, kuendelea kuwaomba wahisani mbalimbali na Taasisi mbalimbali za kidunia, umoja wa Kimataifa na wengineo kuweza kusaidia ili Taasisi hii iweze kuendelea katika misingi iliyotajwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Taasisi hii ni Taasisi muhimu sana na hasa tukizingatia mipango yetu tuliyonayo sasa hivi ya ukombozi ya uendelezi wa uchumi wa wananchi wadogowadogo. Kwa hiyo, mimi napendekeza kwamba Bunge lako Tukufu liridhie kujiunga na Taasisi hii na kulipa haraka iwezekanavyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge tuna tatizo la umeme, lakini msiwe na wasiwasi, kama mnavyojua kuna jenereta la akiba. Unapokatika wa *TANESCO* unachukua muda kidogo ile jenereta ya kwetu kupata nguvu kuweza kuwasha. Sasa unapokuja wa *TANESCO* ule unakuja *automatic*, kwa hiyo kipindi kinakuwa kifupi zaidi. Hata kama ungekula mayai usingeruhusiwa kuendelea bila hii *microphone* kufanya kazi. Kwa hiyo sasa namwita Mheshimiwa Talala Mbise.

**MHE. TALALA B. MBISE:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ya kuchangia kwenye Azimio hili. Kwanza nampongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri na timu nzima ya Wizara kwa kuleta Azimio hili.

Nami naungana na wenzangu kwamba chombo hiki kwanza kabisa nilipoona *SEAMIC* ilinikumbusha *ESAMI* na ndipo ikanipa motisha ya kweli kweli kwamba siwezi kuacha hii fursa ipite bila kuichangia. Kukichukua chombo hiki *SEAMIC* pamoja na Chuo chetu cha Madini Dodoma pamoja na taaluma ya madini, Chuo Kikuu Dar es Salaam ukivichanganya pamoja ni nguvu kubwa katika uchumi wetu na Sekta ya Madini. Kwa kweli tungekuwa tunaitumia hiyo nguvu, vyombo hivyo vitatu *SEAMIC*, taaluma ya Chuo Kikuu pamoja na Chuo chetu cha Madini hapa Dodoma ingekuwa ni nguvu nzito katika kuendeleza Sekta ya Madini na uchumi wetu hapa Tanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukienda kwenye migodi ya madini hapa nchini, utakuta kwamba walioajiriwa kwenye kazi za utaalam na teknolojia au Maabara ni wageni watupu. Sehemu zote za ngazi za juu katika migodi yetu ya madini hapa nchini, wataalam wa fedha wanaotunza Hazina, taarifa *(information technology),* wanaowasiliana na wateja sehemu za nje, wanaotunza masoko, Bohari, wanaoshughulika na ununuzi, wanaoshughulika na uuzaji ni wao kwa wao kutoka nje, hutakuta Watanzania licha na nguvu zote na rasilimali tunazowekeza katika kuhakikisha watu wetu wana taaluma ya kutosheleza kuwakuza watu wetu katika shughuli hizi. Sisi wananchi tunabaki kuangalia tu, lakini ndani hatuoni.

Mheshimiwa Naibu Spika, ardhi iliyo na hii rasilimali ya madini ni yetu na Mungu ndiye katupa na tunamshukuru kwa kutupa hiyo rasilimali ya ardhi yetu. Tuna kila haki ya kushiriki katika kuifaidi na sioni ni kwa nini sisi tubakie tu kuwa wadogo wadogo na kama tunavyoita kule Arusha kubakia wana Apolo na wenzetu ndio wawe wakubwa tu na kwamba sisi ndio tunaowatunzia tu hiyo kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, moja ya njia ambayo tunaweza kushiriki, ni njia ambayo nakumbuka mwaka 2001, mojawapo ya Kampuni kubwa kutoka mojawapo ya migodi sehemu za Mkoa wa Manyara sitaitaja jina, ilikuja ikasema kwamba ingewekeza kwenye Soko la Hisa, Dar es Salaam ikasema kwamba ingewekeza kwenye hilo Soko ili nasi tupate fursa ya kushiriki katika shughuli za migodi hiyo. Bahati mbaya mpaka leo haijawekeza au nyingine yoyote ya migodi ya madini hakuna ambayo imewekeza katika Soko la Hisa Dar es Salaam.

Nimeona kwenye taarifa za habari kwamba, imewekeza kwenye Soko la Hisa London, Uingereza. Wanaofaidi ni Waingereza na sio sisi walalahoi ambao hiyo rasilimali inatoka kwenye ardhi yetu na ni rasilimali aliyotupa Mwenyezi Mungu. Kwa kweli wale maskini ambao ndio sisi tunaiona ikienda, tunaona uchungu, tunaona machozi yetu yakitiririka, tunaona uchungu kwamba kwa nini sisi tusiweze kuona kwamba tunaweza kushiriki katika kuifaidi hiyo rasilimali? Njia ambayo ilikuwepo ya waziwazi ni hiyo njia ya kupitia uwekezaji katika Soko la Hisa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pendekezo langu ni kwamba, Serikali ijitahidi ifanye moja kati ya mawili au yote mawili. Moja, iwe ni sera na ikiwezekana sheria kwa kila Kampuni ya Madini iwe na utaratibu wa kuajiri Watanzania katika ajira zake kwenye ngazi zote. Pawepo na utaratibu ambao labda kwa uwiano wa aina fulani *progressively* sidhani kwamba inawezekana kwamba wanapokuja wachukue *hundred percent,* lakini *progressively* pawepo na utaratibu wa kuchukua Watanzania. Iwe ni sera ambayo inafuatiliwa kiutaratibu mpaka mwishowe Watanzania wafikie *level* fulani ya kuhakikisha kwamba tunashiriki katika uzalishaji na sisi tupate kujifunza kutokana na kazi wanayofanya na kujifunza jinsi ya kushiriki kuvuna rasilimali yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, pili, pawepo na utaratibu au sera pamoja na sheria kuhakikisha kwamba Kampuni za migodi hapa Tanzania zinashiriki na kuwekeza katika Soko la Hisa hapa Dar es Salaam. Wao wana fedha na ni nyingi, nina imani ni nyingi kiasi fulani, si kidogo kama tunavyosoma kwenye Vyombo vya Habari kwamba wana hela kiasi fulani. Soko letu la Hisa hapa Dar es Salaam limeishiwa fedha au hela zinazidi kupungua na tunaona kwamba bei zinaanza kupungua *liquidity level* inaanza kushuka. Wao ndio wanaweza kutu-*bail out.* Tunaomba tafadhali Serikali itazame kwamba ni uwezekano upi unawezekana ili hawa jamaa wa migodi washiriki, hatuwanyang'anyi hela yao ila tunawaambia tu wawekeze ili na sisi tushiriki katika hiyo shughuli yao ya migodi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine na langu la kukaribia mwisho ni kuhusu fursa hii ya *SEAMIC* ambayo kwa kweli kama walivyosema waliotangulia, bado ni kubwa. Ni fursa ambayo sisi Watanzania tusingetaka kwamba ipungue kwa kitu chochote kile. Tutaiunga mkono mia kwa mia. Tujitahidi kama Serikali tuipe nguvu, kwa sasa hivi naona kwa kuona jinsi ambavyo nasoma tangu ianze mpaka hapa ilipo *trend* yake imesuasua kidogo kwa kiasi kikubwa na inavyoelekea ni kwamba yamekuwepo matatizo kwa kiasi fulani na ninavyoona ni kwamba jitihada inayofanya Serikali sasa hivi ni kuhakikisha kwamba ni kubadilika, nguvu zinapatikana na hii *SEAMIC* inapewa

mazingira ya kuweza kuhakikisha kwamba inajipipa nguvu na kutoa *contribution* zake katika uchumi wetu na wa nchi ambazo ni *member states* wa *SEAMIC*.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono na naitakia kheri Wizara au Serikali katika utekelezaji wa hili Azimio. *(Makofi)*

**MHE. SEMINDU K. PAWA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nitaongea kwa muda mfupi kwa sababu ni Kituo cha kitaalam na hili ni Azimio. Kwa hiyo kwa kuwa Azimio lenyewe limeletwa na Waziri na sisi tulitembelea eneo lile, nilitaka kuonyesha tu *concern* ya Bunge. Baada ya kupitisha Azimio hili katika Bunge hili Tukufu, basi tutakuwa na uwezo mkubwa; kwanza, nchi kutambulika kwa sababu Makao Makuu ya nchi hizi ambazo zimesaini ni Dar es Salaam. Kwa hiyo, tutafaidika wa kwanza, tunasema kwanza sisi, wengine baadaye. Kwa hiyo, nchi kama Ethiopia, Angola na Uganda ambazo zimetajwa katika *article* ukurasa wa tatu zitafuata. Vile vile, tulikuta wanafunzi pale ambao wanachukua mafunzo ya kukata zile aina za madini na vile vile kutambua aina ya madini na zile madini feki. Kuna tabia ya watu kuuza madini feki. Lakini ipo mitambo kama aina tano ambayo haijapata kutokea katika Taasisi nyingi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kitu kilichonifurahisha, nilikuta mtambo mmoja unaitwa *Neuclear Magnetic Reasonunca* ambayo inaonyesha *quantity* ya kila kitu pale na madini gani na kuna *quality* gani na *elements* gani. Ipo *Atomic absorption* SP inaonyesha kiasi chake, *melting point* na kila kitu na madini machafu hutolewa *Isolopos*. Nikakuta kitu kinaitwa *Polaragraphy* ambayo ina-*separate* vitu vingine. Nikakuta upande wa *laboratory* vile vile kuna *Destructive Test* ambayo walitufanyia majaribio pale kama ikiwa ni almasi au dhahabu haiwezi kuwa *destroyed*. Tukakuta vile vile, vipimo mbalimbali na kuonyesha athari ya *protective area,* tukakuta upande wa *computer* ambao unaonyesha vile vile Taasisi ilivyoendelea katika teknolojia ya kisasa.

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vile tukakuta maeneo ambayo yana chumba kimoja kikubwa sana, lakini ndani mle kuna kitu kinaitwa *Flormeter* na mambo mengine mengine haya ya *SP Spectroscope* ambazo zinaonyesha aina ya mitambo ya kutambua madini ambayo hata ikiwa kwenye mchanga unaweza kuchambua.

Lakini jambo lilifurahisha ni kwamba, nao watengenezaji wanatengeneza vifaa kama vikombe vya aina ya *ceramic*. Hii teknolojia ni nzuri. La msingi baada ya kupita ni kwamba Kituo hiki kisiwe kinatambulika tu katika makaratasi. Nawatangazia Watanzania kupitia Bunge hili kwamba sasa kama una jiwe lolote ambalo una wasiwasi nalo au unalitambua kwamba hii ni aina fulani ya madini na mali, basi peleka *SEAMIC*. *SEAMIC*, Dar es Salaam ambapo ukidhani Waheshimiwa Wabunge watakuwa watumishi wakubwa kuwaambia Watanzania hii ni moja katika upande wa *MKUKUTA* na huo ambao tulikuwa tumeupitisha siku ile.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa yapo mawe kwa mfano maeneo ya Jimbo letu katika maeneo ya Mwalazi kule, watu wanadhani rubi ni kitu cha thamani kweli. Kuna watu ambao wanakaa na mawe ya thamani, wanalima shambani, wanakuta mawe ambayo yana dhahabu, lakini anakaa nalo nyumbani kwa sababu hawezi kutambua. Sasa

*SEAMIC* ni mkombozi, atakuwa ameleta ukombozi mzuri tu. Kilichobakia ni kwamba Wizara kitumieni vizuri kwa sababu kipo kwetu msiwe na tabia ya muwa. Kwamba mahali pale karibu ambapo pana majani ambapo hutengeneza sukari siyo patamu, utamu unakuwa mbali. Sasa naomba muache tabia hiyo, kitumieni ninyi wenyewe semeni sisi kwanza wengine baadaye. *(Kicheko)*

Kwa hiyo kituo kile kitumieni vizuri sana na sasa Tanzania tuache utoto, kwa sababu watoto huacha tabia baada ya makuzi. Zipo tabia ambazo mtoto anafanyiwa mambo mazuri lakini analalamika, analia wakati anataka kuoga kwa usafi wake mwenyewe, analia hata wakati wa kula. Sasa tumepata kituo hiki, tukitumie kutusaidia. Kwa utaratibu huu, basi nadhani *SEAMIC* itakuwa mkombozi wa Tanzania. Naomba tuliridhie Azimio hili. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru na naunga mkono Azimio hili. *(Makofi)*

**MHE. GWASSA A. SEBABILI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi. Kwanza naomba nitangulie kwa kuishukuru Wizara kwa kuleta Azimio hili na kusema kweli ni kwamba Azimio hili limechelewa sana hata kama limeanza miaka hii miwili iliyopita, lakini limechelewa mno.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuridhia Azimio hili kutatusaidia sana kupunguza matatizo mengi tuliyokuwanayo katika eneo hili la madini. Kwanza wataalam wetu wengi sana walioanza katika uchimbaji wa madini nchini humu hawamo katika nchi yetu. Hivi karibuni nilikuwa Botswana wataalam wengi walioanza na Mwadui wote wapo kule na ni mabosi wakubwa sana ndio wana-*master* shughuli zote za madini hasa machimbo ya almasi katika nchi ile. Naamini tutakapokuwa tumefikia hapo pengine Kituo hiki kitatusaidia kuwaita watu kama hawa kuja kuendesha shughuli za madini katika nchi yetu tunaweza kuwa na watu ambao wanaweza kusimamia maendeleo ya uchimbaji wa madini au hata kuyauza.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini pia kuwa na Kituo hiki kutatusaidia kuondoa huu ukiritimba wa kuuza madini yetu nje wakati mwingine hata bila kuandaliwa vizuri. Pia, naamini hii itatusaidia kupunguza matatizo ya kupeleka michanga yetu. Kama tunavyokumbuka, miaka michache matashari yalizama kule Tanga yakiwa yanapeleka michanga yetu kutoka Bulyankhulu kwenda Japan. Kwa hiyo, uwezekano wa kuomba Wahisani kwa sababu tutakuwa tuna umoja wa nchi nyingi kuweza kutujengea kiwanda kama hicho kwa kufanya uchambuzi mzuri, naamini itakuwa ni nafuu zaidi. Michanga hii inapokwenda nje hatujui kinachokwenda huko na wala hatujui kama tunachorudishiwa ni kile ambacho tulikuwa tunategemea.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la kwamba nchi za Rwanda, Burundi na *Congo* nao wanaomba kuingia ni suala la kupongeza sana, tunakuwa tumefunguliwa nafasi ya kwenda Magharibi zaidi ya nchi yetu. Mikoa ya Magharibi ya nchi hii kusema kweli ina madini mengi ambayo hayajaweza kutambulika na hasa kuchimbwa. Kwa hiyo, inapokuwa nafasi imepatikana ni pamoja na kuwavuta tena Wawekezaji ambao

watusaidie katika shughuli hii na pia watatusaidia kuanzisha miradi mingine ya kimaendeleo na hivyo kuinua maendeleo ya wananchi wetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi nasema kweli Azimio hili ni muhimu sana, nami moja kwa moja naunga mkono kwamba lipite na kazi ianze mapema sana. Ahsante. *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote napenda nichukue nafasi hii kuwashukuru Waheshimiwa Wabunge wote waliochangia kwa kuunga mkono hoja hii na napenda nichukue nafasi hii kuwatambua kwa majina. Kwanza, Mheshimiwa Herbert Mntangi, ambaye amemwakilisha Mwenyekiti wa Kamati, Mheshimiwa Isaac Cheyo, kwa upande wa Upinzani, Mheshimiwa Mbarouk Mwandoro, Mheshimiwa Profesa Talala Bana Mbise, Mheshimiwa Semindu Pawa na Mheshimiwa Gwassa Sebabili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sikupata michango ya maandishi. Kwa hiyo, hawa niliowataja ndio waliochangia na kama nilivyosema, awali nawashukuru sana kwa michango yao na kwa kuunga mkono Azimio hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kama ambavyo imeonyeshwa katika ratiba iliyogawiwa leo na tarehe 30 mwezi huu tutakuwa na Semina ya kupitia au kujadili Taarifa ya Tume ya Kipokola, Tume ambayo Mheshimiwa Waziri Mkuu aliiunda katika kutathmini suala zima la madini, ni imani yangu kwamba wakati wa Semina ile tutapata fursa nzuri zaidi ya kujadili na kubadilishana mawazo kama ilivyo kawaida yetu kuhusu suala la madini. Kwa hiyo, nisingependa kuchukua muda mrefu kujibu kila lililozungumzwa hapa na kwa hakika kama tulivyoona yote yaliyozungumzwa ni mazuri, yote yamezungumzwa kwa nia njema ya kuunga mkono hoja na kuboresha kwa upande wa Serikali. Lakini kuna machache ambayo nadhani ni vizuri nikayatolea maelezo.

Kwanza kabisa napenda niungane na Kamati, sio tu kwa kuunga mkono, lakini pia kwa sababu walizotoa kwa kuunga mkono hoja hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pili, napenda nizungumzie masuala ambayo ameyazungumza Mheshimiwa Isaac Cheyo, Mheshimiwa mtani wangu, hayupo hapa sasa hivi. Kwanza, kabisa lile lingine alilolisema kwa kweli halikuhusiana sana la hii habari ya umeme na *Net Group* na mimi sijui pia sababu zilizotokea sasa hivi. Kwa hiyo, ningependa nisiliguse hilo la kukatikakatika kwa umeme, ni kadhia ambayo hata na sisi tumeiona, lakini sina maelezo yake kwa sasa hivi.

Lakini nataka nije kwenye yale aliyoyachangia kwenye hoja. Amezungumzia juu ya Sheria zetu za Madini kuwa zimepitwa na wakati. Napenda nichukue nafasi hii niseme kwamba, si kweli kwamba Sheria zetu zimepitwa na wakati kiasi hicho. Si kweli kwa sababu hizi nchi alizozitaja kwamba eti zimepitwa na wakati na kwamba kuna nchi nyingine zilizo wanachama, hizi nchi zinakuja Tanzania kujifunza juu ya suala la madini kwa kuona sera yetu na sheria yetu. Hivi karibuni tu tulikuwa na ugeni wa Waziri wa Madini wa kutoka Ethiopia ambaye amekuja Tanzania kujifunza na wanatusifu kwa

sheria yetu nzuri na jinsi tulivyoweza kuwashawishi Wawekezaji katika miaka michache iliyopita tangu mwaka 1998 ilipopitishwa sheria hii hadi sasa na kuweza kuchipukia sana katika Sekta hii ya Madini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa mimi sisemi kwamba hatuna matatizo ya hapa na pale. Hii ni sekta mpya iliyochipukia, lazima katika muda fulani tutakaa tujadiliane tuone yapi yanaweza kurekebishika na ndio maana basi Serikali kwa kutilia maanani hata Waziri Mkuu akaunda Tume ya Kipokola kuhakikisha kwamba tunapitia baadhi ya mambo.

Pia, kwa sababu hiyo hiyo na kuzingatia umuhimu wa mambo mengi ambayo Waheshimiwa Wabunge walikuwa wanayasema humu kwamba ipo Semina tutakayoweza kuzungumzia au kujadili taarifa hizi, lakini si kweli kwamba Sheria ya Madini imepitwa na wakati.

Mheshimiwa Naibu Spika, la pili ambalo amelizungumzia ni kwamba wazawa hawanufaiki kwa maana ya wananchi kwa ujumla wote hawanufaiki. Sekta hii ya madini sasa hivi kwa upande wa wachimbaji wadogo wadogo, karibu Watanzania milioni moja wanategemea kwa maisha yao ya kawaida katika Sekta hii ya Madini. Sasa si kweli kwamba mtu anasema kwamba hii hainufaishi kabisa. Lakini sio hivyo tu, hata katika haya Makampuni makubwa yaliyoingia nchini na sasa hivi yapo karibu sita, haya Makampuni yamefanya pia kazi kubwa hata katika maeneo ambayo haya Makampuni yapo.

Kwa hiyo, kama nilivyosema awali, si kwamba kila kitu kimekwenda bila kuwa na matatizo madogo madogo ya hapa na pale. Lakini ukichukulia muda ambao Sera ya Madini imewekwa mwaka 1997 na Sheria ya Madini mwaka 1998, ni muda mdogo kwa kweli katika maisha ya ukuzi wa ukuaji wa Sekta ya Madini na katika muda huu Serikali yetu na nchi hii imefanya mambo makubwa katika Sekta ya Madini na Sekta ya Madini imechipukia sana na imechangia kwa kiasi kikubwa katika ukuaji wa pato la Taifa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine ambalo ningependa nilitolee kauli pia amelizungumzia Mheshimiwa Cheyo ni kusema kwamba, wachimbaji wa *tanzanite* hawawezi kuuza *tanzanite* hii mpaka wauze kupitia Kampuni moja kubwa ya hapa nchini na nadhani pengine alikuwa anaizungumzia *Tanzanite One* au zamani ilikuwa ikiitwa *AFGEM*. Pia akasema hivyo hivyo kwa almasi.

Mimi niko tayari kukaa na mtani wangu kuweza kumpa taarifa zaidi baadaye pengine labda hafahamu, lakini haya si ya kweli. Nikija kwenye almasi ambayo inatoka kwa watani zangu Wasukuma, kule Shinyanga kuna Kampuni moja imechipukia ya mchimbaji Mtanzania *El-Hilary Minerals* ambayo imeingia katika Sekta ya Uchimbaji wa Almasi na haitegemei kuuza almasi yake kupitia kwa *Williamson Diamond* na kadhalika. Ukija kwenye hao watu wanaochimba *tanzanite*, nadhani Waheshimiwa Wabunge wengi wanafahamu kwamba kuna wachimbaji wadogo wadogo wengi ambao

wanauza almasi yao moja kwa moja kwenye masoko ya nchi za Asia, Ulaya na Marekani na si kweli kwamba hii *tanzanite* haiwezi kuuzwa mpaka ipitie kwenye Kampuni moja tu.

Mheshimiwa Naibu Spika, niliona haya niyatolee kauli kwa sababu yanapotosha Umma na ni vizuri wananchi wakaelewa ukweli wa mambo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mengine ambayo yamezungumzwa ambayo pengine ni vizuri nikayatolea kauli ni hili la uwekaji wa hisa kwenye soko la hisa ambalo amelizungumza Mheshimiwa Profesa Talala Bana Mbise. Ni jambo zuri, lakini napenda niseme kwamba Kampuni hii ya *AFGEM* ambayo ilikuja hapa Bungeni na ikasema ingependa iwekeze katika soko la hisa na sasa hivi Kampuni hii inaitwa *Tanzania One*, wao walifanya jitihada zote za kutaka kufanya hivyo. Hatuwezi kuwalaumu wao na kwa kweli hakuna mtu wa kumlaumu kwa sababu uwekezaji katika soko la hisa una taratibu zake na wenzetu wa soko la hisa nadhani wameona pengine muda bado haujafikia kwa Kampuni hii kuweza kuwekeza. Lakini bado Kampuni hii inaendelea na taratibu na inaendelea kujaribu kufuata masharti ili wawekeze katika soko hili la hisa na kuweza kuuza hisa hizi kwa Watanzania wengine. Kwa hiyo, hili nalo niliona bora nilifafanue.

Mheshimiwa Naibu Spika, mengine kama ambavyo yamezungumzwa hapa ni kama nilivyosema awali ni mambo ambayo kwa ujumla yameunga mkono Azimio hili. Kama nilivyosema baada ya Mheshimiwa Cheyo alikuja Mheshimiwa Mbarouk Mwandoro, ambaye amezungumzia umuhimu wa Kituo hiki na kwamba nchi nyingine zishawishiwe na tunakubali ushauri wake na ndivyo tunavyofanya. Mengine amezungumza Mheshimiwa Talala Bana Mbise juu pia ya umuhimu wa Chuo hiki na juu ya kuajiriwa kwa Watanzania, ni kweli kwamba Makampuni haya hayana *program* ya kuajiri Watanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, itachukua muda mpaka Watanzania wengi kuweza kushika nafasi za juu, lakini kwenye ngazi za Uhandisi wanajitahidi kuchukua Watanzania. Tunapokea ushauri huu kwa Wizara na Serikali kwa ujumla kuendelea kuwasisitizia wenye Makampuni haya kuhakikisha kwamba idadi kubwa ya Watanzania inaendelea kuajiriwa katika ngazi mbalimbali kulingana na aina ya kazi kwa sababu baadhi ya kazi hizi zinahitaji utaalam fulani. Lakini Makampuni haya pia yanatoa fedha maalum za mafunzo kwa Watanzania kila mwaka, fedha maalum za mafunzo za Wahandisi wetu na wataalam wengine kuhakikisha kwamba wataalam wetu wanapata utaalam unaotakiwa ili wanaporudi waweze kutumikia nchi yetu katika maeneo mbalimbali ikiwemo katika migodi inayowekezwa hapa nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia namshukuru Mheshimiwa Semindu Pawa ambaye amezungumzia habari ya umuhimu wa Kituo hiki kama Wabunge wengine na akatupa uzoefu wake wa vifaa vingi ambavyo amevikuta pale na yeye kama Mkemia tunayemfahamu wa zamani anatukumbusha baadhi ya vifaa ambavyo amevikuta pale.

Pia ametoa wito kwa Watanzania wapeleke mawe yao pale na mimi namuunga mkono hivyo kwamba ni muhimu tutumie Taasisi tulizokuwa nazo. Kuna *SEAMIC* Dar es Salaam, kuna Chuo cha Madini, Dodoma, lakini pia kuna *Tanzania Geological Survey* iliyopo hapa kwenye majengo ya Wizara ya Nishati na Madini na wao pia wana Maabara. Kwa hiyo, nadhani ni muhimu tupeleke mawe pale, lakini tufahamu pia kwamba katika

kupeleka mawe kuna ada kidogo inatozwa.  Kwa hiyo, tusidhani kwamba tunapeleka tu hayo mawe, hapana.  Kuna ada kidogo inatozwa na ni muhimu ada hii ikalipwa ili kuhakikisha kwamba Taasisi hizi zinafanya kazi inavyotakiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, namshukuru pia Mheshimiwa Gwassa Sebabili, alipozungumzia juu ya wataalam ambao wapo nje.  Kwa upande mmoja ni vizuri pia Watanzania nao wakawa na fursa ya kwenda sehemu mbalimbali na hasa hizi nchi ambazo Mheshimiwa amezitaja ni nchi za umoja wa *SADC* na nchi nyingine, ni vizuri wakaenda wakapata uzoefu.  Lakini nadhani alichokuwa akizungumzia ni kwamba hapo baadaye pengine na hawa wanaweza kurudi wakaendelea kushughulika hapa nchini. Wanakaribishwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu mchanga unaokwenda Japan, niseme kwa uchache tu kwamba najua ni jambo ambalo tumelitolea ufafanuzi mara nyingi Bungeni. Lakini niseme kwa uchache tu kwamba, Chuo au Kituo hiki hakihusiki moja kwa moja na suala la kupeleka mchanga Japan.  Mchanga unaohitajika ili kujengwa kiwanda au *smelter* kwa uchache kabisa ni tani laki moja na nusu.  Kiwango kinachotolewa sasa ni karibu tani 24,000 na ndio tatizo.

Lakini hoja yake Mheshimiwa Gwassa Sebabili, ina umuhimu na kwa kuwa sasa hivi nchi zipo pamoja, basi huenda ikatoa fursa hapo baadaye, tukaweza kushawishi nchi au Wawekezaji wengine wakaweza kuanzisha kiwanda na kuendelea kuchipukia kwa Sekta hii ya Madini, itaweza kuzalisha mchanga mwingi zaidi na kutokana na mchanga mwingi zaidi tuweze kupata kile kiwango kinachotakiwa kwa ajili ya ujenzi wa kiwanda. Kwa maana hiyo au kwa maana ya hoja ya aina hiyo, nakubaliana kabisa na Mheshimiwa Gwassa Sebabili.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kuyapitia haya, napenda nirejee kuwashukuru sana Waheshimiwa Wabunge wote kwa michango yao waliyoitoa kwa hotuba.  Pia, napenda nichukue nafasi hii basi, kwa mara nyingine tena kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Nishati na Madini kuliomba Bunge lako Tukufu likubali na liridhie Mkataba huu wa Wanahisa wa Chuo cha *SEAMIC* ili tuweze kuziendeleza nchi zetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa hoja.  *(Makofi)*

Azimio la Kuridhia Makubaliano ya Nchi Wanachama wa *Southern and Eastern Africa Mineral Centre*
*(SEAMIC)* kuhusu Mkataba wa Wanahisa wa *SEAMIC uliridhiwa na Bunge*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge hapo ndipo tumefika mwisho wa shughuli za leo kama mlivyopata ratiba ambayo ilitolewa na Mheshimiwa Spika leo asubuhi.  Kwa hiyo kutokana na ratiba hiyo, sasa naahirisha shughuli za Bunge mpaka Alhamisi, tarehe 28 Aprili, 2005, saa tatu asubuhi.

**WABUNGE FULANI:** Kesho tunakuja saa tatu?

**NAIBU SPIKA:** Kama nilivyosema, mimi ndio naongoza Kikao hapa. *(Kicheko/Makofi)*

Kama mtu anataka kuja saa Tatu kesho au Jumatatu aje. Kwa hiyo, naahirisha kama nilivyosema mpaka tarehe 28 Aprili, 2005, siku ya Alhamisi, saa tatu asubuhi.

*(Saa 1.30 usiku Bunge liliahirishwa Mpaka Siku ya Alhamisi Tarehe 28 Aprili, 2005 Saa Tatu Asubuhi)*